Nipashe
Alhamisi Januari 2, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580117
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## Polisi adaiwa kukatwa sehemu za siri na mkewe

UKURASA 3


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Viini pori vya mazao vyatafutwa kustahimili janga la tabianchi
2020: Ethiopia, Sudan na Misri kuafikiana ya Nile?
Nyuki mkubwa zaidi duniani agundulika
OFISI YA DAWATI LA JINSIA NA WATOTO SERENGETI
JANGA LA UKEKETAJI
UNFPA: Ukiwaona mabinti 10, uwezekano mmoja yamemfika

UKURASA 13

# Magufuli: Nitaendelea kutumbua majizi 2020

• **Maaskofu** waonya ulaji fedha Ukimwi, uchaguzi mitaa; Shein: Amani, utulivu...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**JENEZA LAZUA TAHARUKI SOKONI**
WANANCHI wa eneo la Soko la Soweto wameuanza mwaka kwa taharuki ya...

UKURASA WA 5
**WAZIRI KIGWANGALLA ADAI KUMALIZANA KATIBU**
SIKU moja baada ya Rais John Magufuli, kutoa siku tano kwa Waziri wa Maliasili...

UKURASA WA 5
**MAWAKILI BINAFSI WABANWA KUTOZA FEDHA**
SERIKALI imewapiga marufuku baadhi ya wanasheria Mkoa wa Morogoro...

## Makusanyo Desemba yavunja rekodi TRA

UKURASA 3



Wananchi na wafanyabiashara wa Soko la Soweto jijini Mbeya, wakijiandaa kufunua jeneza lililokutwa limetelekezwa sokoni hapo jana na kuzua taharuki. **PICHA: NEBART MSOKWA.**


Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

RIPOTI MAALUMU

## Vyoo duni vinavyokwaza elimu kwa watoto wa kike

UK. 4

MICHEZO **SIMBA YAFUNGUKA KUUZWA STRAIKA** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Magufuli: Nitaendelea kutumbua majizi 2020

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, amesema mwaka 2020 ataendelea kutumbua majizi yote, na fedha atakazozipata atazipeleka kwenye miradi ya maendeleo.

Aidha, alitaja miradi hiyo kuwa ni ununuzi wa ndege, kujenga reli na elimu bure, huku akitaka Watanzania kudumisha amani na upendo ili uwe mwaka wa maendeleo na ustawi kwa taifa.

Kwa mujibu wa salamu za Mwaka Mpya kwa Watanzania zilizopo kwenye taarifa kwa vyombo vya habari, Rais Magufuli alisema, serikali itaendelea kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma ili iendelee kutekeleza miradi ya maendeleo yenye manufaa kwa wananchi.

Alitoa salamu hizo jana, wakati akiagana na maofisa na askari wa wanyamapori na Hifadhi ya Misitu wa Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo ambako alitembelea na kujionea vivutio vya utalii pamoja na wananchi wa Nyabugera na Muganza aliowasalimu wakati akiwa njiani kurejea nyumbani kwake Chato.

"Nchi hii ilikuwa inaliwa sana na majizi na mpaka sasa bado wapo, namwomba Mwenyezi Mungu aendelee kunipa uhai ili katika mwaka 2020 niendelee kuwatumbua majizi wote na fedha tutakazopata tuzipeleke kwenye miradi ya maendeleo kama ambavyo tumenunua ndege 11, tunajenga reli (standard gauge), tunatoa elimu bure na mengine mengi," alisema.

Aidha, Rais amemwonya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Eliud Mwaiteleke, kwa matumizi mabaya ya fedha yanayofanywa na halmashauri hiyo na ametaka dosari hizo zirekebishwe mara moja.

"Nataka ujirekebishe, wananchi hawa wanateseka sana," alisisitiza.

Baada ya kuvuka Ziwa Victoria kwa kivuko cha MV Chato, Rais Magufuli alikutana na wananchi wa Kasenda na kuelezea kutoridhishwa kwake na ukusanyaji wa mapato ya soko la dagaa na samaki la Kasenda baada ya kuelezwa kuwa makusanyo ya mapato ya soko hilo ni Sh. 500,000 kwa siku licha kuwa soko kubwa la pili kwa kuuza dagaa katika ukanda wa Ziwa

INAENDELEA UK. 26



Rais John Magufuli na mkewe Janeth Magufuli, wakiwa wameshika samaki aina ya sangara waliovuliwa Ziwa Victoria walipofanya ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo wilayani Chato, mkoani Geita juzi. **PICHA: IKULU**

# Maaskofu waonya ulaji fedha za Ukimwi, uchaguzi S/Mitaa

**Na Waandishi Wetu**

MAASKOFU wametoa ya moyoni kuhusu upigaji wa fedha za Ukimwi na wapinzani kususia uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika Novemba 24, mwaka jana.

Viongozi hao waliyasema hayo kwa nyakati tofauti kwenye ibada za mkesha wa Mwaka Mpya 2020.

Askofu wa Jimbo Katoliki la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, alionya tabia ya watu kupenda kujinufaisha kupitia matatizo ya wengine, ikiwamo kutafuna misaada ya watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi.

Alisema mwaka 2020 ni wa kujali watu wenye matatizo na kuwapatia faraja, wakiwamo wanaoishi na VVU na kuacha pia tabia ya kuwanyanyapaa, pamoja na kutafuna misaada yao ambayo hupewa na wahisani mbalimbali.

Katika ibada hiyo katika Kanisa Kuu la Mama Mwenye Huruma Parokia ya Ngokolo Shinyanga Mjini, alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya watu nchini kupenda kujinufaisha wenyewe kupitia matatizo ya watu wengine, ikiwamo kutafuna misaada ya wanaoishi na VVU ambayo hupewa na wahisani mbalimbali.

"Tunapoukaribisha mwaka 2020 uwe mwaka wa kusameheana, tutende mambo mema, tuache maovu, tusaidie watu wenye uhitaji na matatizo, tuache kuwanyanyapaa wagongwa wa Ukimwi na wakati mwingine hata misaada ambayo hupewa na wahisani imekuwa haiwafikii walengwa wenyewe na kuishia kutafunwa," alisema Askofu Sangu.

"Pia tuwasaidie wajane na yatima, ambao nao wamekuwa wakidhulumiwa haki zao ikiwamo mirathi ambayo huachiwa na wapendwa wao pale wanapokuwa wametangulia mbele za haki, na kuacha kuwatenga ikiwa sisi sote ni ndugu ambapo tumeumb

INAENDELEA UK. 8

# Malezi watoto yatakiwa, manabii waongo waonywa

**Na Waandishi Wetu**

MAASKOFU na viongozi wa serikali wamewataka Watanzania kudumisha amani na upendo kwa kuzingatia malezi ya watoto, kuacha kuamini manabii wa uongo ili kuepusha mvurugano kwenye jamii.

Viongozi hao walitoa rai hiyo kwa nyakati tofauti wa kati wa ibada za mkesha wa mwaka mpya wa 2020 kwenye mikoa ya Kagera, Dodoma na Tanga.

Mkoani Kagera, Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki la Bukoba, Askofu Desderius Rwoma, aliwaka wananchi wa mkoa huo kujali malezi ya watoto ili wakue wakiwa na maadili mema na hofu ya Mungu.

Askofu Rwoma pia aliwataka wananchi kujitokeza kuwekeza kwa lengo la kuongeza vitega uchumi ili kuongeza kipato cha familia, mkoa na taifa kwa ujumla.

**RC ALILIA MAUAJI**

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, aliwataka wakazi wa mkoa huo kudumisha upendo, ili kukomesha mauaji ya mara kwa mara yanayotokea katika jamii.

Alisema kuwa vitendo vya mauaji vinavyoendelea mkoani Kagera haviwezi kuondolewa kwa kutumia mbinu za kijeshi au kwa kutumia dola, lakini watu wakipendana na kuthaminiana vinaweza kupungua.

Alisema, Kagera inakabiliwa na changamoto kubwa ya mauaji ngazi ya jamii na kuwa kila siku yanaripotiwa ya mtu mmoja au zaidi, na kutaja chanzo chake kikuu kuwa ni migogoro ya ardhi, mirathi na wivu wa kimapenzi.

Gaguti alisema kuwa vifo hivyo vinatokea ndani ya jamii, kwa kaka kumuua dada, mtoto kumuua baba, na kuwa sio rahisi kuvizuia kwa kutumia bunduki na anaamini upendo pekee kwenye jamii ndiyo utaepusha majanga hayo.

**DODOMA ASKOFU AONYA**

Askofu wa Jimbo Kuu Katoliki Dodoma, Beatus Kinyaiya, amewataka wakristo waliokengeuka kurudi katika mstari ulionyooka na kuacha kukimbilia manabii wa uongo wanaopotosha maneno yaliyo katika Biblia Takatifu.

Alisema hakuna sababu ya kuwafuata manabii wa uongo kinachotakiwa ni kujitathmini wao wenyewe na kurejea katika mstari ulionyooka.

"Sioni sababu ya kukimbilia kwa manabii wa uwongo sali ukiomba Mungu ili akutimizie kile ulichomwomba," alisema Askofu Kinyaiya.

**MWINJILISTI ALILIA AMANI**

Wilayani Muheza mkoani Tanga, Watanzania wametakia kuendeleza upendo, amani na mshikamano ili kuleta maendeleo katika familia zao na nchi kwa ujumla kwani bila kufanya hivyo kutakuwa hakuna maendeleo yeyote.

Mwinjilisti wa Kanisa la KKKT Usharika wa Muheza Mjini, Aminiel Dhahabu, aliyasema hayo jana katika ibada ya Mwaka Mpya.

Alisema kuwa lazima Watanzania wapendane kwa kuwa madhehebu yote nchini yanalenga kuleta amani.

**Imeandikwa na Renatha Msungu, DODOMA, Lilian Lugakingira, BUKOBA na Steven William MUHEZA**



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni (kulia), akifuatilia uingizwaji wa taarifa za wananchi waliotoka sehemu mbalimbali mkoani Morogoro na kufika Ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), zilizopo eneo la Tungi-Mfuruni mkoani hapo, ikiwa ni mwendelezo wa zoezi la kujipatia kitambulisho hicho kwa wananchi nchini kote. Wa pili kulia ni Ofisa Usajili wa NIDA Mkoa wa Morogoro, James Malimo. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# Jeneza lazua taharuki sokoni

**Na Nebart Msokwa,**

MBEYA

WANANCHI wa eneo la Soko la Soweto wameuanza mwaka kwa taharuki ya aina yake baada ya kuamka asubuhi siku ya mwaka mpya na kukuta jeneza tupu likiwa limetelekezwa juu ya meza nje ya duka katika eneo hilo.

Tukio hilo limekuwa la tatu kutokea katika miaka ya karibuni baada ya mwaka juzi kutokea matukio mawili ya ajabu, la kwanza likiwa la wananchi wa eneo la Isanga kuusahau mwili wa marehemu ndani na kwenda kuzika sanduku peke yake na waliporejea nyumbani kuukuta mwili ndani.

Tukio hilo lilizua taharuki na baadhi ya wananchi walihusisha na imani za kishirikina na kabla hilo halijapoa lilitokea tukio lingine katika eneo la Shigamba baada ya mwanamke mmoja kufukua mwili wa mwanaye aliyekuwa amezikwa na kuurejesha nyumbani kisha kuanza kuombea kwa madai kuwa angefufuka.

Tukio lililofungua mwaka 2020 la kutelekezwa jeneza sokoni, limeibua maswali miongoni mwa wananchi.

Baadhi ya wananchi walioshuhudia tukio hilo walisema kuwa jeneza hilo lilikuwa limetumika na wana wasiwasi kuwa aliyefanya tukio hilo ni mtu anayejihusisha na imani za kishirikina.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Oscar Kilasi, ambaye ni miongoni mwa wafanyabiashara wa soko hilo, alisema aliwahi asubuhi sokoni hapo

INAENDELEA UK.8

# Polisi adaiwa kukatwa sehemu za siri na mkewe

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamshikilia Flora Adamu (23), mkazi wa Shinyanga Mjini, kwa tuhuma za kumkata mumewe sehemu za siri, ambaye ni askari Polisi mwenye Namba H, 8980 Pc Kazimiri, kwa madai ya kumtuhumu kutokuwa muaminifu katika ndoa.

Imeelezwa kuwa mtuhumiwa huyo alimtuhumu mumewe kuwa ana nyumba ndogo. Alizungumza na wanahabari, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Deborah Magiligimba, alisema tukio hilo limetokea Desemba 28 mwaka jana, majira ya saa 6:30 usiku wakati wanandoa hao wakiwa wamelala.

Alisema wakiwa wamelala, ghafla Flora aliamka na kuanza kumnyatia, huku akiwa ameshika kitu chenye ncha kali kisha kumkata mumewe sehemu za siri na kumjeruhi vibaya.

"Baada ya askari huyu kukatwa uume wake alikimbizwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga ili kupatiwa matibabu ya haraka, ambapo alilazwa kwa muda wa siku mbili kisha kuruhusiwa kurudi nyumbani kuendelea kujiuguza kidonda," alisema Kamanda Magiligimba.

"Chanzo cha tukio hilo ni wivu wa kimapenzi, ambapo mwanamke alikuwa akimtuhumu mume wake kuwa ana nyumba ndogo, ndipo akaamua kuchukua kitu chenye ncha kali kisha kuanza kuukata uume wa mumewe na kumjeruhi vibaya," aliongeza.

Aidha, kamanda huyo alisema Jeshi la Polisi linamshikilia mwanamke huyo, na kwamba uchunguzi ukikamilika, atafikishwa mahakamani.

# Makusanyo ya Desemba yavunja rekodi ya TRA

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imevunja rekodi kwa kukusanya jumla ya Sh. trilioni 1.987 kwa mwezi Desemba, mwaka jana, mapato ambayo hajawahi kukusanywa tangu kuanzishwa kwake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, jijini Dar es Salaam, Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede, alisema makusanyo hayo ni sawa na asilimia 100.20 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2018.

Alisema lengo la mwaka 2018 lilikuwa Sh. trilioni 1.983 na zilikusanywa Sh. trilioni 1.628, ikiwa ni ongezeko la asilimia 22.05 kwa robo ya mwisho ya mwaka jana.

Kwa mujibu wa Dk. Mhede, rekodi hiyo imevunjwa ikilinganishwa na ya mwezi Septemba mwaka jana kwa Mamlaka kukusanya Sh. trilioni 1.767 sawa na asilimia 97.20 kutoka lengo la Sh. trilioni 1.817.

Vilevile, alisema makusanyo hayo yanamaanisha kuwa kwa miezi miwili, Novemba na Desemba, zimekusanywa Sh. trilioni 4.972 sawa na asilimia 97.49 ya lengo la Sh. trilioni 5.100.

"Makusanyo haya ni sawa na ukuaji wa asilimia 19.78 ikilinganishwa na kipindi kama hiki kwa robo ya pili ya mwaka 2018/19 zilikusanywa Sh. trilioni 4.151 ikiwa ni sawa na asilimia 87.59 kutoka lengo la kukusanya mapato ya Sh. trilioni 4.739 kwa kipindi hicho," alifafanua.

Alisema makusanyo ya mwezi Oktoba yalikuwa ni Sh. trilioni 1.484 sawa na asilimia 93.98 na Novemba Sh. trilioni 1.501 sawa na asilimia 97.59, hiyo ikiwa ni kutoka malengo

INAENDELEA UK. 8


**Pakistan Navy Ships "PNS ASLAT" and "PNS MOAWIN" to Visit Dar es Salaam Port from January 3-6, 2020**




Two Pakistan Navy ships PNS ASLAT and PNS MOAWIN will be paying goodwill visits to the Port of Dar es Salaam, United Republic of Tanzania, from January 3-6, 2020. The visit is part of similar goodwill visits and training cruises undertaken to the ports of some other friendly countries in Africa in recent weeks.

The two PN Ships are led by Commodore Abdul Munib SI(M), Commander 25th Destroyer Squadron, Captain Shafiq ur Rehman, TI(M), Commanding Officer, PNS ASLAT and Captain Muhammad Zeshan Nabi Sheikh, Commanding Officer, PNS MOAWIN.

The four-day visit will cover a host of activities including meetings and courtesy calls by the Pakistan Navy Officers on high-ranking officials of Tanzanian People's Defence Forces. The hallmark of the visit is PNS MOAWIN's 'Free Medical Camp for the Needy' during its stay in Dar es Salaam.

The Charge d' Affaires of Pakistan, Mr. Muhammad Saleem, High Commission for Pakistan, Dar es Salaam, will host a reception in honour of Pakistan Navy officers, Tanzanian dignitaries and high ranking civil and defence forces officers of the United Republic of Tanzania. The Commander and officers of PN Ships will also host a reception on board the Ship.

The forthcoming goodwill visit, in the beginning of new year 2020, is a landmark in the broader framework of further augmenting the close and cooperative ties between the Armed Forces and Navies of Pakistan and Tanzania as part of strengthening bilateral relations in diverse fields. The visit will provide an opportunity to the two Navies to share professional experience and discuss future prospects of cooperation for their mutual benefit.

**Pakistan High Commission, Dar es Salaam**

RIPOTI MAALUM

# Vyoo duni vinavyokwamisha elimu kwa watoto wa kike

**Na Renatha Msungu,**
MANYARA

USHUHUDA wa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Geita, Upendo Peneza, kuhusu wasichana kulazimika kutohudhuria shuleni kipindi wanapokuwa katika siku zao umejidhihirisha Shule ya Sekondari Ayalagaya, wilayani Babati mkoani Manyara, ambayo imekuwa na tatizo la utoro kwa muda mrefu kabla ya kutatuliwa mwaka jana.

Mwaka 2018, mbunge huyo aliwasilisha kwa Spika Job Ndugai, maombi ya kuwasilisha hoja binafsi bungeni kuitaka serikali itoe taulo za kike kwa wanafunzi wote wa shule za msingi na sekondari nchini bila malipo, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wake wa kutoa elimu bure kuanzia shule za awali hadi kidato cha nne.

Katika kujenga hoja yake, Upendo alisema mabinti wengi wamekuwa wakilazimika kutohudhuria shuleni kutokana na kukosa vifaa hivyo muhimu wakati wa hedhi, huku mazingira ya vyoo vya shule nayo yakiwa si rafiki kwao.

Hata hivyo, Spika Ndugai alizuia hoja hiyo kuwasilishwa bungeni, akiagiza ifanyiwe kazi na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

NI sura nyingine ya vikwazo vinavyoikabili sekta ya elimu nchini huku awali kukitolewa taarifa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwamba kuna uhaba mkubwa wa samani na miundombinu katika shule mbalimbali nchini, hali inayosababisha wanafunzi kufanya vibaya kwenye masomo yao.

Katika ripoti yake mwaka 2015/16, CAG alisema hali ni mbaya zaidi katika shule za msingi kutokana na miundombinu na samani zake kutokuwa katika hali nzuri na kutokidhi matakwa ya viwango vya ubora.

CAG alibainisha kuwa ukaguzi wake ulibaini udahili wa wanafunzi umeongezeka, lakini miundombinu ikiwa ovyo na isiyoendana na idadi ya wanafunzi.

Alisema hali ya ukaaji dasarani kwa shule za serikali ni ya wastani wa wanafunzi 77 badala ya 40 katika darasa moja inavyotakiwa kisera.

CAG alisema huduma za choo nazo ni tatizo, akibainisha kuwa wakati kiwango kinachotakiwa kisera ni wanafunzi wa kiume 25 na wanafunzi wa kike 20 kwa tundu moja la choo, Tanzania kwa sasa tundu moja linatumiwa na wavulana 57 huku wasichana 56 wakitumia tundu moja.

Taswira ya ushuhuda huo wa CAG inaonekana kujidhihirisha katika Shule ya Sekondari Ayalagaya ambayo wadau wa elimu wameamua kujenga vyoo vya kisasa ili kutatua tatizo la utoro kwa watoto wa kike waliokuwa wanalazimika kukacha masomo kwa siku kadhaa wanazokuwa katika 'siku za mwezi'.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako.

Nipashe ilipomdadisi Mkuu wa Shule hiyo ya kata, Simon Atu, alisema ujenzi wa vyoo hivyo vya kisasa ulioanza mwaka 2017 na kukamilika rasmi Machi, mwaka jana, umesaidia kuongeza idadi ya mahudhurio kwa watoto wa kike ambao wengi wao walikuwa wakikosa siku kadhaa katika kila mwezi, hasa wakiwa kwenye kipindi cha hedhi.

"Shule ilianzishwa rasmi mwaka 2006. Kabla ya ujenzi wa vyoo hivi vya kisasa, tulikuwa na matundu sita tu ya vyoo vya shimo; matatu kwa ajili ya wavulana na matatu kwa ajili ya wasichana.

"Hivi vyoo vya kisasa vina matundu 16 kwa ajili ya wasichana, manane kwa ajili ya haja kubwa kwa wavulana na mengine saba mahususi kwa wavulana kujisaidia haja ndogo," alisema.

Katika kile kinachooneka vyoo bora vina mchango katika mahudhurio ya wanafunzi wa kike shuleni, Mwalimu Atu alisema kabla ya ujenzi wa vyoo vya kisasa shuleni kwake, mahudhurio ya wasichana yalikuwa asilimia 60 hadi 70, sababu kubwa ya utoro akiitaja kuwa ni wengi wao kushindwa kuhudhuria shuleni kutokana na kutokuwa na sehemu ya kubadili taulo za kujisitiri.

Alisema kwa sasa mahudhurio ya wanafunzi wa kike ni ya asilimia 92, takwimu ambazo ni sawa na wanafunzi wa kike 280 kati ya 307 walioko katika shule hiyo.

"Niseme tu kweli, wanafunzi wa kike walikuwa wakisumbuka sana na hali hiyo tofauti na ilivyo sasa, vyoo hivi vina huduma zote muhimu, wanafunzi wa kike wanaweza kufua vitambaa vyao ndani ya vyoo hivi, wakabadili taulo na kurejea darasani kuendelea na masomo," alisema.

Mwalimu Atu alisema utoro wa wanafunzi, hasa wa kike shuleni hapo, uliwashtua wadau wa elimu ambao kwa kushirikiana na serikali, waliamua kufanya ukarabati wa vyumba vya madarasa na kujenga vyoo vya kisasa.

Alisema ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule hiyo umefanywa na Karimu International Foundation kwa kushirikiana na serikali na wananchi kata hiyo.

"Vyoo vilivyokuwapo hapa awali vilikuwa vichache na havikuwa na sehemu maalum ya watoto wa kike kubadili vitambaa wanapokuwa katika siku zao za hedhi, matundu hayakuwiana na idadi ya wanafunzi waliopo shuleni. Tunawashukuru sana wadau hawa kwa msaada wao huu muhimu," alisifu.

Mwalimu Atu pia aliipongeza serikali kwa kutoa ushirikiano mkubwa kwa wafadhili hao katika kuboresha miundombinu ya sekta ya elimu, akieleza kuwa wasichana wengi shuleni hapo walikuwa wanafanya vibaya kimasomo kutokana na utoro.

Meneja Miradi wa Karimu International Foundation Mkoa wa Manyara, Shau Erro, alisema mkakati wao mwingine ni kuhakikisha shule hiyo inakuwa na majengo bora ya madarasa ya kidato cha tano na cha sita pamoja na hosteli za wanafunzi watakojiunga na shule hiyo.

Alisema taasisi yao imeona kuna haja kuisaidia serikali kuboresha sekta ya elimu ili kutengeneza kizazi bora kwa taifa la kesho lenye vijana waliosoma katika mazingira bora ya shule.

Diwani wa Kata ya Ayalagaya, Sabini John, alipongeza jitihada za wadau hao wa elimu na wananchi wa kata hiyo kwa kushiriki katika uboreshaji wa shule hiyo.

### OFISA ELIMU ANASEMAJE?

Udadisi wa Nipashe ulihamia kwa Ofisa Elimu wa Wilaya ya Babati, Rose Mpare, aliyekiri kujengwa kwa vyoo hivyo vya kisasa kumesaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la utoro kwa wanafunzi wa kike katika shule.

"Unajua, msichana akiwa katika hali hiyo (hedhi), anahitaji usafi wa hali ya juu ili kuepuka kupata madhara ya kukaa na pedi au kitambaa cha kujisitiri kwa muda mrefu.

"Tunawashukuru wadau Karimu International Foundation kwa kushirikiana na serikali kujenga vyoo hivyo, tunaamini ni msingi mzuri kwa wasichana kwa sababu vinawasaidia kutokosa masomo yao ya kila siku hata pale wanapokuwa katika siku zao.

"Suala la mtoto wa kike kukosa masomo kisa ameingia kwenye hedhi halikubaliki kabisa, vyoo vya kisasa ni kinga kwao kuepuka kukosa masomo ya darasani wanapokuwa katika hali hiyo," alisema.

Alisema shauku yake ni kuona kila shule wilayani kwake inakuwa na vyoo vya aina hiyo kwa kuwa vinasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza mahudhurio ya watoto wa kike shuleni.

### HATUA ZA HALMASHAURI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Babati, Hamisi Malinga, alisifu utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya shule hiyo, akieleza kuwa Karimu International Foundation walipata ushirikiano mzuri kutoka serikalini na wananchi katika ujenzi huo.

"Ujenzi wa vyoo bora vya kisasa katika shule hii ni jambo muhimu sana, kwa sababu shule hizi za pembezoni watoto wengi wamekuwa wakikosa masomo kutokana na kukosa sehemu ya kujisitiri kipindi cha hedhi," alisema na kutaja faida za utekelezaji wa mradi huo akifafanua:

"Kwa kweli mahudhurio ya sasa kwa watoto wa kike ni mazuri sana, tuna kila sababu ya kuwashukuru Karimu International Foundational, kwa sababu wamesaidia kupunguza utoro shuleni, hususani kwa watoto wa kike."

Alisema serikali iko mstari wa mbele kushirikiana na wadau wanaounga mkono jitihada zake za maendeleo katika sekta mbalimbali, akitoa wito kwa wadau wengine kujitokeza kutoa mchango wao kuboresha miundombinu ya shule zilizoko katika halmashauri hiyo. Alisema lengo lao ni kuona halmashauri inakuwa na vyoo vya kisasa katika shule zote ili kumwezesha mtoto wa kike kupata haki yake ya elimu bila vikwazo vya kimiundombinu.

### SAUTI ZA WANAFUNZI

Nuria Mwanja, mwanafunzi wa kidato cha kwanza wa sekondari ya Ayalagaya, aliiambia Nipashe kuwa ujenzi wa vyoo hivyo vya kisasa umefanyika wakati mwafaka kwao kwa kuwa awali walikuwa wanalazimika kukosa vipindi vya masomo kwa siku tatu hadi nne kila mwezi kutokana na kuhofu kuaibika mbele ya wanafunzi wenzao kwa sababu za kibaiolojia.

Alisema vyoo vya awali vilikuwa vichache na havikuwa na sehemu maalum ya kujisitiri, lakini sasa maeneo hayo yapo na hawana sababu tena ya kuhofu kuchekwa na wenzao.

"Kwa sasa msichana kukosa vipindi darasani kwa sababu ya hedhi haipo tena, labda iwe kwa sababu nyingine, tunafurahia mazingira yaliyopo ni mazuri na rafiki kwetu," alisifu.

Alisema kuna haja serikali kushirikiana na wadau kuboresha miundombinu ya shule, hasa vyoo kwa kuzingatia mahitaji ya wasichana na watu wenye ulemavu.

Maria Gorbe, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika shule hiyo, alisifu uboreshaji wa miundombinu ya shule yao, akieleza kuwa kwa sasa inavutia kutokana na mandhari nzuri iliyopo.

Alisema awali vyoo vilikuwa vichache na havikuwa na sehemu ya kuweka taka kama pedi zilizotumika, lakini maboresho yaliyofanyika yamezingatia suala hilo, huku pia kukijengwa sehemu ya kufua na kunawia mikono mwanafunzi anapotoka kubadili nguo au vitambaa anavyovitumia wakati wa hedhi.

## HABARI KITAIFA

# Kigwangalla: Nimemalizana na Katibu Mkuu

**Na Salome Kitomari**

SIKU moja baada ya Rais John Magufuli, kutoa siku tano kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla na Katibu Mkuu wake, Prof. Adolf Mkenda kupatana, waziri amedai wamemaliza tofauti zao.

Hata hivyo, Prof. Mkenda, hakutaka kuzungumza kama mapatano yameshafanyika kati yao au la.

Katika ukurasa wake wa Twiter, Waziri Kigwangalla alisema baada ya kikao na Katibu Mkuu Kiongozi, wamemaliza tofauti zao na sasa hali ni shwari.

"Kazi ya urais ni ngumu sana, tulioteuliwa na Rais kumsaidia utendaji/usimamizi wa maeneo mbalimbali hatupaswi kumwongezea Rais 'frustrations' (usumbufu) nyingine zaidi," alisema kwenye ukurasa huo na kuongeza:

"Sisi kwenye wizara yetu, baada ya kikao na Chief Secretary (Katibu Mkuu Kiongozi), tulimaliza tofauti zilizokuwapo na sasa hali ni shwari."

Nipashe ilimtafuta Prof. Mkenda, ambaye baada ya kuelezwa alichokisema waziri na kama wamemaliza tofauti zao, alijibu: "Nisingependa kabisa kuongelea jambo hili, mkuu wa nchi ameshaongea vizuri, mimi sipo Twitter ila ningependa nisiongee."

Juzi kupitia taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Ikulu, Rais John Magufuli akizungumza na maofisa na askari wa wanyamapori wa Hifadhi ya Misitu ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo ambako ametembelea na kujionea vivutio vya utalii, alitoa siku tano kwa viongozi hao kumaliza tofauti zao.

Katika salamu zake, alilipongeza Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) kwa kazi nzuri ya uhifadhi, kukuza utalii na kuchangia mapato ya serikali, lakini alielezea kusikitishwa kwake na mahusiano mabaya yaliyopo kati ya Waziri Dk. Kigwangalla na Katibu Mkuu wake Prof. Mkenda hali ambayo inasababisha baadhi ya shughuli za wizara kusuasua.

Alisema anafahamu kuwa viongozi hao hawaelewani na anawatazama taratibu na kwamba alishampa kazi Katibu Mkuu kiongozi awaite na wasipobadilika atawaondoa.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe (mwenye suti ya bluu), akifurahi baada ya kukata utepe kuzindua mnara wa mawasiliano katika kijiji cha Kanoge kilichopo wilayani Mlele, mkoani Katavi. Wa pili kushoto ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Rachel Kasanda na wa tatu kulia ni Justina Mashiba, Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri apiga 'stop' mawakili binafsi kutoza fedha hati kiapo

**Na Ashton Balaigwa**

SERIKALI imewapiga marufuku baadhi ya wanasheria Mkoa wa Morogoro kuwatoza fedha wananchi kiasi cha Sh. 6,500 kwa ajili ya kugharamia hati ya kiapo, ili kukidhi vigezo vya kupata namba ya kitambulisho na badala yake imeahidi kutoa wanasheria wa serikali kutoka ofisi ya mkoa ili kusaidia kutoa huduma hiyo.

Katazo hilo lilitolewa na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alipofanya ziara ya kushtukiza katika Ofisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) mkoa wa Morogoro kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi waliojitokeza kwa ajili ya kufanya usajili wa kupata vitambulisho vya Taifa, ambapo baadhi ya wananchi waliwasilisha kero hiyo.

Ziara ya Masauni Morogoro imekuja siku chache baada ya Rais John Magufuli kuongeza siku 20 kwa wananchi kusajili laini za siku zao kwa njia ya vidole gumba.

Baadhi ya wananchi walipata nafasi ya kuelezea changamoto zinawapata wakati wa kufuatilia namba za kitambulisho cha Taifa, walisema wanapata usumbufu kutoka kwa baadhi ya maofisa wa Nida Morogoro wanapowarudisha baada ya kuona hati za kiapo kukosekana na kuwaelekeza waonane na wanasheria waliopo nje ya geti la ofisi hizo, ambako wanatozwa shilingi 6,500.

"Sisi wengine tumekwama katika zoezi la kupata kitambulisho kutokana na kurudishiwa fomu zetu na maofisa wa Nida wakitutaka tupeleke hati ya kiapo na kutuelekeza kuonana na mawakili nje ya geti na ukifika huko unaambiwa gharama ni shilingi 6,500,"

INAENDELEA UK. 8

# Usafiri wa treni sasa warejea

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

USAFIRI wa treni kutoka jijini Dodoma kuelekea mkoani Kigoma uliokuwa umesitishwa kwa muda kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, ulirejea jana asubuhi, huku tatizo likibakia kwa treni kwa wasafiri wanaoanzia Dodoma kuelekea Dar es Salaam kutokana na eneo la Godegode bado halijaimarika.

Kwa upande wa wasafiri wanaoanzia Dodoma kwenda Kigoma unaendelea kutoa huduma kutokana na eneo la Kigwe na Zuzu ambapo reli ilikuwa imejaa maji.

Alizungumza na Nipashe jana Stesheni Master wa Dodoma, Rose Ngauga, alisema awali walisitisha usafiri huo kutokana na stesheni ya Kigwe Zuzu nje kidogo ya Dodoma kuelekea Kigoma na kutoka Dodoma kuelekea Dar es Salaam ilishindikana kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha na kusababisha mchanga kujaa katika baadhi ya maeneo hayo.

Alisema eneo la Kigwe kilomita 482 .7 hadi 482.9, maji yalijaa na kuchimbua tuta la reli kitendo ambacho kilisababisha kusimamishwa kwa huduma ya treni hiyo ya mwendokasi Delux

Alisema hali hiyo ni hatari kuruhusu treni kufanya kazi Lea kwa sababu unaweza kuhatarisha maisha ya watu.

Alisema wapo abiria waliokwama Dodoma, Morogoro pamoja na Dar es Salaam walitafutiwa usafiri wa magari kwa ajili ya kuwafikisha walikokuwa wanakwenda.

Ngauga alisema abiria walioukuwa wakitokea Dar es Salaam na Mkoa wa Morogoro kwenda Kigoma walisafishwa kwa mabasi mbalimbali ikiwamo ya Abood hadi Dodoma, ili kupanda usafiri wa treni kutokea Dodoma ambapo kipande kilichokuwa kinaleta shida wataalamu wamekirekebisha.

Alifafanua kuwa abiria zaidi ya 1,000 waliokuwa wamekwama Morogoro na Dar es Salaam walisafirishwa hadi Dodoma na juzi asubuhi kwa treni ya Delax pamoja na treni ya B15 iliyoondoka jana kuelekea Kigoma.

Alisema wanashukuru wataalamu wanaendelea na matengenezo kuhakikisha reli inakuwa sawa na kuendelea na safari zake kama kawaida.


**BANI INVESTMENT LIMITED**
**DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS**

**NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KWA WADAIWA WA NBC BANK MAKAO MAKUU DAR ES SALAAM**

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA NBC MAKAO MAKUU** tunatoa notisi ya siku 14 na tangazo la mnada wa hadhara wa mali zilizoorodheshwa hapo chini ambazo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo. Hivyo basi utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili,Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada.Mnada utafanyika mahali zilipo mali hizi, siku na saa kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

| JINA LA AKAUNTI | MMILIKI | MALI ZILIZOWEKWA DHAMANA | MAHALI | TAREHE | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| Amoni A.Mchomvu | Amoni Augustino Mchomvu | Nyumba ya kuishi yenye CT No.82240, L.O. No.349806, Plot No.2053 Block 'B' | Kimara Bonyokwa area, Dar es salaam | 16.1.2020 | 4:00 asubuhi |
| Malobeni Traders | Simon Abel Mbatiani | nyumba yenye CT No.55664, L.O. no.205318, Plot no.82/1 Block 'A' | Ubungo Kibangu | 16.1.2020 | 8:00 mchana |
| Alphord B Pius | Alford Mbunga Pius | nyumba ya kuishi yenye CT.no.17352-LR Mwanza, LO no.182649, plot no. 107, block 'DD' | Ngokolo - Shinyanga | 18.1.2020 | 4:00 asubuhi |
| Majid Hussen Mwesi | Majid Hussein Mwesi | Nyumba ya kuishi yenye CT No.19994-LR Mwanza, Plot No.66, Block 'EE' | Ngokolo, Shinyanga | 18.1.2020 | 8:00 mchana |
| Salum Mohamed Mahinya | Juma Ally Mbarika | Nyumba ya kuishi C.T No. 34889, L.O. No. 84653, Plot No. 349, Block 'Y' Mfaranyaki | Mfaranyaki-Songea | 25.1.2020 | 4:00 asubuhi |
| Jackson Nyanje | Omary Mariam Nyanje | Nyumba ya kuishi yenye CT No.13355-MBYLR, L.O. No.295648 Plot No.1 | Tunduma urban area | 31.1.2020 | 4:00asubuhi |
| Simbo Yonah Kimaro | Simbo Yonna Kimaro | Nyumba ya kuishi yenye C.T No.14310-MBYLR, L.O No. 240065, Plot no.7 | Nsalala Mbalizi urban area, Mbeya district | 29.1.2020 | 4:00 asubuhi |
| Festo Eston Ilomo | Festo Eston | CT no.11821-MBYLR, LO no.173343, plot no.1113, Block 'OO' | Hali ya hewa, sumbawanga | 04.2.2020 | 4:00 asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali zitauzwa "kama zilivyo " as is where is basis"
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:

**Kwa maelezo zaidi wasiliana Na ofisi ya BANI INVESTMENT LTD Nkurmah Street, Lida Building, Ghorofa ya 3, Chumba No. 0313 S.L.P 71340 Dar es Salaam au kwa simu na. 0713 224578, 0713, 295747, 0653 640999**

215570502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Afadhali Masauni ameliona hili Nida

**KASI** ndogo ya utolewaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi, imekuwa ikielezwa kuwa inasababishwa na mambo kadhaa.

Wananchi kadhaa wamekuwa wakiitupia lawama Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) kuwa maofisa wake ni warasimu, hivyo kusababisha kasi ndogo ya kutolewa kwa vitambulisho hivyo.

Hata hivyo, wakati mwingine malalamiko ya baadhi ya watu yanaonekana kutokuwa na mashiko kwa kuwa mchakato wa kutolewa kwa vitambulisho hivyo ulianza miaka kadhaa iliyopita.

Kimsingi, wananchi wengi hawakujitokeza au kwa lugha nyingine hawakuchangamkia fursa hiyo hadi baada ya serikali kutangaza utaratibu wa kusajili laini za simu kwa njia ya vidole gumba.

Wengi walipuuzia kwenda kujiandikisha kwa ajili ya kupata vitambulisho kutokana na kutokuona umuhimu, kicha ya hamasa iliyokuwa ikitolewa, hadi baada ya kuona muda wa kuzima laini unakaribia ambao ulikuwa Desemba 31, mwaka jana, kabla ya Rais John Magufuli kuongeza siku 20 kuanzia jana hadi Januari 20.

Inawezekana Nida ikawa na udhaifu kwa baadhi ya watumishi wake, lakini si jambo la busara kuitupia lawama hizo, kwa kuwa hata baadhi ya wananchi wanakaidi kufuata maelekezo yanayotolewa na taasisi hiyo kuhusiana na taratibu za kufuata kupata vitambulisho.

Jana serikali ilibaini moja ya usumbufu wanaoupata wananchi wanapokwenda kutafuta vitambulisho hivyo, ambao ni mawakili binafsi wanatoza Sh. 6,500 kwa ajili ya kupata viapo.

Moja ya masharti ya kupata vitambulisho hivyo ni mwombaji kuwa na kitambulisho cha kuzaliwa, hivyo kama hana, anatakiwa kuapa kwa wakili au mahakamani.

Kutokana na kuona fursa hiyo, mawakili binafsi wamekuwa wakienda karibu na ofisi za Nida kwa ajili ya kuwahudumia waombaji wa vitambulisho kwa kuwapa viapo kwa malipo.

Hata hivyo, kutokana na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masaini akiwa mjini Morogoro katika ofisi za Nida na kupokea malalamiko ya wananchi kuhusu kutozwa kiasi hicho cha fedha, akiwapiga marufuku baadhi ya wanasheria binafsi Mkoa wa Morogoro kuwatoza fedha wananchi kiasi hicho 6,500 kwa ajili ya kugharamia hati ya kiapo, ili kukidhi vigezo vya kupata namba ya kitambulisho na badala yake ameahidi kutoa wanasheria wa serikali kutoka ofisi ya mkoa ili kusaidia kutoa huduma hiyo.

Ni kweli malipo hayo ni makubwa kwa wananchi wengi ambao kipato chao ni kidogo, hivyo kukwama kukidhi matakwa ya kupata vitambulisho vya Taifa.


Sisi tunaona kuwa kama serikali ingeweka utaratibu tangu awali wa kuwapeleka mawakili wa serikali kuwahudumia wananchi kuwapa viapo, watu wengi wangekuwa wamevipata, ingawa tunaelewa pia kwamba mawakili wa serikali hawatoshi kutoa huduma hiyo kwa Watanzania wote.

Tunaamini kuwa kama utawekwa utaratibu mzuri jambo hili linawezekana katika mikoa mingine, baada ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, kukubali kutekeleza agizo la Masauni la kupeleka wanasheria wa serikali kusaidia.

Tunawasisitiza wananchi kufuata maelekezo ya Nida wakati wote wa mchakato wa kutafuta vitambulisho vya taifa hata baada ya kumalizika muda wa kusajili laini za simu.

Tunasema hivyo kwa kuwa vitambulisho vya taifa ni suala nyeti kwa kuwa bila mamlaka husika kuwa makini, vinginevyo inaweza kuwapa vitambulisho watu wasio raia wa nchi hii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Mvua hizi, kanuni zake kujihami nazo hizi hapa

**NI** msimu wa mvua ambao mikoa mbalimbali nchini, zinanyesha na kusababisha aina mbalimbali ya mafuriko, japo sura ya pili ina neema zake. Sote tunajua 'maji ni uhai.'

Ushahidi wa jumla ni kwamba, katika maeneo mbalimbali mtu anakopita anakutana na adha za mvua mito kupanuka, majengo kuathiriwa na athari hizo.

Kunaponyesha mvua, baadhi ya watu katika jamii wanashindwa kutumia ustaarabu kukabili mvua hizo na mvua hizo hutumika kutiririsha maji machafu.

Shida mojawapo inayojitokeza ni baadhi ya watu hugeuza mvua na maji yake mbadala wa kushughulikia athari zao, wakitiririsha maji machafu ya vyooni kupitia maji yaliyojaa.

Hapo ndipo shida inaanza, kwani maji machafu yanatiririka katika makazi ya umma jirani. Kuna sehemu yanaingia kwenye bustani za mboga zinazodhaniwa kuwa mlo wa umma.

Simulizi inayofuata baada ya hapo, ni kushuhudia magonjwa ya milipuko, kwani maji machafu yana mengi. Mtu anapoyakanyaga tu, anaweza kupata magonjwa ya kuambukiza kama vile fangasi na ndio mwanzo wa matatizo kama maradhi ya ngozi.

Hivyo basi, jamii inatakiwa kuwa makini kupitia mvua hizo kijihami kuzingatia suala la afya ya umma.

Hivi karibuni imeelezwa kuwa Watanzania hususani wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wamehimizwa kuzingatia kanuni za afya na usafi wa mazingira, hasa katika kipindi kilichopo cha msimu wa mvua za masika, waepuke magonjwa mbalimbali.

Mkurugenzi wa Idara ya Kinga, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, anasema Watanzania wanatakiwa kujua hiki kilichopo ni msimu wa mvua kubwa, katika maeneo mbalimbali kitaifa.

Ingawaje ni neema, lakini wakati mwingine inakuwa adha, inapoangaliwa katika mtazamo wa kiafya, mwenyewe akitamka: "Tunakuwa na maji mengi, tunakuwa na mafuriko, kwa hiyo tuendelee kuzingatia kanuni za afya katika maeneo yetu."

Anatoa mfano wa Jiji la Dar es Salaam, kwamba lilikumbwa na mlipuko wa homa ya dengue na serikali ikachukua hatua ya kuidhibiti kwa nguvu zote, hivyo madhara ya mvua nayo yanapaswa kudhibitiwa, mosi kwa kuizingatia kanuni zilizopo za afya.

Dk. Subi anaongeza kuwa eneo wanaoliona limezungukwa na maji, wanapaswa kuendelea kutumia dawa, kulala kwa kutumia vyandarua, kufukia madimbwi ya maji na kuondoa vifuu vya nazi, tena bila ya kuruhusu uwepo wa mazalia ya mbu.

Anashauri sheria zichukuliwe, kwa wote watakaobainika kutiririsha maji katika kipindi cha mvua zinaponyesha na kwa wananchi kuhakikisha matumizi ya maji yawe ya kunywa, kunawa mikono au kuoshea vyombo ni yaliyochemshwa, lengo ni kuhakikisha wadudu waenezao magonjwa wanakufa.

"Hivyo, pamoja na kwamba upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam umeimarika hadi kufikia asilimia 85, bado kuna ile asilimia 15," anasema.

Anashauri jamii kuendelea kuhakikisha wanatumia maji safi na salama, muhimu wachemshe maji ya kunywa, wakiona hawawezi basi watumie dawa aina ya 'chlorine' na 'water guard' ambazo ni nzuri katika maeneo yao, huku wakinawa mikono hasa kabla ya kula chakula.

"Hizi ni baadhi ya kanuni za afya ambazo tunahimiza wananchi waendelee kuzingatia, tuna uwezo kabisa wa kupambana na maradhi. Tumetolewa pia wito kama unakaa kwenye mabonde hama, serikali imetoa wito kwa wananchi wote.

"Wale ambao wanakaa kwenye maeneo hatarishi kuhama, kwa sababu ni hatarishi kwa afya lakini pia ni hatarishi kwa maisha yao na familia zao," anasema kiongozi huyo wa afya .

Mwisho, anatoa rai kwa jamii kuwalinda watoto, walemavu na wagonjwa ambao wanataabika, katika suala la usafi wa ndani ya nyumba, kwa kupuliza dawa za mbu ili kujikinga.

## BARUA & MJADALA

## Tushikamane vita kichaa cha mbwa

**Mhariri,**

*HIVI karibuni nilikuwa nafuatilia kwa karibu matangazo ya afya redioni na mahususi kuhusu ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Kuna jambo lilinishtua sana.*

*Kimsingi, haya si maradhi mapya katika jamii zetu, bali imezoeleka na inafahamika sana katika jamii yetu.*

*Katika maelezo hayo, licha ya uzoefu na uelewa wangu, nilipata darasa lingine lililonifungua uelewa na elimu ya ziada, kwamba athari zake zikikaa kati ya wiki moja na mbili, kuna uwezekano tiba yake ikakwama isipowahiwa, hata kufikia hatua ya mauti.*

*Pia ikaelezwa kwamba katika mazingira ya jamii zetu mijini na vijijini, kuna mbwa wengi wanaosumbuliwa na shida hiyo na kwa bahati mbaya wako wengi wanaozurura mitaani.*

*Hapa binafsi inanipa ujumbe mzito unaoendana na mshtuko unaonigusa, pia nikiangaza jamii kwa jumla, haja ya hatua zaidi inapaswa kuchukuliwa kukabili uwezekano wa janga hilo.*

*Serikali, kupitia halmashauri zake mbalimbali nchini, ina nafasi kubwa ya kuendeleza kile inachokifanya kukabili madhara ya kichaa cha mbwa kupitia tiba kwa wanyama hao, vivyo hivyo hata kampeni za kuua mbwa wanaozurura ovyo.*


*Kwanza nikianza na suala la mbwa kuzurura ovyo ni zao la uzembe wetu jamii tunachangia hilo kwa kiasi kikubwa na wajibu wa kwanza ni kudhibiti hilo kwa namna yoyote na hatuchangii katika uwepo wa mbwa wazururao ovyo.*

*Pili tunaoishi mitaani tunapaswa kuwa mstari wa mbele kuipa serikali ushirikiano katika kampeni za udhibiti, tukianzia na viongozi wa mtaa kama wenyeviti wa mitaa na vijiji, madiwani na wadau wengine wa ngazi hiyo.*

*Kama alivyosema Mwalimu Julius Nyerere miaka 55 iliyopita, kwamba 'inawezekana, timiza wajibu wako,' ndicho nasi mtaani tunaweza katika hilo la kukabili kichaa cha mbwa kila mtu akachukua nafasi yake kukikabili.*

**Erenest Arbogasti,**
**Kasulu.**

# Wanafunzi hamieni mtindo afya kwanza, mimba subirini




**Na Sabato Kasika**

**KIKWAZO** kikubwa kwa watoto wa kike ambacho kinachangia kuwafanya waharibu afya zao na wakati mwingine washindwe kuendelea na masomo, ni mimba za utotoni wanazokumbana nazo.

Taarifa kutoka mikoa mbalimbali zimekuwa zikionyesha idadi ya wanafunzi wanaokatisha masomo kwa kupachikwa mimba au kuolewa, hali ambayo inawanyima nafasi ya kutimiza ndoto zake katika elimu.

Kwa mfano, hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, alisema kuanzia Januari hadi Novemba mwaka uliopita wanafunzi 150 wa msingi na sekondari mkoani humo walikatisha masomo kwa sababu ya mimba.

Huo ni mfano mmojawapo, lakini ninaamini tatizo hili la mimba liko mikoa mingi tu hapa nchini ingawa juhudi mbalimbali zimekuwa zikifanyika za kukomesha mimba hizo ili kumwokoa mtoto wa kike.

Serikali na wadau wa afya kwa ujumla wao wanaendelea na juhudi zinazolenga kuhakikisha mimba hizo zinakoma, lakini pamoja na hayo, ni vyema juhudi zaidi zikaelekezwa kwenye elimu ya afya ya uzazi.

Elimu ya afya ya uzazi ni muhimu na ile ya elimu rika, kwani vijana wakiipata na kuizingatia inaweza kusaidia kupunguza mimba na ndoa za utotoni ambazo ni kama jambo la kawaida kwenye baadhi ya mikoa hapa nchini.

Ingawa elimu hii inaweza kuwa ni tatizo kwa baadhi ya watu wanaoamini kwamba ni sawa na kumfundisha kijana wa kike au wa kiume kuanza mambo ya uhusiano mapema, lakini inasaidia kuwajengea ufahamu.

Wakiwa na ufahamu wa kutosha itakuwa ni rahisi kumaliza tatizo la mimba za utotoni, ambazo zinakwamisha watoto wa kike kuendelea na masomo na hata wakati mwingine kuharibu afya zao.

Kuna umuhimu kwa mtoto wa kike kujitambua na kuepuka vishawishi ambavyo vinaweza kumwingiza kwenye mahusiano ambayo mwisho wake ni kupata mimba katika umri mdogo.

Njia nzuri ya kuepuka mimba hizo kama nilivyosema, ni kupewa elimu ya afya ya uzazi na elimu rika, na kuizingatia kwani hivyo vyote ni vya msingi kwa maendeleo ya elimu na afya ya mhusika.

Kimsingi, mimba za utotoni huathiri afya, elimu na haki za mtoto wa kike, kwani mtoto wa kike asiye na elimu atakuwa na ugumu kupata ajira na kujijengea maisha bora na familia yake.

Vilevile, msichana anayeshika mimba akiwa na umri wa miaka 14 au chini yake, haki zake zitakuwa zimekiukwa, hivyo ni muhimu kumlinda ili asikumbane na matatizo hayo.

Wataalamu wa afya wansema, mimba za utotoni zina madhara ya kiafya kwani anapopata ujauzito na umri mdogo, kuna uwezekano wa kupoteza maisha na viungo vyake vya mwili wakati wa kujifungua vinakuwa bado havijakomaa kuwa na uwezo wa kushika mimba.

Miili yao bado haiwezi kuhimili mikikimikiki ya ujauzito hadi kujifungua na kuna wakati analazimika kufanyiwa upasuaji.

Inaelezwa kitaalamu, akilazimisha kujifungua kwa njia ya kawaida, anajihatarisha hata kupoteza maisha. Mbali na madhara hayo, wanataja mengine kupatwa na magonjwa hatari yanayoambatana na ngono, kama vile ukimwi na maradhi hatari ya zinaa; kisonono na kaswende.

Mtindo wa kutoa mimba, nao unatajwa kusababisha madhara ya kiafya, hasa kwa wale ambao hukumbwa na tatizo na kukimbilia kutoa, wanaweza kupoteza maisha, wakiwa katika harakati hizo.

Madhara ya kiakili nayo yanatajwa kumharibu mtoto wa kike, kwa vile binti mdogo kupata ujauzito anakuwa na mawazo mengi juu ya ujauzito huo kwamba ataamua kulea au kuutoa.

Kwa hiyo, mbadala ya msingi klwa binti ni kuzidisha elimu ya afya ya uzazi na elimu rika, ili kuwanusuru na madhara hayo na pia ifike wakati waseme afya kwanza, mimba baadaye na kusimamia uamuzi huo.

Inauma sasa binti kupoteza maisha au kukosa elimu kwa sababu ya mimba za utotoni, ambazo jamii ikiamua kushirikiana na serikali kikamilifu, katika vita hii, inaweza kusaidia kuitokomeza.

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Waziri apiga 'stop' mawakili binafsi kutoza fedha hati kiapo

INATOKA UK. 5

alisema Mwajuma Ally, mkazi wa Kata ya Kichangani na kuendelea:

"Waliokuwa nazo wanalipa na sisi wengine tusiokuwa na hela imebidi turudi tukatafute... na leo tumepata ndio tumekuja."

Baada ya kusikia kero hiyo, Masauni alionekana kutopendezwa na utaratibu huo na kueleza kwa kuwa unawapa kero wananchi wenye kipato cha chini, hivyo kuuagiza uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Morogoro kutumia wanasheria wake ili kuwasaidia wananchi.

Aidha, alimwagiza Mkurugenzi wa Nida makao makuu kufuatilia kwa karibu kitengo cha uchunguzi ambao wanadaiwa kuchelewesha kutoa mrejesho wa fomu za wananchi zilizoonekana zina changamoto, hivyo inayodaiwa kuwaongezea usumbufu wananchi pamoja na kuongeza msongamano mkubwa katika ufuatiliaji wa namba za vitambulisho vya taifa.

Naibu Waziri alitoa siku tatu kwa Nida makao makuu kuhakikisha anapata majibu ya kuridhisha katika mamlaka hiyo wakati mkakati wa kukamilisha zoezi la usajili katika kipindi cha siku ishirini kilichoongezwa na Rais John Magufuli kuanzia jana hadi Januari 20.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, alimweleza Naibu Waziri kuwa wananchi Mkoa wa Morogoro wamejisajili kwa asilimia 76, ambapo asilimia 24 pekee ndio wanaendelea kujisajili.

Pia aliahidi kupeleka wanasheria wa serikali katika ofisi ya Nida ili kutatua kero za wananchi wanaotozwa fedha za wanasheria binafsi kwa ajili ya viapo.



Askofu wa Kanisa la Romani Katoliki Jimbo la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, akibariki waumini wa kanisa hilo, wakati akiingia kuendesha misa ya mkesha wa kuukaribisha mwaka mpya 2020, kwenye kanisa hilo Parokia ya Ngokolo Shinyanga Mjini. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Makusanyo ya Desemba yavunja rekodi ya TRA

INATOKA UK. 3

ya kukusanya Sh. trilioni 1.579 na Sh. trilioni 1.538 kwa kipindi kama hicho.

Kamishna alisema makusanyo hayo yanaonyesha ukuaji wa asilimia 14.40 na asilimia 23.31 kulinganisha na makusanyo ya mwezi Oktoba na Novemba, 2018.

"Makusanyo haya ni mwendelezo wa kiashiria cha wazi kwamba walipakodi na Watanzania walio wengi wameendelea kuelewa, kukubali na kuitikia wito wa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria," alisema na kuongeza: "Asiwepo mlipakodi ambaye atathubutu kubaki nyuma, walipe kodi inayotakiwa...kodi ni tukufu lazima ilipwe kwa ukamilifu wake na ndiyo maana imetajwa kwenye vitabu vitakatifu," alisema.

Kadhalika, Kamishna alisema mikakati ya sasa ni TRA kujiimarisha kiteknolojia kwa kujenga mifumo rafiki ya ukusanyaji kodi na maboresho yanayoendelea ili kufanya kazi kama timu moja na kupata mafanikio zaidi.

Kwa mujibu wa Dk. Mhede, pamoja na mafanikio hayo bado hawajafikia malengo yao kwa kuwa upo uwezekano mkubwa wa kukusanya fedha kodi nyingi na kuwa nchi yenye mafanikio makubwa barani Afrika.

Kamishna huyo aliwakumbusha wamiliki wa majengo nchini kujitokeza kulipa kodi za majengo haraka iwezekanavyo ili kuepusha usumbufu.

"Kwa sasa viwango ni rafiki vinalipika kwa kuwa ni Sh. 10,000 kwa nyumba ya kawaida na Sh. 50,000 kwa kila sakafu nyumba ya ghorofa katika majiji, manispaa na halmashauri za miji, huku Sh. 20,000 kwa jengo la ghorofa katika maeneo ya halmashauri za wilaya," alifafanua.

Aliwaonya wanaojihusisha na kughushi au kusafirisha risiti za kielektroniki (EFD), na kwamba operesheni ya sasa ni kufuatilia matumizi sahihi ya mashine hizo pamoja na kuchukua hatua stahiki kwa wasiofuata taratibu.

# Maaskofu waonya ulaji fedha za Ukimwi, uchaguzi S/Mitaa

INATOKA UK. 2

wa kwa mfano wa sura ya Mungu na tuishi kwa kupendana," aliongeza.

Mkoani Arusha, Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dk. Solomon Massangwa, alisema vyama vya siasa vya upinzani nchini, havikupaswa kususia uchaguzi wa serikali za mitaa, badala yake walitakiwa kuwa hodari, wajasiri, mashujaa na wangepambana hadi hatua ya mwisho bila kukata tamaa.

Katika ibada hiyo ilifanyika katika Kanisa Kuu la KKKT, Dayosisi ya Kaskazini Kati, alisema katika siasa ukikubali mpinzani wako anapokudhoofisha kwa maneno unakuwa umempa nafasi ya kukushinda na utakaporejea ulingoni iitabidi kuanza mwanzo.

Alitolea mfano wa kwenye Biblia kuwa wakati wa kujenga nchi ya ahadi kwa wana wa Israeli, Mungu alimwambia Yoshua awe na moyo wa ushajaa, hodari na mjasiri ili kudhihirisha uaminifu mbele za Mungu.

"Ndugu zangu wakristo na Watanzania ni watu hodari na majasiri sote tukiwa mashujaa na majasiri Tanzania itakuwa na wananchi wasiyoyumbishwa," alisema.

"Waliposema hawataki tena kushiriki katika uchaguzi imeonyesha wazi kwamba wameogopa ulingo na mapambano ya kisiasa wakati awali walishakubali kuingia huko... Kanisa linataka Wakristo kuwa wajasiri, mashujaa na hodari wasikubali kuyumbishwa na jambo lolote," aliongeza.

**Imeandikwa na Marco Maduhu, SHINYANGA na Allan Isack, ARUSHA**

## Jeneza lazua taharuki sokoni

INATOKA UK. 3

kwa ajili ya kufungua biashara yake ya samaki na alipofika sokoni hapo alishangaa kuona jeneza kubwa likiwa juu ya meza mbele ya duka lililo jirani na duka lake, hali iliyomshangaza na kuamua kuwaita walinzi wa soko hilo kuwauliza.

"Nilimuita mmoja wa walinzi wetu wa hapa sokoni ambaye alikuwa anaingia ndani ya soko akasema hajui chochote na wakati tukiendelea kuulizana na kushangaa ndipo umati wa watu nao ukaanza kusogea kushuhudia tukio hili la ajabu," alisema Kilasi.

Naye Kefas Nkonde, mkazi wa Ilemi, jijini Mbeya alisema, tukio hilo linatisha kwa vile sio kitu cha kawaida jeneza kuonekana sokoni na kuiomba serikali ifanye uchunguzi wa kina kuhusiana na tukio hilo.

"Jeneza sio mzinga wa nyuki kwamba tutapenda kuangalia, bali ni kitu kinachoogopesha jamii, hivyo linapoonekana katika maeneo ambayo halitarajiwi kuwapo ni vizuri serikali ikafanya uchunguzi wa kina kujua kiini cha uwapo wake mahali hapa," alisema Nkonde.

Alisema wanachoelewa ni kwamba kwa imani ya Wakristo jeneza linapaswa kuzikwa pamoja na marehemu na kwa utamaduni wa Waislamu jeneza halizikwi, lakini linahifadhiwa msikitini.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Soweto, Ramadhan Tavee, alisema tukio hilo limewashtua wananchi wake kwa vile sio la kawaida, na kwamba kinachoshangaza zaidi limetelekezwa mbele ya duka ambalo mmiliki wake anauguza mgonjwa hospitalini.

Alisema baada ya kuona tukio hilo aliamua kuwasiliana na viongozi wake wa juu katika ngazi ya kata kabla hajapiga simu polisi kwa ajili ya kuomba msaada wa ulinzi katika eneo lake.

"Nilipopata taarifa hii kama kiongozi nilifika mahali hapa mara moja kujiridhisha na niliona jeneza hili, niliwasiliana na viongozi wangu wa kata kisha nikapiga simu polisi na ninashukuru maana askari wamefika kwa wakati na kuhakikisha mtaa wangu unaendelea kuwa na amani na utulivu," alisema Tavee.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Soko la Soweto, Fred Mwaiyongano, alisema baada ya kuliona jeneza hilo aliamua kufuatilia kwa kina ili kujua limefikaje sokoni hapo kwa sababu sio jambo la kawaida na halijawahi kutokea.

Alisema aliwauliza vijana wanaoshusha mizigo kwenye magari sokoni hapo na wakamweleza kuwa jeneza hilo lilishushwa na gari moja la mizigo aina ya Fuso lililokuwa limepeleka nyanya sokoni hapo likitokea katika mji wa Makambako mkoani Njombe.

"Tuliwasiliana na wapakiaji wa mizigo wa Njombe wakasema jeneza hilo lilitumika kusafirisha mwili wa marehemu kutoka Mbeya kwenda Makambako na lilitakiwa kurudishwa Mbeya na ndipo wakalipakia kwenye Fuso hilo ili walipeleke kwenye msikiti mmojawapo uliopo Sokomatola, jijini Mbeya," alisema Mwaiyonga.

Alisema vijana hao walieleza kuwa wakati wa kushusha nyanya sokoni hapo dereva alilisahau katika eneo hilo badala ya kulipeleka eneo alilokuwa ameelekezwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi ili kubaini sababu za jeneza hilo kutelekezwa sokoni hapo.

Alisema mtu mmoja tayari anashikiliwa na Jeshi la Polisi kusaidia uchunguzi wa tukio hilo na akawataka wananchi kuwa watulivu wakati uchunguzi unafanyika.

HABARI KITAIFA



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akishiriki matembezi ya tamasha la kitaifa la mazoezi ya viungo Zanzibar yalioanzia katika Viwanja vya Mnazi Mmoja na kumalizikia katika Uwanja wa Mao Zedong, jijini Zanzibar jana. Wengine ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohammed Aboud Mohammed na Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid. **PICHA: IKULU**

# Tanzania yageukia Vietnam vivutio vya utalii

**Na Beatrice Philemon**

BODI ya Utalii Tanzania (TTB) inatarajia kwenda Vietnam ili kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania, ikiwamo fursa za uwekezaji na biashara zilizopo nchini.

Akizungumza na Nipashe Mwenyekiti wa TTB, Jaji mstaafu Thomas Mihayo, alisema bodi kwa kushirikiana na wadau wengine waliopo katika sekta ya utalii watakwenda Vietnam Aprili.

"Mpaka sasa tumeshaongea na balozi wa Tanzania nchini Vietnam na ametuthibitishia kuwa soko la Vietnam ni zuri, Tanzania inaweza kwenda na kutangaza vivutio vyake kwa Wavietnam ili waje kutembelea Tanzania," anasema.

TTB imeamua kwenda kutangaza vivutio vya utalii katika nchi hiyo baada ya kugundua kuwa Wavietnam wengi hawafahamu vivutio vya utalii vinavyopatikana Tanzania zikiwamo fursa za uwekezaji na biashara zilizopo nchini. Mbali na hilo, pia TTB itatumia ziara hiyo kutangaza hifadhi mpya ya Taifa ya Burigi-Chato ili wananchi wa Vietnam wafahamu vivutio vya utalii vinavyopatikana katika mkoa wa Geita.

Ziara hii itasaidia vivutio vya utalii wa Tanzania kujulikana katika nchi hiyo na kuvutia watalii wengi zaidi kuja kutembelea Tanzania na kuongeza fedha za kigeni zinazotokana na pato la utalii.

"Sisi kama TTB tunafurahi kuona sekta ya utalii inazidi kukua na mpaka sasa sekta ya utalii inachangia pato la Taifa kwa asilimia 17.5 ukiondoa sekta ya kilimo na katika ajira ni sekta ya kwanza," anasema.

Anasema ingawa TTB imeamua kujikita katika soko hili, bado inaendelea kutangaza vivutio vya utalii katika nchi zingine kama vile China, Israel, Korea Kusini ili kuongeza idadi ya watalii wanaokuja kutembelea vivutio vya utalii nchini.

Mbali na hilo hivi sasa mazao ya utalii yameongezeka toka zao moja ambalo tulikuwa tunajikita zaidi hasa zao la utalii wa wanyama na Mlima Kilimanjaro, sasa hivi kuna zao la utalii wa mambo kale, misitu, fukwe, nyuki, utalii wa mikutano na utalii wa meli (cruise ship).

# Makundi maalum yatakiwa kutumia fursa mikopo

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

MBUNGE wa Ilemela, Angelina Mabula, ameyataka makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu yanayonufaika na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na serikali kupitia halmashauri kutumia fursa hiyo vizuri.

Wito huo aliutoa katika ziara ya kutembelea vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela wakati akizungumza na vikundi kutoka kata nne za Bugogwa, Shibula, Kayenze na Sangabuye.

Alisema mwaka mpya unapoanza makundi hayo hususan wanawake watumie fursa za mikopo hiyo kwani ni njia ya serikali kuwawezesha na haiwezi kumfikia mtu mmoja mmoja bali ni kwa vikundi.

Alisema, wakiitumia vizuri watafika mbali, huku akiwataka pale wanapounda kikundi waelewane na kufikia malengo kwani mikopo hiyo wanapewa kwa ajili ya kuanzisha mradi wa pamoja ambao utawasaidia kurejesha fedha hizo ili wengine waweze kupewa. "Kuna baadhi ya wanakikundi wanatumia migongo ya wenzao kujinufaisha kwa kukopa fedha kisha kugawana wachache, ambapo marejesho yanabana kikundi chote hivyo waache tabia hiyo na pale mnapopata mkopo wanakikundi wote wajue kwani ni mkopo wa wazi, na ukitaka mkopo lazima ujue namna gani ya kuutumia ili usishindwe kurejesha," alisema Mabula.

Aliongeza kuwa mikopo hiyo inatolewa kila robo ya mwaka na halmashauri hiyo kabla ya kupitisha bajeti ya kitu kingine wanatenga kwanza asilimia 10 za mapato kwa ajili ya makundi hayo, hivyo aliwataka kutumia sehemu ya mikusanyiko ya watu kama mikutano, semina kuuza na kutangaza bidhaa wanazozalisha.

Kaimu Mkurugenzi, Ofisa Ardhi na Mipango Miji wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Shukrani Kyando, alivitaka vikundi vyote ambavyo vimepatiwa mikopo virejeshe kabla hawajawafuata kwani vinanyima fursa vikundi vingine kunufaika na fedha hizo.

# Sheikh akemea utumikishaji watoto

**Na Shaban Njia,**
KAHAMA

WANANCHI wa Kata ya Chela Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kuacha kuwatumikisha watoto wao wenye umri wa kwenda shule katika shughuli za kilimo na uchungaji wa mifugo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Sheikh wa Wilaya ya Kahama, Ramadhani Damka, wakati wa ufunguzi wa Msikiti wa Chela ambao umejengwa kwa ufadhili wa Jumuiya ya International Istiqaama Muslim Community ya Oman.

Alisema kila mzazi ana wajibu wa kumsomesha mtoto wake kwa ajili ya maandalizi ya baadaye na sio kumtumikisha katika shughuli za kilimo na ufugaji wa mifugo wakati umri wake unahitaji kuwa shuleni.

Aidha, Damka alisema nchi zilizoendelea wananchi wake wamewasomesha watoto wao na kuondokana na kuwa tegemezi kwenye Taifa na kujitambua pamoja na kuwa na hofu ya kutojihusisha katika vitendo vya mauaji ya vikongwe na watu wenye ualbino.

"Wengi wetu tuna watoto wana umri wa kwenda shuleni, lakini hatuwapeleki shule, tunawapeleka kwenye shughuli za kilimo na malisho ya mifugo…hapo unakuwa unatengeneza kizazi cha kuwa tegemezi kwenye jamii na sio wa kuja kukusaidia wewe mzazi," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Chela, Anthony Shagembe, alisema wamekuwa wakiwachukulia hatua za kisheria kwa kuwatoza faini ya mfuko mmoja wa saruji wazazi ambao hawawapeleki watoto wao shuleni.

Pia alisema kuwa mifuko hiyo ambayo huwatoza wazazi faini inatumika katika ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa, ambavyo vimeanzishwa kwa nguvu ya wananchi na kutokamilika kwa wakati.

Shagembe aliwataka viongozi wa Jumuiya ya International Istiqaama Muslimu kusaidia pia katika sekta ya elimu hasa katika ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na afya katika maeneo ya pembezoni mwa mji.

Naye Mwenyekiti wa Msikiti wa Al-wahaab, Mohamed Issa, alisema msikiti uliojengwa unatakiwa kutumika katika matumizi yaliyopangwa hasa kwa kutoa elimu kwa wananchi ili wawe na hofu ya kutojihusisha na vitendo viovu.

# Utalii wa ndani wapewa sapoti

**Na Mwandishi Wetu**

SEKTA ya utalii nchini imetangaziwa fursa zaidi, baada ya mmoja wa wadau kuahidi kuendelea kutoa sapoti.

Mdau huyo Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), imetangaza kuwa itaendelea kusapoti sekta ya utalii nchini kutokana na mchango wake katika kuinua pato la taifa.

Akizungumza katika hafla ya kuwaaga washindi wake wa kampeni ya Ibuka Kidedea na NBC Malengo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere(JNIA) jijini Dar es Salaam, Meneja Chapa na Mawasiliano wa NBC, David Raymond, alisema benki hiyo imekuwa kwa kipindi kirefu ikiweka juhudi mbalimbali katika kuhakikisha sekta ya utalii pamoja na mnyororo wake wa thamani ukifanikiwa.

"Mfano ni kupitia kampeni yetu ya 'Ibuka Kidedea', pamoja na zawadi mbalimbali, lakini leo hii tunapeleka washindi wetu wanne katika mbuga za wanyama za Serengeti ili kuona vivutio vya kipekee ambavyo si rahisi kuviona mahali pengine.

"Hii ni moja ya juhudi za benki katika kusapoti utalii wa ndani, tunajua ni nafasi nzuri kwa wateja wetu na wenza wao kupata nafasi hii ya mapumziko katika mwisho wa mwaka, lakini kwa tukio hili kwa namna nyingine tutakuwa tukisaidia juhudi za serikali yetu katika kutangaza utalii wa ndani na vivutio vya mbuga zetu za wanyama," aliongeza Raymond.

Meneja wa Bidhaa za Uwekezaji wa NBC, Dorothea Mabonye, alisema benki imewekeza kwa kiasi kikubwa katika bidhaa za kidigitali katika kuhakikisha wateja na wasio wateja wanafikiwa na huduma za benki hiyo mahali walipo.

"Ni matumaini yetu washindi wa 'Ibuka Kidedea' watafurahia safari hizi za kitalii na pia wataweza kufurahia huduma za NBC kwa njia za kidigitali popote watakapokuwa," alisema.

Mmoja wa washindi wa Ibuka Kidedea na NBC Malengo, Esther Ndunguru, anayekwenda kufanya utalii wa ndani katika Hifadhi ya Serengeti pamoja na mwenza wake, alisema amefurahishwa sana na safari hiyo.

Walioshinda safari ya Serengeti ni Christopher Mgote kutoka Nzega, Makongoro Makongoro kutoka Arusha, Jocelyine Rwechengura na Esther Ndunguru wote kutoka Dar es Salaam.

Walioshinda safari ya Sychelles ni Wambura John Wambura kutoka Tarime mkoani Mara, Ramadhan Saidi, Lettice Rutashobya na Sylevester Ambokile wote wa jijini Dar es Salaam.

# Sababu wanawake kudumazwa kiuchumi hii

**Na Sabato Kasika**

UCHUMI wa wanawake hususan wa vijijini, unadaiwa kudumazwa na fikra za huduma za kijamii ikiwamo nishati ya umeme, kutokana na uhaba wa huduma hiyo katika maeneo mengi nchini.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam juzi na Mwezeshaji wa Masuala ya Kijinsia, Anna Sangai, katika semina ya kuwajengea uwezo wanawake walioko ngazi za chini, ili watumie nishati mbadala.

Semina hiyo ya siku tatu iliandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na kushirikisha wanawake kutoka mikoa mbalimbali ikiwamo ya Shinyanga, Morogoro na Dar es Salaam.

Alisema, nishati jadidifu ni mbadala wa chanzo cha nishati kilicho na unafuu kwa mtumiaji kama yalivyo matumizi ya umeme yatokanayo na jua, maporomoko ya maji, upepo na kinyesi ambayo ni rahisi.

Sangai alisema, waathirika wakuu, kwenye suala la ukosefu wa nishati bora na nafuu ni wanawake, hivyo hawanabudi kusaidiwa kwa kupewa elimu kama hiyo, ili waondokane na tatizo hilo.

"Matumizi ya kuni yanamfanya mwanamke kuzitafuta mbali na kutumia muda mrefu kupikia chakula, lakini akitumia nishati kulingana na chanzo kilichopo katika eneo lake kama gesi hawezi kupoteza muda," alisema Sangai.

Alisema, utafiti unaonyesha kuwa Mkoa wa Singida na Makambako mkoani Njombe, kuna nishati mbadala itokanayo na upepo, na kwamba fursa ya vyanzo vya nishati mbadala zitapunguza athari za kimazingira na za kiafya.

Kwa upande wake mmoja wa washiriki wa semina hiyo, Fridea Saidi kutoka Kata ya Ukenyenge, Wilaya ya Kishapu Mkoa wa Shinyanga, alisema katika vitu ambavyo vilipaswa kupewa kipaumbele ni namna ya upatikanaji nishati nafuu itakayozalisha umeme unarahisisha shughuli za kila siku.

"Asilimia nne ya fedha halmashauri za mikopo kwa wanawake zitumike kwa ajili ya kujenga vyanzo vya umeme kwa kutumia sola za kusukumia maji na kuwafikia kila mmoja nyumbani," alisema Saidi.



Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ambaye ni Mbunge wa Kisarawe, Selemani Jafo, akimtua ndoo ya maji Neema Petro, kuonyesha kukamilika kwa mradi wa maji wa Kisarawe na wananchi wa mji huo kuanza kupata huduma ya majisafi. Mradi huo umejengwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa thamani ya Sh. bilioni 10.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vuguvugu laja na makubwa ya mazingira, usawa jinsia

**Na Moshi Lusonzo**

VUGUVUGU la watu wanaopenda mabadiliko ya kijamii linalofahamika kama 'We Make Change' limezinduliwa nchini na likiahidi kujikita katika suala la utunzaji wa mazingira na usawa wa kijinsia.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi, Mratibu wa vuguvugu hilo, Rehema Mmanga, alisema kazi yao ya kwanza itakuwa kushirikia kupanda miti katika Jiji la Dodoma na kulifanya kuwa la kijani.

Alisema kazi zote zitakazofanywa na wanachama wa kundi hilo zitakuwa za kujitolea na zenye kulenga kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

"Vuguvugu hili la 'We Make Change' litafanya kazi ya kuleta mabadiliko kwa njia ya kujitolea, tutafanya kazi kwa uzalendo wa nchi yetu na kila mmoja ataonesha jinsi gani anaguswa na hilo," alisema Rehema.

Alisema kujitolea ni njia bora zaidi ya kuleta mabadiliko katika nyanja zote kwa sababu inafanywa na mtu mmoja mmoja kabla ya kuhusisha watu wengine.

"Ndani ya vuguvugu tuna malengo 17, lakini sisi tumechagua mawili ya kuanza nayo, kwanza tunashiriki kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na pili tutapigana katika kutetea haki ya kijinsia," aliongeza kusema.

Rehema alisema mwezi huu watashirikiana na Wakala wa Misitu nchini (TFS) katika zoezi la upandaji miti katika Jiji la Dodoma ili kuligeuza kuwa la kijani.

Kiongozi mwingine wa kundi hilo, Said Omar, alisema vuguvugu hilo limeanzia nchini Uingereza na kuenea katika nchi mbalimbali duniani, na lengo lake ni kuibua moyo wa kujitolea na kuifanya jamii kuishi kama kitu kimoja.

Alisema hapa nchini wameweza kuwaunganisha idadi kubwa ya watu katika mikoa ya Mwanza, Mbeya, Tanga, Dar es Salaam na Morogoro.

# Mkurugenzi OBC aendelea kusota mahabusu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Arusha, juzi imeshindwa kuendelea na kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Mkurugenzi wa Kampuni ya Otterlo Business Limited (OBC), Isack Mollel, kutokana na mazungumzo yanayoendelea na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kutokamilika.

Akizungumza juzi katika mahakama hiyo, mbele ya Hakimu Nestory Baro, Wakili wa Serikali, Naomi Mollel aliomba kesi hiyo kuahirishwa kutokana na mazungumzo na DPP kutokamilika.

Alisema mshtakiwa ataendelea kuwa mahabusu katika Gereza Kuu la Kisongo lililopo Mjini Arusha kutokana na kesi yake kutokuwa na dhamana.

Baada ya Wakili Naomi kuwasilisha ombi hilo, Hakimu Baro aliahirisha kesi hiyo hadi Januari 13, mwaka huu, itakapotajwa tena.

Mollel anakabiliwa na makosa 10 ikiwamo ukwepaji kodi na utakatishaji fedha haramu, anaodaiwa kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 12.4.

Mollel ni miongoni mwa watuhumiwa walioandika barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), kuomba kukiri mashtaka yanayomkabili.

Mollel anaendelea kusota katika Gereza Kuu Kisongo baada ya kukamatwa Februari 21, mwaka jana, kwa ajili ya kesi hiyo ambayo haina dhamana.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Mhandisi Zephania Chaula (katikati), akigonga glasi kuadhimisha miaka 20 ya Kampuni ya Sprad Traders ya Mji Mdogo wa Mirerani. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Dennis Kimario. **PICHA: GIFT THADEY**

# Zaidi ya watoto 1,000 wanufaika kielimu

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

SHIRIKA la Compassion Tanzania limewezesha kielimu watoto wanaoishi mazingira magumu zaidi ya 1,000 wa Kituo cha Huduma ya Mtoto Babati, kilichopo Kanisa la kinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa kituo hicho, Jonathan Mbesere, wakati akitoa taarifa ya kituo kwenye tafrija iliyofanyika katika kanisa hilo Mjini Babati.

Mbesere alisema tangu kuanzishwa kwa Shirika la Compassion limekuwa mstari wa mbele kutoa huduma ya huruma kwa miaka 67 iliyopita na watoto wengi wa jamii ya kimaskini wamenufaika.

Alizitaja nchi wanazowapa ufadhili watoto wa kundi hilo ni Marekani, Uingereza, Korea, Cuba, Canada na Australia ambao wanawezesha watoto wasio na uhakika wa huduma ili wasome vizuri na kufaulu.

Mbesere alisema Babati kuna vituo sita ambavyo ni Kanisa la Anglicana Singe, Anglicana Nakwa, Kanisa la KKKT Babati, Kanisa la FPTC Babati, Kanisa la Elimu Pentekoste Babati na Kanisa la Mungu lililopo Babati.

Alisema vituo hivyo vimeanza kuwaandikisha watoto kuanzia mwaka 2001, kila kituo kiliandikisha watoto 230 na siyo kila mtoto alikuwa anapata fursa ya kuandikishwa badala yake walikuwa wanapita mitaani na kuwaona watoto wakicheza na kuwabaini wenye hali ngumu.

"Mfano tulikuwa hatutangazi siku ya kuanza kuandikisha hawa watoto, ili tusije kuandika ambao hawatakiwi badala yake tulikuwa tunatembea na kukuta wanacheza labda hawana viatu, nguo na tunawaambia watupeleke kwao na tukifika tulikuwa tunakuta mazingira ni magumu, mtu ukiomba maji ya kunywa unapewa kwa kikombe cha chuma au plastiki na tulikaribishwa kukalia vigoda," alisema.

Vilevile, alisema watoto waliokuwa na uhitaji walichukuliwa kuanzia miaka mitatu hadi saba na kuwapatia huduma zinazotakiwa shuleni kuanzia chekechea mpaka elimu ya chuo kikuu, na mhusika hatakiwi kuzidi miaka 22 kabla hajahitimu elimu ya juu.

Alifafanua kuwa watoto walifanikiwa kuhitimu shahada ni wanafunzi watano, stashahada 10, astashahada 20, kidato cha sita 10, elimu ya kidato cha nne 58 na vyuo vya ufundi walihitimu 105, huku akiwataja walioajiriwa ni watoto 42 na waliojiajiri wapo 142.

Miongoni mwa changamoto zinazowakabili katika kituo hicho ni pamoja na ushiriki wa baadhi ya vijana, katika programu za kituoni kuwa mdogo kutokana na wazazi kutokuwahimiza vijana wao na ufinyu wa bajeti wa kuwahudumia vijana ambao wengi wao wako katika vyuo mbalimbali na hivyo gharama zao kuwa kubwa hasa kwa vituo vyenye umri mkubwa.

Mmoja wa wanufaika wa Compassion International, Anna Jonas, aliiambia Nipashe kuwa walimkuta barabarani walipomwandikisha na alikuwa anaishi na mama yake ambaye hakuwa na uwezo, hivyo Compassion wamemsomesha kuanzia darasa la kwanza mpaka Diploma na sasa ameajiriwa na Compassion Kituo cha Msoga kilichopo mkoani Pwani.

Aliwataka watoto ambao wanasaidiwa na shirika hilo, kujituma katika masomo yao na kutokubali kushawishika hasa watoto wa kike ambao wengine wamekuwa wakidanganywa na wanaume na kuwapachika mimba.

# Vikundi 47 vyanufaika mikopo

**Na Cynthia Mwilolezi,**
MANYARA

VIKUNDI 47 vikiwamo vya wanawake 36, vijana tisa na wenye ulemavu wawili, wamepatiwa mikopo ya thamani ya Sh. milioni 165.8 na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, akizungumza jana katika halmashauri hiyo, alisema kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 walitenga Sh. milioni 207.8, kwa ajili ya mikopo hiyo.

Myenzi alisema kiasi cha Sh. milioni 26.2 bado hakijakopeshwa kwa vikundi kutokana na uhakiki wa vikundi ambavyo vimeomba.

Alisema halmashauri hiyo imeweka utaratibu wa kutenga kiasi kisichopungua Sh.milioni 20 kila mwezi, ili kuhakikisha walengwa wananufaika na mikopo hiyo kulingana na sheria.

"Fedha za mikopo bado tunazo kwa ajili ya kuvipatia vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu, hivyo ni wao kujipanga na kuchangamkia fursa hiyo kikamilifu," alisema.

Alisema kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2018 hadi Aprili 2019, kumefanyika marejesho ya Sh. milioni 58.4 ambazo zinatumika kwa ajili ya uhamasishaji, ufuatiliaji, uhakiki wa vikundi na kuvikopesha vingine.

"Changamoto kubwa ni vikundi vya vijana kuwa na wanachama wanaozidi umri wa miaka 35, hivyo kukosa vigezo na vikundi vya wenye ulemavu kuwa vichache, licha ya uhamasishaji mkubwa kufanyika," alisema Myenzi.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti aliipongeza halmashauri hiyo kwa kutoa mikopo hiyo, kwa vikundi hivyo kwani wametekeleza ahadi ya serikali.

Mnyeti alisema mikopo hiyo ni utekelezaji wa sera ya serikali kuu inayozitaka halmashauri zote nchini, kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu, kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani.

# Mzazi matatani madai ya kumuoza mwanafunzi

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

SHERIA ya Elimu ya Mwaka 1978 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2016 imeanza kuuma, baada ya mzazi mmoja katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, kuburuzwa kortini kwa kosa la kusaidia kumuozesha binti yake ambaye ni mwanafunzi mwenye umri wa miaka 14.

Msichana huyo aliyenusurika kuozeshwa kwa nguvu, akiwa na umri mdogo ni mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Embukoi iliyopo Kijiji cha Munge, Kata ya Donyomoruwa.

Aliyefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Siha, akishtakiwa kwa kosa hilo ni mkazi wa Kijiji cha Munge, Julius Mollel (41).

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka iliyosomwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Simoni Feo, mshtakiwa Mollel anakabiliwa na kesi ya kujaribu kuozesha mwanafunzi ambaye ni mwanawe wa kumzaa.

Katika kesi hiyo inayosikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Siha, Jasmin Abdul, inadaiwa kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Desemba 12, mwaka jana, huko katika Kijiji cha Munge, Kata ya Donyomoruwa. Akisoma hati hiyo ya mashtaka, Feo aliendelea kudai kuwa mshtakiwa alimuozesha binti yake mwenye miaka 14 ambaye ni mwanafunzi wa darasa la sita, huku akijua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

"Mheshimiwa Hakimu, hili kosa alilotenda mshtakiwa aliyeko mbele yako (Julius Mollel) ni kinyume na kifungu 60A (4) cha Sheria ya Elimu kama ilivyofanyiwa marekebisho katika kifungu 22 cha Sheria, namba 2 ya mwaka 2016," alidai mwendesha mashtaka huyo.

Mshtakiwa hata hivyo, alikana shtaka lake na Hakimu Mkazi Mfawidhi Jasmine alitoa masharti ya dhamana na mshtakiwa huyo alitimiza matakwa ya dhamana ya kuweka bondi ya Sh. milioni mbili na kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambuzi wa mkazi kutoka serikali ya Kijiji cha Munge.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Januari 29, mwaka huu, itakapotajwa tena kwa mara ya pili mahakamani hapo.



Ofisa Mtendaji wa Kata ya Machame Narumu, Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Marystella Thomas (aliyeshika kikombe), akimlisha uji wa lishe, mmoja wa watoto waliopelekwa katika uzinduzi wa shughuli za lishe ngazi ya jamii zilizofanyika Kijiji cha Usari jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoto wakutwa athari ya udumavu

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WATOTO 16 kati ya 100 waliofanyiwa uchunguzi wa afya kuhusu udumavu na madhara yatokanayo na kukosa lishe bora katika Kata ya Machame Narumu, Wilaya ya Hai, wamekutwa katika hatari ya kuathiriwa na maradhi hayo.

Ofisa Lishe wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Silvania Kullaya, aliyasema hayo jana, wakati alipokwenda kuzindua shughuli za lishe ngazi ya jamii katika Kata ya Machame Narumu.

"Niseme kweli kwamba ninayo furaha kubwa kwamba Narumu mmekuwa kata ya kwanza kati ya kata zote 17 za wilaya yetu kutekeleza makubaliano ya mkataba wa utendaji kazi na usimamizi wa shughuli za lishe ngazi ya jamii, hongereni sana.

Zaidi alieleza: "Wakati nakuja hapa nilikuta zoezi la upimaji na ugawaji wa chakula linaendelea, wataalamu wangu wa afya wamebaini kwa haraka, kati ya watoto 100 wa kwanza waliotangulia kuchunguzwa, watoto wawili wamekutwa na rangi nyekundu machoni jambo ambalo ni hatari zaidi kiafya na watoto 16 wamekutwa na matatizo ya lishe."

Hata hivyo, takwimu za afya zinaonyesha kuwa tatizo la udumavu wa watoto katika Wilaya ya Hai kwa sasa ni asilimia 29. Ukondefu wa watoto chini ya miaka mitano katika wilaya hiyo ni asilimia 3.1 na kitaifa ni asilimia tano. Kwa mujibu wa Kullaya, pia katika wilaya hiyo uzito pungufu kwa watoto wachanga kwa sasa ni asilimia 10.

Awali Ofisa Mtendaji wa Kata ya Machame Narumu (WEO), Marystella Thomas, alimweleza Ofisa Lishe wa Wilaya ya Hai kuwa kutokana na hali hiyo, wamejipanga kukabiliana na tatizo hilo kwa kufanya tathmini kuhusu hali ya lishe katika vijiji vya Orori, Usari, Tela na Malama, kila baada ya miezi mitatu kuanzia mwaka huu.

Mtendaji huyo alieleza: "Tutafanya tathmini kila baada ya siku 90 kuanzia mwaka 2020 kwa sababu tunataka kutimiza malengo na Dira ya Taifa ya kuondokana na kabisa na vifo vya watoto wachanga kufikia mwaka 2020/2025. Naomba mjue sasa serikali ngazi ya kata hii iko kazini na lishe duni inayosababisha udumavu kwa watoto tutahakikisha inakoma."

Utekelezaji wa mpango huo wa kupambana na lishe duni ni maelekezo yaliyomo katika mkataba wa lishe pamoja na maelekezo ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa Agosti 2017 katika mkutano wa kimataifa wa urutubishaji vyakula.

# Sakata la kuondoa wakulima lafukuta

**Na Godfrey Mushi,** SAME

SAKATA la wakulima 34 wanaoendesha shughuli za kilimo katika eneo la Ngurunga lililopo katika Kijiji cha Gundusine, Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, kuamriwa na Halmashauri ya Wilaya hiyo kuondoka kwenye mashamba yao kupisha mradi wa uhifadhi, bado bichi.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alithibitisha kupokea taarifa kuhusu mgogoro huo siku chache zilizopita, huku akiahidi kuutafutia ufumbuzi ndani ya siku saba kuanzia sasa.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Senyamule alisema: "Siwezi kusema kwa kirefu sana kwa sababu hilo suala bado tunaendelea kulishughulikia, lakini kwangu limefika wiki ya jana, sasa unajua kukiwa na pande mbili ambazo zinatofautiana, ni lazima upate nafasi ya kujua kwa undani kila upande na baadaye utoe ushauri au kutoa maelekezo.

"Kwa hiyo, naomba mnipe muda kwa sababu bado ninaendelea kulishughulikia kama serikali, naomba wananchi wakae kwa amani wakati huu, ambapo jambo hilo linaposhughulikiwa na watapata tu maelekezo sahihi kama kweli wanachosema ni haki yao au vinginevyo."

Mwishoni mwa mwaka jana, wakulima hao ambao waligoma kuhama na kuondoa mazao yao katika eneo hilo, baada ya kuamriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Same kusitisha shughuli zote za kilimo na pia kutoruhusiwa kukanyaga kwenye mashamba hayo.

Wakulima hao wanadai hawataondoka katika ardhi yao kwa kuwa wameishinda serikali mara mbili mahakamani na kupewa haki ya kuendelea kukaa katika mashamba hayo. Kutokana na mgogoro huo kujitokeza, wamemwomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kuingilia kati.

Mkazi wa Kijiji cha Gundusine, anayemiliki shamba hilo katika eneo Ngurunga, Yohana Hondo, alisema wanashangazwa na hatua ya Halmashauri ya Wilaya ya Same kuwaandikia barua ya kuwataka kuacha kulima ndani ya mashamba yao kwa madai kuwa ni eneo la Msitu wa Hifadhi wa Lungwana Ngurunga.

"Hatuelewi kwa nini wanatuamuru kuacha kulima na kufanya shughuli za kilimo katika maeneo yetu ya asili ambayo tuliachiwa na wazee wetu na wakati kuna chakula shambani. Tuliwashinda kesi mara mbili Baraza la Ardhi la Kata ya Hedaru na nyingine ni Mahakama ya Ardhi ya Wilaya.

"Tunaonewa, tunanyanyaswa na kutaka kudhulumiwa haki yetu. Hii si sawa hata kidogo, tunamwomba Rais John Magufuli atusaidie kupata haki yetu kwa sababu anasaidia wengi," alieleza zaidi Simon Samwel.

Katika barua ya Halmashauri ya Wilaya ya Same (Nipashe imeona nakala yake), inaelekeza kusitishwa kwa shughuli za kilimo katika eneo hilo.

Amri hiyo ya serikali, imefafanua kuwa kufanya hivyo ni kukiuka sheria ndogo zilizopitishwa na vikao vyote halali vya kijiji, kata na wilaya pamoja na Sheria ya Misitu ya Namba 14 ya Mwaka 2002.

Pamoja na mambo mengine, barua hiyo imeagiza endapo wananchi hao watakaidi amri hiyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya Simon Samwel na wenzake.

Kwa mujibu wa barua hiyo, eneo la Lungwana Ngurunga ni la msitu wa hifadhi na mchakato wa kuuhifadhi ulianza rasmi mwaka 2011 na kukamilika mwaka 2017 na sheria ndogo ilisainiwa Machi 31, 2017.

ama
ALHAMISI JANUARI 2, 2020
AFYA NA MAZINGIRA


Ukurasa 18

**Viini pori vya mazao vyatafutwa kustahimili janga la tabianchi**


Ukurasa 17

2020; Ethiopia, Sudan na Misri kuafikiana ya Nile?


Ukurasa 14

**Nyuki mkubwa zaidi duniani agunduliwa**




JANGA LA UKEKETAJI

# UNFPA: Ukiwaona mabinti 10, uwezekano mmoja yamemfika

Ukurasa 16



Madaktari wakiwa kazini katika Visiwa vya Samoa. **PICHA: MTANDAO.**

# Krismasi yaishia kukabili mlipuko

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU ya Krismasi kwa madaktari wa nchini Uingereza, ilikuwa fursa yao kupigania afya ya wakazi 5,500 wa visiwa vya Samoa, ambayo ni nchi huru.

Mlipuko wa magonjwa hayo ya kuambukiza, iliifanya serikali ya Samoa kutangaza hali ya hatari nchini humo, Novema mwaka jana.

Kundi hilo la madaktari na wauguzi Waingereza, walilazimika kwenda huko kusaidiana na madaktari wazawa, kutokana na kuzuka maradhi yaliyokwishachukua uhai wa watu 79 hadi Krismasi. Wengi waliofariki ni watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

"Ni jambo fulani hivi, unapofika mahali na kukuta wodini kumejaa wagonjwa ni jambo ambalo hatujalizoea," anasema daktari bingwa, Rachel Anderson, kutoka Edinburgh, akionyesha ishara ya kusikitika.

Inatajwa ni athari zilizoenda mbali kwa koo, moyo na ngozi zimeathirika, jambo ambalo liliwatisha matabibu hao Waingereza wakisema hawajazoea kuyaona hayo.

Wanasema hatua kama hiyo ya kupeleka madaktari na wauguzi, ilishawahi kufanyika kuisaidia Afrika Magharibi kuliko kuwapo maradhi ya ebola kwenye mlipuko mwingine wa maradhi ya maambukizi, kati ya mwaka 2014 na 2015.

AFYA

# Nyuki mkubwa zaidi duniani agunduliwa msituni Indonesia



Ndivyo alivyo nyuki mkubwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**JAKARTA,** Indonesia

WANASAYANSI wanaeleza kugundua uwapo wa kinachoaminika nyuki wakubwa zaidi duniani, wanaopatikana nchini humo.

Inaelezwa wana ukubwa wa kidole gumba na mabawa yenye upana wa sentimita sita. Ni mtazamo mpya, kwa awali walikuwapo na ilidhaniwa wametoweka duniani.

Wataalamu wamempa jina la Wallace, linalotokana na mtaalamu wa viumbe Alfred Russel Wallace, aliyemvumbua mdudu huyo mwaka 1858.

Mtafiti wa sasa alimpiga picha na akaifanya kuwa nembo ya uhifadhi wa mazingira, ikiwa ni hatua ya wanasayansi kupata viumbe vilivyopotea duniani tangu mwaka 1981.

Mwezi Januari mwaka huu wanasayansi walifuata nyao za Wallace katika ziara ya Indonesia, katika juhudi za kupata picha ya nyuki

> "Yaani uzuri na ukubwa wake wa kipekee, nilijisikia raha sauti ya mbawa zake akiruka kuzunguka kichwa changu...sikuamini.



huyo na wakafanikiwa.

"Inafurahisha sana kuona nyuki mkubwa hivi ambaye tulidhania hayuko duniani," anasema aliyepiga picha, Clay Bolt.

Kuhusu makazi yake yanatokana na majani ya magamba ya miti na chakula chake ni mchwa wanaopatikana kwenye miti, huku mvumbuzi wake akitamka:"Ana umbo kubwa zaidi ya wadudu wengine wanaopatikana kwenye spishi (jamii) hiyo".

Uvumbuzi huo umefufua matumaini kuwa misitu inayopatikana katika visiwa vya Moluccas Kaskazini, nchini Indonesia, huenda ina aina za wadudu wengi wa kipekee duniani.

Kwa sasa mahali hapo hakuna sheria mahsusi zinazodhibiti au kusimamia shughuli za kibinadamu katika misitu hiyo.

Eli Wyman, ni mmoja wa watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Princeton, anasema kuwa matumaini ya uvumbuzi huo utawapa motisha ya kufanya utafiti zaidi kuhusiana na historia ya nyuki katika juhudi za kuhakikisha mdudu huyo, uwepo wake hautaangamizwa duniani.

Katika historia ya kitaalamu ni kwamba, alishatoweka miaka 38 iliyopita, ndipo anapatikana katika visiwa vya Moluccas Kaskazini, nchini Indonesia.

Ni kazi iliyofanywa na watafiti wanabaiolojioa kutoka Marekani Kaskazini na Australian, waliomgundua nyuki huyo mkubwa mwenye makazi kwenye mmea wenye urefu wa mita mbili ardhini.

"Yaani kwa uhakika tulipumua kumuona nyuki huyo dume ambaye hatukuamini kama bado anaishi," anatamka, Clay Bolt mshiriki wa kazi hiyo ya ufuatiliaji na bingwa katika jukumu alilopewa la kupiga picha.

"Yaani uzuri na ukubwa wake wa kipekee, nilijisikia raha sauti ya mbawa zake akiruka kuzunguka kichwa changu...sikuamini," anasema.

Hata hivyo, kuna taarifa ya kuonekana kwake mwaka 1991 alipokuwa na miaka 10 tangu atoweke, lakini hakuingia katika ripoti au taarifa yoyote ya kitaaluma, ikiwamo majarida ya kisayansi.

Maisha ya nyuki hao kwa kawaida inaelezwa yanathiriwa na mabadiliko ya kimazimngira, hasa kwenye ufyekaji misitu, ikiwamo mahsusi kwa kilimo.

Msimamizi wa mradi, Robin Moore, ana ufafanuzi: "Tunafahamu kwamba kutowekwa taarifa kuhusu ugunduzi mpya ya kuonekana kama hatari kubwa, lakini niseme ukweli kwamba wavunaji wa mahali hapo (msituni aliko) wanajua kama nyuki hao wapo pale."

Sasa wagunduzi hao wanaeleza faraja yao kuifahamisha rasmi serikali ya Indonesia, kuwapo viumbe hao katika ardhi yake, kitu kinachoiamsha rasmi nayo kuchukua hatua ya kuwatunza.

AFYA

MALARIA & CHANDARUA

# Mbu wanafuta makali ya dawa, watafiti wahaha kusaka mbadala

Na Michael Eneza



Watu wamelala ndanI ya neti. Picha nyingine, mbu aenezae malaria. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

KUPUNGUA nguvu kwa vyandarua vilivyowekwa dawa kumekuwa gumzo miongoni mwa watafiti wa malaria kwa miaka kadhaa. Sasa kunatajwa kuwapo maendeleo makubwa yamefikiwa kugundua chanzo hicho.

Watafiti kutoka Taasisi ya Tiba Magonjwa Nchi za Joto ya Jiji la Liverpool nchini Uingereza, wamechapisha utafiti unaobainisha mkakati ulikuwa haufahamiki, kuhusu jinsi mbu wenye malaria, wanavyoweza kukabili kinga dhidi ya dawa wakitua kwenye vyandarua vilivyowekwa dawa.

Ni utafiti unaotarajiwa kubadilisha muundo wa dawa za kudhibiti mbu kwa kutumia vyandarua, ambao sasa umetawala katika sehemu nyingi.

### WATUMIACHO

Kuna protini ambayo watafiti wameiita 'Sensory Appendage Protein' (SAP2) inayokaa miguuni kwa mbu, aina ya Anopheles Gambiae (wenye asili ya nchini Gambia, Afrika Magharibi) na Anopheles Coluzzii.

Protini hiyo inapokutana na dawa na kutua kwenye chandarua chenye dawa, hujiambatanisha na viini vya dawa hiyo. Hiyo inaifanya dawa hiyo kutoweza tena kumdhuru mbu.

Anakuwa huru kuuma, kunyonya damu na kuacha vijidudu vya malaria kupitia mate, akiweka kitu kama ganzi anayeumwa asisikie kwa haraka.

Utafiti unaonyesha kwamba kadri mbu anavyokuwa na SAP2 kwa wingi, ndivyo anavyokuwa na kinga zaidi iliyowekwa kwenye chandarua.

Ni habari mpya, kwani ni miongo kadhaa sasa vyandarua vyenye dawa vimekuwa silaha madhubuti ya kuzuia malaria katika maeneo mengi ya Afrika.

Hata hivyo, kuwapo hali aina hiyo tiba kukosa nguvu, imezua maswali na kulazimisha kufanyika utafiti kwa wingi, kuhoji kisa cha dawa hizo kukosa nguvu.

Watafiti wamegundua kupungua kiasi kwa dawa SAP2 kunawafanya mbu waliokuwa na kinga dhidi ya chandarua chenye dawa waathiriwe.

Pia imebainika kwamba kuongeza SAP 2, kunawawezesha mbu wasiokuwa na kinga na dawa za vyandarua, kupata kinga hizo, jambo linalotoa uthibitisho mmoja wa kuwapo uhusiano wa kinga ya mbu na dawa SAP2.

Victoria Ingham, aliyeongoza utafiti huo, anasema ugunduzi huo ni mpya katika kutafuta vyanzo vya ustahimilivu wa mbu dhidi ya dawa, jambo linalopunguza ufanisi wa utumiaji vyandarua kuzuia malaria.

> Ushauri wa mtaalamu huyo ni kwamba, kinachotakiwa sasa kufanyika ni kulenga dawa kupewa uwezo zaidi wa kuwakabili mbu, kupitia vyandarua hivyo.

Protini hiyo, kimsingi hutuamishwa miguuni mwa mbu, na inakutana na dawa kwenye chandarua, pale mbu anapotua kwenye chandarua.

Ushauri wa mtaalamu huyo ni kwamba, kinachotakiwa sasa kufanyika ni kulenga dawa kupewa uwezo zaidi wa kuwakabili mbu, kupitia vyandarua hivyo.

Takwimu za kuongezeka malaria barani Afrika licha ya kutumia vyandarua vilivyowekwa, zimekuwa zikileta mshangao na wasiwasi mkubwa katika nchi hizo, pia washirika wahisani.

Utafiti mpya unashauri utumiaji vyandarua vyenye dawa, usababishe ushindani kati ya mbu na dawa, ili kupata wanaostahimili zaidi changamoto ya vyandarua vyenye dawa, ikiwa na maana ya mbu waliofika kwenye chandarua wakarudi.

Hapo ina maana kwamba, ugunduzi wa vidhibiti vya dawa ya mbu kwenye chandarua, unaanza na mbu kutua katika chandarua asiyekufa na kuondoke.

Kinachoangaliwa hapo ni namna mwili wake unaanza kujenga viini vya kustahimili hali hiyo, kwani anakuwa katika namna ya kwamba amechanjwa, anapewa dozi kidogo ya dawa, halafu anaizoea.

Kutokana na mazingira hayo mapya ya mbu kujenga vidhibiti vya dawa mwilini ambavyo vikigusa na kudhibiti dawa yambu anapotua katika chandarua.

### KIDHIBITI KIPYA

Hivi sasa kuna kidhibiti kipya cha uwezo huo wa mbu kilichobuniwa na kuingizwa sokoni kiitwacho 'piperonyl butoxide' (PBO), hicho kimeongezewa katika dawa za chandarua.



Ni nyongeza inayolenga kikemikali iitwayo 'cytochrome P450' inayojengwa na mbu kuunda SAP2, inayomsaidia kuzuiaji dawa za chandarua kufanya kazi.

Kupitia mabadiliko mapya yanayopendekezwa kitaalamu, mbu akitua katika chandarua anatarajiwa atakufa.

Kwa njia hiyo, mchanganyiko wa dawa za kawaida za kuwekwa kwenye chandarua na POB, unaonyesha faraja ya kuwezesha kurudisha mwelekeo wa kupunguza kasi ya kuenea malaria, pale nguvu ya kazi ya chandarua inasuasua.

Hata hivyo, watafiti wanasema tangu matumizi ya dawa hiyo mchanganyiko yaanze, mbu nao wameanza kujenga kinga za ziada kukabili mageuzi ya kinga dhidi yao. Inaelezwa na wataalamu, kuna baadhi ya mbu wanaotarajiwa kutua kwenye chandarua na hawatakufa.

Hao miili yao inaanza kujenga usugu wa dawa hiyo, kwa kuichanganya na vitu vinavyoendana nayo, kwa nafasi ya mvutano wa kikemikali mwilini.

Kila kemikali inakuwa na madhara kwa kuungana na viini mwilini, iwapo ni kemikali rafiki na watafiti waliangalia viini-nasaba kutoka maeneo kadhaa ya nchi za Burkina Faso na Ivory Coast, kunakojulikana kuwapo ustahimilivu mkubwa dhidi ya dawa zinazotumika kujenga udhibiti mbu kaitka chandarua na upokeaji mdogo wa PBO.

Watafiti wanagundua usugu aina mbalimbali ya tiba na kinga kupitia kanuni za utafiti wanazotumia, lakini kadri wafanya uvumbuzi, mbinu kinzani zinachukua nafasi katika vita vya malaria.

Hiyo inajenga maana ya kwamba mapambano katika kudhibiti dawa yanatoka kwa mbu waenezai malaria,kwa njia endelevu, kwani hatua za awali kurudishia makali ya dawa katika vyandarua yanapwaya.

AFY A

JANGA LA UKEKETAJI

# UNFPA: Ukiwaona mabinti 10, uwezekano mmoja yamemfika




Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, akiwa na viongozi wa UNFPA na Asasi ya Hope for Girls and Women Tanzania, baada ya kuzindua ofisi ya Dawati la Jinsia na Watoto katika Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Serengeti. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA.**

**Na Sabato Kasika**

UKATILI wa kijinsia kwa wanawake na hasa ukeketaji, ni tatizo la kitaifa na limeendelea kuwapo.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo Tanzania (UNFPA), linasema kwamba mwanamke mmoja kati ya 10 wenye umri wa miaka 15 hadi 49 nchini, amefanyiwa ukeketaji.

Katika kundi hilo UNFPA inasema asilimia 35 kati yao wamekeketwa, kabla ya kufikia umri wa mwaka mmoja na kuna tofauti kubwa kimikoa, kuhusu takwimu za kuenea matukio ya ukeketaji.

Hapo inatajwa mikoa ya Manyara, Dodoma na Arusha na Mwakilishi Mkazi wa UNFPA, Jacqueline Mahon, anasema ukeketaji umeenea maradufu vijijini kwa asilimia 13, kulinganisha na mijini, ambako ni asilimia tano kwa mujibu wa utafiti waliofanya.

Mahon anasema takwimu zao za Juni 2018, zinaonyesha kuwa ongezeko la idadi ya watu linahatarisha maendeleo na juhudi zilizofikiwa za kukomesha vitendo vya ukeketaji.

Anasema, hiyo inatokana na uhalisia kwamba wasichana wako hatarini kukeketwa zaidi, hivyo kupungua ukeketaji kuliko kushuhudiwa, hakutoshi kuleta uwiano wa uongezeko la idadi ya watu linalotarajiwa.

> **Ukeketaji unakwamisha utendaji kazi wa asili wa mwili wa mwanamke na una madhara makubwa kwa afya ya wanawake na wasichana, ikiwa ni pamoja na afya yao kisaikolojia, kimahusiano na afya ya uzazi.**




Mwakilishi Mkazi wa UNFPA Tanzania, Jaqueline Mahon (katikati), akipeana mkono na Balozi wa Ireland nchini, Paul Sherlock, baada ya ubalozi huo kuipa asasi hiyo ya Umoja wa Mataifa Euro milioni moja za kuboresha afya ya wanawake mkoani Kigoma. Mwingine ni Dk. Majaliwa Marwa wa UNFPA.

### KWA NINI?

Mama huyo anaeleza kwamba, ukeketaji umejikita kwenye kanuni na taratibu za kijamii, imani za kitamaduni na vichocheo vya kiuchumi vinavyoonekana kutumika kudhibiti haja ya tendo la ndoa kwa wanawake.

Mahon anasema, katika jamii nyingi inachukuliwa kama jambo la muhimu kwenye shughuli za jando na unyago, simulizi potofu kuhusu ukeketaji zimekuwa zikirudiwa na mara nyingi kiasi cha kusadikiwa ukweli wake.

Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA-VAWC)), unatafsiri ukeketaji ni mila inayowaathiri wanawake na watoto nchini.

Hivyo, mpango huo unanuwia kukomesha ukatili wa aina zote dhidi ya wanawake na watoto ikiwamo ukeketaji, hatua inayoendana na utekelezaji Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya 2030.

Hivyo, mwitikio wa jumla wa sekta mbalimbali ni muhimu katika ukomeshaji ukeketaji na watendaji katika sekta ya kisheria, ni vyema wakafuatilia wanahakikisha sheria inayozuia ukeketaji unatekelezwa.

### KIFANYIKE NINI?

Jamii pia inasisitizwa kutumia njia mbadala kwenye sherehe za jando na unyango, programu hizo zizingatie makundi mbalimbali yanayojihusisha na ukeketaji wakiwamo ngariba.

Vilevile, kuna maeneo salama yanayopaswa kuanzishwa kwa ajili ya wasichana waliopo hatarini, pia mipango ya sekta ya afya inayotakiwa kujumuisha mikakati ya kuzuia na kutokomeza ukeketaji.

UNFPA inafafanua kwamba njia mbadala katika kutekeleza shughuli za unyago kama sehemu ya programu pana ya kukomesha ukeketaji, ambazo yenyewe hushiriki kwa kutoa msaada wa kuongeza idadi ya wasichana.

Anawataja wasichana hao ni wanaoweza kushiriki kwenye programu tajwa na kuhakikisha kuna upatikanaji wa msaada wa kisaikolojia kwao na wazazi wao.

"Hii ni sehemu ya programu pana inayoungwa mkono na UNFPA, ambayo inahusisha kujenga uwezo wa vyombo vya habari, polisi, mahakama, walimu na waganga wa jadi, katika kuzuia ukeketaji," anasema.

### JINAI ILIKO

Mwaka 1998, serikali ilipitisha sheria iliyofanya ukeketaji kuwa kosa la jinai na tangu wakati huo, matukio yake yalianza kupungua kati ya asilimia 18 wakati huo, kufikia asilimia 10 za sasa.

Ni hatua inayoonyesha kuwapo maendeleo makubwa, katika kuikomesha nchini, na sasa wasichana wengi zaidi wanapitishwa njia mbadala za unyago.

Vilevile matukio mengi zaidi yanaripotiwa na kushughulikiwa na polisi, ikiwa ni matokeo ya mafunzo ya kuongeza uelewa, yanayofanyiwa na maofisa wanaosimamia sheria hatua kwa hatua, katka kukomesha ukeketaji na unyanyasaji kijinsia kwa ujumla.

Hata hivyo, kuendelea kuwapo kwa matukio ya ukeketaji nchini, kunaelezwa kunaleta shaka katika utekelezaji wa mikataba ya haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia.

Mila potofu na zenye madhara bado zinatajwa kuendelea kuwapo katika maisha ya kawaida ya baadhi ya jamii na shaka kuu ni hivi sasa ukeketaji umeelezwa kwa siri kwa watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja.

### MADHARA YALIVYO

Dk. Majaliwa Marwa, ni Mratibu wa Mradi wa Ukimwi wa UNFPA, anayesema ukeketaji una madhara ya muda mfupi na mrefu, kwa anayefanyiwa tendo hilo.

'Ukeketaji unakwamisha utendaji kazi wa asili wa mwili wa mwanamke na una madhara makubwa kwa afya ya wanawake na wasichana, ikiwa ni pamoja na afya yao kisaikolojia, kimahusiano na afya ya uzazi," anasema Dk. Marwa.

Anataja madhara ya muda mfupi ni kifo kutokana na kupoteza damu nyingi na maumivu makali, uharibifu mkubwa wa mfumo wa nje wa viungo vya uzazi na maambukizi ya magonjwa.

> **Madhara ya muda mrefu ni maumivu makali ya muda mrefu, maambukizi yakiwamo ya mara kwa mara ya njia ya mkojo...**

"Madhara ya muda mrefu ni maumivu makali ya muda mrefu, maambukizi yakiwamo ya mara kwa mara ya njia ya mkojo, kupungua kwa raha ya kujamiiana," anasema.

Kwa mujibu wa Dk. Marwa, kisaikolojia mgonjwa anapokuwa na msongo wa mawazo utokanao na maumivu makali, hatari za mgonjwa kujifungua kwa njia ya upasuaji inaongezeka, ikiendana na vifo vya uzazi.

Dk. Marwa anasema ni mazingira yanayochangia watoto kuzaliwa wakiwa na uzito mdogo, pia njiti, njia ya mkojo kwa aliyekeketwa anadhurika zaidi na hata kuugua maradhi ya fistula.

# 2020; Ethiopia, Sudan na Misri kuafikiana ya Nile?



Mradi wa maji wa Grand Ethiopian Renaissance Dam, unaoendelea kujengwa nchini Ethiopia. **PICHA: MTANDAO**

MWAKA mpya unaingia ikitimu siku ya pili, huku kukiwapo matarajio ya mgogoro baina ya nchi tatu kuhusu haki ya matumizi ya Mto Nile unafikia ukingo, panapo majaliwa.

Kwa sasa, mgogoro uko katika suala la matumizi ya Mto Nile, kikuu ni mradi wa Grand Ethiopian Renaissance Dam unaoendelea kujengwa nchini Ethiopia.

Waziri wa Kilimo cha Umwagiliaji wa Sudan, Yasser Abbas, anasema nchi za Misri, Ethiopia na Sudan zinakaribia kumaliza tofauti zao kuhusu matumizi na usimamizi wa bwawa la kuzalisha umeme linalojengwa na Ethiopia.

Ni tangazo lililotolewa baada ya mawaziri wa nchi hizo tatu kukutana mjini Khartoum, Sudan wiki chache zilizopita.

Misri ilikuwa na wasiwasi kwamba mradi wa Grand Ethiopia Renaissance Dam (GERD) unaojengwa wakati uliopo karibu na mpaka wake nchi yake na Sudan kwenye mto wa Blue Nile, utapunguza maji ambayo tayari yameshapungua sana mtoni Nile, sehemu hiyo ikidaiwa chanzo kikuu.

Kwa miezi kadhaa sasa, nchi hizo tatu zimekuwa zikikutana, kutafuta ufumbuzi wa utata huo, ili kupata makubaliano ya pamoja kuhusu matumizi ya bwawa hilo.

Waziri huyo anasema mawaziri wenzake kutoka Misri na Ethopia baada ya kukutana, mapendekezo yameshawasilishwa na mataifa hayo matatu, kuhusu ujazaji bwawa na usimamizi wake.

Abbas anaendelea: "Kulikuwapo na habari muhimu na nyeti za kiufundi tulizobadilishana na kuwezesha kuongezeka ushirikiano kati ya nchi zetu tatu. Hiyo ilikuwa ni pamoja na kueleza maana halisi ya ukame na ukame unaodumu.

"Kulikuwapo na makubaliano kuhusu kuchukua misimamo mipya na kila nchi inakamilisha utafiti wake na tayari kwa kuwasilisha katika mkutano ujao wa Addis Ababa Januari 2 hadi 3, 2020 (kuanzia leo)."

Novemba mwaka jana, mawaziri wa mambo ya nje wa nchi za Ethiopia, Misri na Sudan walikubaliana ifikapo tarehe 15 ya mwezi uliopo, wakutane kutafakari pamoja msuguano walio nao kuhusu bwawa hilo, mradi utakaogharimu dola (za Marekani) bilioni nne.

Ni kikao kinachotarajiwa kufanyika baada ya kukutana na Waziri wa Fedha wa Marekani, Steven Mauchin na Rais wa Benki Kuu ya Dunia, David Malpass, jijini Washington, Marekani.

Mkutano huo ambao ni wa tatu, unatarajiwa kufikia muafaka wa kudumu kumaliza kabisa mvutano uliopo kati ya nchi hizo.

Serikali ya Marekani ilizialika pande hizo tatu, baada ya Misri kutoa wito wa kuwapo mpatanishi kutoka nje, kutokana na uhalisia kwamba pande tatu hizo zimeshindwa kutoa matunda ya mjadala wao.

Ethopia awali ilipinga wazo hilo, ikidai Misri inajaribu kukwepa utaratibu waliokuwa nao. Baadaye, Waziri Abbas akasema wameshakubaliana kurudi na tafsiri ya ukame na jinsi bwawa litakavyofanya kazi wakati wa ukame.

"Bila shaka kuna maelewano mazuri kati ya misimamo ya nchi zetu. Kwa ujumla, mawazo yanafanana, hata hivyo kuna tofauti katika baadhi ya mambo ambayo kila nchi itatafakari kabla ya mkutano wa Addis Ababa," anasema waziri huyo.

Misri kwa upande wake, inasema walitaka kufikia makubaliano ya namna ya kujaza na kuendesha bwawa hilo kwa jambo ambalo imezishawishi nchi zote tatu, ikiamini ndiyo njia sahihi ya kuhifadhi mto kwa maslahi ya pamoja.

Msingi wa migogoro wa Mto Nile, unarejewa na kile Misri inatangaza kama haki yake kupitia tangazo la Gazeti la Serikali la nchi hiyo la Mei 9, mwaka 1929, ambapo walikubaliana mambo kadhaa kuhusu matumizi ya Mto Nile nchi hiyo ikiwa na haki kubwa.

MAZINGIRA

# Viini pori vya mazao vyatafutwa kustahimili janga la tabianchi



Sehemu ya msitu mkubwa duniani wa Amazon na picha nyingine, mkulima akiwa shambani. Vyote ni vyanzo bora vya utafiti wa viini pori. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

WATAFITI wa maeneo mengi duniani kwa kushirikiana na taasisi tofauti za utafiti, wanajenga mikakati ya kupata viini pori kwa ajili ya kuongeza nguvu za mazao ya kawaida, yanayostahimili majanga ya tabianchi.

Inaelezwa, msingi wa utafiti huo ni kuangalia maeneo tofauti duniani mazao yanakotokea na kusambazwa kwingine na kama mimea aina hiyo inahimili mazingira na ukuaji wa porini.

Msingi wa utafiti ni kanuni unayofanana na maisha ya mwanadamu na wanyama, kwamba wakifugwa wanadhoofika.

Watafiti sasa wanaangalia kama eneo ambalo kuna zao, lina asili yake huko na yapo matatizo ya kustahimili mazingira ya sasa, wanaweza kupata viini vya zao pori la aina hiyo, watoe viini ustahimilivu na kuvipandikiza kwa mfumo wa kawaida.

**UTAFITI MPYA**

Ni mkakati uliobuniwa na Mtafiti wa Russia, Nikolai Vavilov, mapema karne iliyopita kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na sasa unaanza kuwa na maana kubwa, kubadili mimea isiyostahili mabadiliko ya tabia nchi, kukwepa kutegemea viini kutoka maabara.

Wataalamu wanasema kwa kutumia viini vya mimea pori kuongeza kiwango cha ustahimilivu wa mimea ya kawaida, bado siyo jambo geni.

Nchini Mexico, kuna mmea wa muhindi pori, ambao mara nyingi unapandwa kando ya mahindi, ili viini vyake vipeperushwe au kufikiwa na wadudu 'poa' wanaotafuta nta kama nyuki, wanaoruka kutoka ua moja hadi lingine, wakiwa na vumbi la viini kutoka ua la kwanza hadi la pili.

> **Taarifa za hivi karibuni zinasema, ni miaka mitatu au minne iliyopita, ndiyo sehemu kubwa ya hifadhi ya viini vya mazao pori imekusanywa.**



Kuna mimea pori ya mazao kama mpunga, nyanya na jamii ya maharage, ambayo katika maeneo kadhaa imeshafanyiwa utafiti na taarifa zinasema majaribio yameshafanyika kwa jumla na mimea bora zaidi imepatikana na stahimilivu.

Unapoingia katika eneo la mimea inayotumika kwa mahitaji tofauti, iwe nafaka au mboga, yote inatazamiwa kutoa viini tofauti vinavyoboresha mazao ya kawaida vikipandikizwa, ingawa utafiti unaweza kuchukua muda kuangalia athari za mabadiliko hayo ya viini, kwa ladha au biashara.

Mfano mmojawapo ni kutumiwa na wanyama, dawa ya binadamu, viungo vya chakula, mapambo na mimea ya misitu na inayotumika kwa mahitaji ya viwanda, kupata mafuta au kamba.

**KIINI CHA TATIZO**

Tatizo linalotokea ni kwenye mbegu zinazotengenezwa maabara, ili kuondoa sukari na linaloambatana na hilo la kutafuta viini pori.

Katika maeneo mengi porini hivi sasa, yanaharibiwa na kusambaa jangwa, kugeuzwa maeneo ya kilimo au makazi, hivyo aina tofauti za mimea yenye faida kwa binadamu inapotea bila kufanyiwa utafiti na viini kuvunwa.

Katika kupanua makazi na mashamba, misitu inapotea na viini pori vya matunda tofauti, navyo hupotelea humo bila ya kufanyiwa utafiti au hifadhi katika maabara, ili kuendelea kufanyiwa majaribio, hata kama mmea unapatikani kirahisi, ikikosa pa kuegemea baadaye.

Hivi sasa, kupungua maeneo ya misitu kunatajwa ni hatarishi kwa usalama wa chakula, kwani siyo tu kunapunguza maeneo ya kilimo, bali hata uwiano-viumbe, mazingira ya mimea, wadudu na wanyama.

Licha ya shauku ya wanasayansi kuzuia kupanuka kwa jangwa, bado ufanikishaji ni ndoto, huku kukiwapo jitihada mpya zaidi za kupanda miti kwa kutupa mbegu na maji kwa ndege.

**INAVYOLINDWA**

Ziko njia mbili ambazo watafiti wanatumia hivi sasa kulinda mimea pori mbadala au pacha na mazao ya kawaida kutopotea, mojawapo ni kuvilinda ndani ya mazingira yake ya kawaida, ambayo ni ngumu na nyingine kupandikiza kwingine.

Njia ya pili, inaondoa ushindani wa kimazingira unaojenga nguvu za mmea au kiumbe kustahimili mazingira magumu, lakini nje yake siyo rahisi kulinda viini mbadala kwa kuviacha porini.

Wataalamu wangependa kujua katika mazingira hayo ya kuongezeka joto duniani, namna gani viini pori vingeshindana na mimea mingine, kwani kila mfumo wa viini vina silaha zake, mazingira yakibadilika ghafla.

Taarifa za hivi karibuni zinasema, ni miaka mitatu au minne iliyopita, ndiyo sehemu kubwa ya hifadhi ya viini vya mazao pori imekusanywa.

Hadi kufikia mwaka 2016, asilimia 29 ya mimea pori inayofanana na mazao, haikuwapo katika hifadhi ya viini, wakati asilimia 24 ya mimea pori mbadala iliyokuwa katika hifadhi hizo, kwa kuchukua sampuli takriban 10 tu.

Inaelezwa, asilimia 70 ya mimea pori mbadala ya mazao ya kawaida ilikuwa inahitaji kukusanywa kwa wingi, kuhakikisha upatikanaji wake katika hifadhi za viini, wakati zaidi ya asilimia 95 ya viini vya mazao pori mbadala havikutafiti vya kutosha kuhusu mazingira.

Pia kulikuwapo na tofauti kuhusu mahali mimea pori mbadala iliyofanyiwa utafiti na matazamio makubwa kuhusu upatikanaji viini vinavyoboresha mazao yaliyopo au viini vyake, ili yahimili wadudu walio tatizo kubwa upande mmoja na ukame upande mwingine.

Soko la mazao hasa mbegu na matunda, nao linahitaji aina za mimea isiyoshambuliwa na wadudu, hali inayosababisha uharibifu mkubwa kwa mboga au matunda kutokuwa na muda baada ya kuvunwa.

Eneo hilo peke yake linatajwa likipatiwa jawabu kutoka viinipori mbadala na itakuwa mchango mkubwa kwa uhakika wa chakula kuondoa uharibifu mkubwa uliopo hivi sasa.

Safari inatajwa bado ndefu, lakini walau utafiti huo unapunguza kasi ya kutengeneza viini mbadala katika maabara.

AFYA

UZAZI MPANGO MISSENYI

# Mganga Wilaya, wenye mji wafunguka kilichojificha

**Na Lilian Lugakingira,** MISSENYI



Baadhi ya kinamama waliojitokeza kupima afya za watoto wao, kupata ushauri na elimu kutoka kwa wataalamu katika kambi iliyoko Kijiji na Kata ya Bugorora, wilayani Missenyi. **PICHA: LILIANA SILIMA**

"MUME wangu aliniambia nikikubali kutumia uzazi wa mpango, nikirudi atanikata mapanga."

Ni ni kauli ya Jovitha (23) mama wa watoto watatu, mkazi wa Kijiji Bugorora, Wilaya ya Missenyi, anayelalamika mume wake alimzuia kupata elimu ya uzazi wa mpango.

Mtoto wake wa kwanza ana umri wa miaka mitano, wa pili miaka mitatu na miezi sita wa tatu miaka miwili na miezi minne.

Anasema alipojifungua mtoto wake wa kwanza mwaka 2014, alimuomba mume wake aanze kutumia njia za uzazi wa mpango ili watoto wake kupishana angalau kwa miaka mitatu, lakini alikataliwa na mume, kwa msimamo mkali.

"Katika kipindi hicho sikutumia kitu chochote. Nilijitahidi kuhesabu (siku za uzazi) ili niepuke kukutana naye siku za hatari, lakini sikuweza kulifanikisha hilo.

"Mtoto wa kwanza akiwa na umri wa mwaka mmoja na miezi minne, nilijifungua mtoto wa pili," anasema.

Anasema kutokana na changamoto aliyoipata ya kulea watoto wawili kwa wakati mmoja wote wakiwa wadogo, alimbembeleza mume akubali atumie njia za uzazi wa mpango, na anataja majibu aliyopokea:

"Bado alikataa na kuniambia hawezi kuruhusu hilo na kwamba nikitoroka nikatumia siku akinigundua atanikata kwa mapanga. Niliona niache kwa usalama wangu. Lakini nimejikuta nikipata tena mtoto wa tatu."

Kilio cha mama huyo sasa ni kwamba, analea watoto wake watatu wote katika umri mdogo, hali inayosababisha afya zao kuathirika kutokana na kukosa huduma sahihi.

Hiyo ni changamoto ambayo anayo Irene, mkazi mwingine wa Kijiji Bugorora, mwenye watoto wawili, wa kwanza ana umri wa miaka miwili na miezi saba na wa pili akiwa na miezi mitano.

Simulizi yake kutoka kizuizi cha mume ni kwamba: "Mume wangu hapendi na mimi nakubaliana naye siwezi kulazimisha. Labda nikifikisha watoto watatu nitamshawishi nione kama atakubali kuniruhusu."

Anasema anapotakiwa kwenda kliniki hana wa kumsaidia, huwabeba watoto wote wawili na kuna wakati mkubwa anatembea, anabeba mdogo tu.

Pia kuna ushuhuda wa Edna, anayeishi katika kijiji hicho, akiwa na mtoto mmoja mwenye umri mwaka mmoja na miezi miwili na hajaanza kutumia njia za uzazi wa mpango, ingawa anadai mume wake si kikwazo.

> **Nafahamu wapo wanaume ambao hawataki kuitikia wito wanapotakiwa kufuatana na wake zao kliniki, lakini si wote, wengine wanabanwa na majukumu ya familia.**

"Mwenyewe ndiye sijaamua kutumia uzazi wa mpango kwa sababu mume wangu anaishi mbali na mimi na haji huku. Mimi ndiye huwa ninakwenda, lakini ninapopanga kwenda nahakikisha sipo katika siku za hatari," anasema.

Anakiri akipata mimba, mtoto wake mwenye umri mdogo ni hatari kiafya, ingawaje anakiri ana mpango wa kuanza kutumia uzazi wa mpango japo si sasa.

"Si kwamba sifahamu maana kila tukienda kliniki tunafundishwa njia tofauti za uzazi wa mpango. Muda bado, ukifika nitaanza ingawa kuna maneno mtaani kuwa matumizi ya njia hizi yanaweza kusababisha mama asipate tena mtoto. Tetesi hizi si kikwazo kwangu bali sijaamua," anasema.

Anatoa ushauri kwa wanaume kuwaruhusu wake zao kutumia njia hizo, kwani wanapowazuia wanasababisha baadhi ya wanawake kutoroka na kutumia kimya kimya, suala ambalo ni hatari endapo watagundulika.

### WANAUME JE?

John Kakuru, ni mkazi wa kijiji hicho anakata dai kwamba wanaume wote hawataki kutoa ushirikiano kwa wake zao au kutozingatia maelekezo, bali muda mrefu wanahangaikia mahitaji ya familia.

"Nafahamu wapo wanaume ambao hawataki kuitikia wito wanapotakiwa kufuatana na wake zao kliniki, lakini si wote, wengine wanabanwa na majukumu ya familia," anasema.

Kuhusu kinamama kutumia njia za uzazi wa mpango haungi mkono, kwa madai si salama.

### WAHUDUMU AFYA

Mhudumu wa Afya Ngazi ya Jamii, katika Kijiji Bugorora, Odiro Adrian, anasema kabla ya kuwapo wahudumu hao, wanawake wengi walijifungulia mitaani kwa wakunga wa jadi, lakini kwa sasa elimu inayotolewa kwa jamii, wengi wanajifungulia vituoni.

Adrian anasema, mama akishagundulika ni mjamzito, wao huanza kumwelimisha kuhusu umuhimu wa kuhudhuria kliniki mapema, kujifungulia hospitali na umuhimu wa kupanga uzazi ili kulinda afya yake na ya mtoto.

"Wapo kinamama ambao mpaka sasa wanaamini wakunga wa jadi wana uwezo wa kuwasaidia hata katika masuala ya uzazi wa mpango, kwa hiyo tunaendelea kuwaelimisha na pia tunawaelimisha wakunga wa jadi ili tushirikiane nao kuwashawishi wanawake wenye ujauzito waende kupatiwa huduma stahiki, " anasema.

Anasema wanawake wanaowaamini wakunga wa jadi wanahatarisha maisha yao, maana dawa wanazopewa hazina kipimo maalumu na zinaweza kuwaathiri wao na watoto walioko matumboni.

"Tunatumia mikutano ya hadhara, vikao na kupitia vyama vya wanawake na wanaume kutoa elimu, ingawa mwitikio kwa kinababa bado ni mdogo," anasema.

Dk. Hamis Abdallah ni Mganga Mkuu wa Wilaya ya Missenyi, ambaye anathibitisha kuwa kuna umuhimu mkubwa kati ya makuzi ya mtoto na uzazi wa mpango.

"Tunaposema uzazi wa mpango, tunamaanisha mwanamke mwenye umri wa kuzaa anapanga anataka kuzaa watoto wangapi na kila baada ya muda gani," anasema.

Anasema mwanamke anapozaa kwa mpango inamwepusha kubeba mimba zilizoko nje ya mpango, lakini inasaidia kupunguza vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi maana kuna wasichana wanapoteza maisha kwa kutoa mimba.

"Kitaalamu inashauriwa mama ampe uangalizi wa kutosha mtoto wake angalau hata miaka mitatu ndipo abebe mimba nyingine, hii inasaidia kupata muda wa kutosha kumhudumia mtoto," anasema.

Anasema utakuta mtoto ana miezi minane lakini tayari mama ana ujauzito, na kuwa kwa hali hiyo hawezi kumhudumia mtoto ambaye katika umri kama huo bado anahitaji uangalizi wa karibu wa mama, wakati huo pia mama anapaswa kuangalia afya ya ujauzito wake.

Dk. Abdallah anasema kuwa mara nyingi watoto wengi wenye utapiamlo wakifuatiliwa utakuta mama hakupanga uzazi na kuwa hali hiyo inathibitisha kuwa kutopangilia uzazi kunasababisha watoto kuwa na lishe duni.

"Lakini kuna njia za uzazi wa mpango ambazo zikitumika ipasavyo zinamzuia mama kupata ujauzito na wakati huo zinamkinga na magonjwa ya zinaa kama ukimwi, kisonono na kaswende," anasema.

Anasema kama mtoto ananyonya halafu mama akapata hayo magonjwa, ina maana mtoto naye anaweza kuambukizwa kutoka kwa

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Mganga Wilaya, wenye mji wafunguka kilichojificha



Mhudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika Kijiji cha Bugorora wilayani Missenyi, Odiro Adrian (katikati aliyevaa kofia), akijaza taarifa za maendeleo ya watoto wao na kinamama waliofika katika kambi iliyoko katika kijiji hicho. **PICHA ZOTE: LILIAN LUGAKINGIRA.**

**INATOKA UK.19**

mama, na akiumwa mara kwa mara afya yake itatetereka na kusababisha lishe kuwa duni inayoathiri makuzi yake.

Kulingana na idadi ya watu walioko Missenyi, kinamama ambao wako kwenye umri wa kuzaa kwa mujibu wa Dk. Abdalah ni 9,612, na wanaotumia njia za uzazi wa mpango ni asilimia 65 ya kinamama hao, kwa mwaka huu.

Anasema wanawake huelimishwa na kuamua wenyewe wanataka kuzaa baada ya muda gani, na kuwa wanapewa njia za kutumia kupanga uzazi kulingana na maamuzi yao.

"Hatufanyi kazi hii peke yetu, tuna wadau tunaoshirikiana nao ambao ni Marie Stops Tanzania, Ingender Health, Shirika la PSI na USAID Boresha Afya, husaidia katika kutoa mafunzo kwa watoa huduma wa afya kwa kuwaongezea uelewa ili wafanye kazi kwa weledi," anasema.

Anasema pia wadau hao wanasaidia katika utoaji wa huduma kupitia ratiba zao kwa kushirikiana na wataalamu wa halmashauri na kuwafikia wananchi hasa wale wanaoishi mbali na huduma, ingawa fedha za wafadhili hao haziingizwi katika akaunti ya halmashauri.

"Yaani mtu anatembea kama kilomita saba kufuata huduma ya uzazi wa mpango haitakua rahisi, lakini anapofuatwa aliko (Huduma Mkoba) inakuwa rahisi kwake kuhamasika," anasema.

Anasema kuna njia tatu za uzazi wa mpango, zikiwamo za muda mfupi, mfano, sindano; za muda mrefu, mfano, vipandikizi na za kudumu ambazo ni kufunga uzazi.

> **Wanawake huelimishwa na kuamua wenyewe wanataka kuzaa baada ya muda gani, na kuwa wanapewa njia za kutumia kupanga uzazi kulingana na maamuzi yao.**

Anasema, ipo dhana potofu kuwa njia za uzazi wa mpango zina madhara lakini si kweli, bali zina maudhi madogo ambayo mama huelezwa kabla ya kuanza kutumia, na kuwa endapo mama atapata maudhi ambayo hakutarajia anashauriwa kwenda kuonana na wataalamu.

Dk. Abdallah anasema kuwa wilaya hiyo ina vituo 37 vya utoaji huduma za afya, miongoni mwake vya serikali ni 27 na kuwa kati ya hivyo vituo 33 vinatoa huduma ya baba, mama na mtoto, ambapo njia inayotumiwa zaidi Missenyi ni vipandikizi.

"Mama anapopata ujauzito anapaswa aanze kuhudhuria kliniki, huko kunakuwa na ratiba ya kutoa elimu kuhusu umuhimu na njia za uzazi wa mpango, na mama akifikia muda wa kujifungua anakuwa tayari ameelewa na kuchagua njia inayomfaa," anasema.

Analia na mfumo dume ambao unaathiri moja kwa moja matumizi ya njia za uzazi wa mpango, na kuwa ili njia hizo zitumike vizuri inabidi kina baba waelimishwe ili waweze kuruhusu wake zao kupanga uzazi kwa lengo la kupata watoto wenye afya bora.

Anasema kitaalamu umri wa mwanamke wa kuzaa ni kuanzia miaka 15 hadi 49, lakini umri salama ni kuanzia miaka 19 hadi 45.

Anasema vipo vitu vinavyoweza kusababisha mama asizae maana



Ofisa Lishe Mkoa wa Kagera, Yusuph Hamis, akitoa taarifa ya hali ya lishe katika Mkoa wa Kagera.

inafika umri mayai yanakuwa hayatengenezwi yaani mama anakuwa hana uwezo tena wa kuingia katika mzunguko wake wa damu wa kila mwezi.

"Inategemea hii hali mama kaifikia kwa umri gani, lakini wengi ni kuanzia miaka 40 na kuendelea," anasema.

Anasema kuhusu idadi ya watoto anaopaswa kuzaa mama kitaalamu kuna magonjwa mbalimbali yenye uhusiano na suala hilo mfano saratani ya shingo ya kizazi, ambayo moja ya sababu inawezekana ikawa kuzaa katika umri mdogo mfano miaka 14.

Anasema pia kitaalamu mama anashauriwa kutozaa watoto wengi maana inaonekana kuwa inachangia kupata saratani hiyo, ingawa si lazima kila mama aliyezaa watoto wengi mfano 15 anapatwa na tatizo hilo.

"Lakini takwimu zinaonyesha kinamama wengi waliozaa katika umri mdogo na waliozaa watoto wengi wanapata hiyo saratani," anasema.

Anasema pia kinamama wengi ambao wamezaa mfano kuanzia ujauzito wa nane, tisa au kumi wako katika hatari ya kutokwa na damu nyingi baada ya kujifungua ambayo inaweza kusababisha kupoteza maisha.

Kuhusu bajeti anasema haipo inayotengwa kwa ajili ya uzazi wa mpango bali huingizwa katika bajeti ya dawa ya halmashauri, na kupitia fedha za mfuko wa afya wa pamoja, kwa mwaka wanapata Sh. milioni 518.

"Asilimia 33 ya fedha hizi ni ya kununua dawa, vitendanishi na vifaa tiba, hizi njia za uzazi wa mpango ni vitendanishi," anasema.

Anasema kutopanga uzazi kunasababisha vifo vitokanavyo na uzazi, na kwa mwaka 2018 kulitokea vifo sita, viwili vilisababishwa na utoaji mimba, viwili kifafa cha mimba na viwili vingine kutokwa na damu nyingi baada ya kujifungua.

"Kwa mwaka 2019 Januari hadi Desemba vimetokea vifo vitano vitokanavyo na uzazi, na sababu ni kama za vilivyotokea mwaka 2018," anasema.

Dk. Abdallah anasema ipo dhana imejengeka kwa kinamama ambao hupata mimba na kuchelewa kuanza kliniki wakisubiri ikue mfano ifikishe kama miezi mitano ndipo aende, na kuwa kufanya hivyo anakuwa amechelewa kupata vipimo ambavyo vingegundua mapema kama ana magonjwa.

"Vipimo vya awali vinagundua kama mama ana magonjwa ili atibiwe mapema, kwa mama anapobaini ana mimba hapaswi kusubiri, anapaswa kuanza kliniki ili kama ana tatizo libainike mapema kwa lengo la kuepusha madhara kwake na kwa mtoto," anasema.

Anataja baadhi ya changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu hayo kuwa ni mfumo dume unaowafanya kina baba kushindwa kufika katika vituo vya kutolea huduma wakiwa na wenzi wao ili wapatiwe elimu ya pamoja.

Anasema vijana wa kike wanapobeba mimba na kulazimika kuzitoa kwa njia zisizo salama, wanasababisha kizazi kupata uchafu ambapo hukaa nyumbani akitumia dawa za miti shamba, na anapozidiwa ndipo hupelekwa hospitali, hali inayoweza kusababisha kupoteza maisha.



# Polisi yaendelea kutafuta watoto waliopotea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limesema linaendelea kufuatilia tukio la kupotea kwa watoto wawili wa familia moja wakazi wa Mtaa wa Shewa, katika Kata ya Mwakibete jijini hapa, ambao walipotea katika mazingira ya kutatanisha.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi ofisini kwake, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, aliwataja watoto waliopotea kuwa ni Faisal Mashaka (5) na Farhana Mashaka (mwaka mmoja na miezi mitano).

Alisema watoto hao ni wa Mashaka Juma, na kwamba walipotea Desemba 28, mwaka jana katika mazingira yenye utata wakati wakiwa nyumbani kwao Shewa. Kamanda Matei alisema watoto hao waliachwa nyumbani na dada wa kazi ambaye alikuwa anaendelea na shughuli nyingine na akawaacha wanacheza nje ya nyumba na wakati wazazi hao wanarudi hawakuwakuta watoto wao.

Alisema baada ya kubaini hivyo walitoa taarifa kituo cha Polisi na wakaendelea kushirikiana na majirani kuwasaka watoto hao bila mafanikio na mpaka sasa hawajapatikana licha ya jitihada zinazoendelea.

"Tunaamini kuwa watoto hao wapo na tutawapata wakiwa hai, tunaendelea kushirikiana na majirani wa bwana Mashaka, lakini tunaendelea kuwashirikisha watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa eneo hilo," alisema Kamanda Matei.

Alisema vilevile wamewashirikisha viongozi wa mila na dini kupitia Umoja wa Jamii Tanzania (Mujata), ambao pia wana mitandao yao ya namna ya kushughulikia matukio mbalimbali hasa ya kuleta amani katika jamii.

Kamanda alisema mpaka sasa haijafahamika sababu ya mhusika au wahusika kuwaficha watoto hao kwa maelezo kuwa angekuwa ana nia ya kupata chochote angekuwa tayari ameanza kupiga simu kudai anachokitaka.

Aliwataka wananchi kuwa makini na watoto wao kwa kuepuka kuwaacha peke yao katika mazingira ya aina yoyote kwa maelezo kuwa wazazi ndio walinzi namba moja wa watoto.

"Kama unaenda sokoni au sehemu yoyote hakikisha unabeba mtoto wako, tujaribu hata kuiga kwa wenzetu wazungu ambao unakuta yuko na kibegi cha kubebea mtoto," alisema Matei.

Alisisitiza kuwa watoto hawawezi kudhurika na wahalifu pekee bali wanaweza wakadhurika hata kwa kugongwa na vyombo vya moto wakati wanapojaribu kuvuka barabara wakiwa peke yao. Matukio ya kupotea kwa watu katika Jiji la Mbeya mpaka sasa watu wanne wamepotea na mtoto mmoja alikutwa akiwa ameuawa na kufukiwa hali iliyosababisha wazazi wake kukamatwa na kuswekwa ndani kwa ajili ya uchunguzi.



Kijana mjasiriamali akimpaka rangi kucha mmoja wa wateja wake katika eneo la Mwanjelwa jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kiwango uzalishaji mpunga hakiridhishi

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

KIWANGO cha mpunga kinachozalishwa katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya hakikidhi mahitaji ya soko la nje ya nchi na hivyo kuwakosesha wafanyabiashara wa Tanzania kupewa mikataba minono na kampuni za kimataifa.

Akizungumza na wakulima wadogo wa Halmashauri za Kyela na Busokelo, wakati wa kuukaribisha Mwaka Mpya 2020, Mkurugenzi wa Kampuni ya Kyela Rice Processor, Moses Mwaipopo, alisema mchele wa Kyela unasifika kwa ubora katika soko la kimataifa.

Alisema pamoja na ubora wa mchele huo, lakini kiwango cha uzalishaji ni kidogo na hivyo kutokidhi mahitaji kutokana na wakulima wengi kutumia mbinu duni za uzalishaji wa zao hilo.

Alisema ndio maana wameanzisha mradi wa kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji kwa kuanzisha mashamba darasa katika vijiji 26 vya halmashauri zote mbili ambazo zipo katika ukanda huo.

Alisema wanatoa elimu hiyo kwa kushirikiana na maofisa kilimo wa vijiji na halmashauri na kwamba wakulima zaidi ya 10,000 wa wilaya hizo watanufaika moja kwa moja na elimu hiyo kupitia mashamba darasa ambayo yatakuwa ya wazi.

"Soko la ndani la mchele wetu halina shida kabisa, tatizo ni soko la nje ambalo linahitaji shehena kubwa kwa mwaka, lakini sisi hatuwezi kukidhi mahitaji kutokana na kiwango kidogo cha uzalishaji," alisema Mwaipopo.

Alisema waliwahi kupata ofa ya kupeleka tani 200 za mchele wa Kyela kila wiki katika Jiji la Lusaka, nchini Zambia, lakini wakashindwa kwa sababu ya uzalishaji kuwa wa kiwango kidogo.

Mratibu wa mradi wa elimu kwa wakulima katika kiwanda hicho, Thobias Mwankonda, alisema lengo la kuanzisha mradi huo ni kuwawezesha wakulima kuacha kilimo cha mazoea na kulima kisasa ili waongeze uzalishaji.

Alisema wakulima wakiongeza uzalishaji hata tija ya kilimo chao itakuwa kubwa kuliko ilivyo sasa na kwamba kipindi hiki ndio mwafaka kufikisha elimu ya aina hiyo kutokana na serikali ya awamu ya tano kusisitiza kuingia katika uchumi wa viwanda ambao unahitaji kuongeza uzalishaji.

Alisema mbali na kutoa elimu, pia wanawaunganisha wakulima na taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo ya kununulia pembejeo pamoja na zana za kilimo.

"Wakulima wetu tunataka waache kilimo cha mazoea, tunataka waachane na jembe la mkono na badala yake watumie mashine za kisasa ili walime maeneo makubwa na kuwa na uwezo wa kuyahudumia," alisema Mwankonda.

Nao baadhi ya wakulima ambao wameanza kunufaika na elimu ya kilimo bora cha mpunga, walisema elimu wanayopata itawasaidia kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kuwa na uwezo wa kumudu mahitaji ya soko.

Mmoja wa wakulima hao, Sande Mwakyusa, alisema walikuwa wamezoea kulima kienyeji, lakini kutokana na elimu wanayopewa wana uhakika watabadili mbinu za uzalishaji.

Alisema hata soko kwa sasa wanalo la uhakika ambalo ni katika Kiwanda cha Kyela Rice Processor ambacho kinasindika zao hilo pamoja na maeneo mengine ya ndani na nje ya nchi.

# Mchungaji ataka 2020 makanisa kusimamia ndoa

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

MCHUNGAJI Kiongozi wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), Forest ya Kwanza jijini Mbeya, Thobis Tambikeni, amesema migogoro na usaliti ndani ya ndoa inajitokeza kwa wingi katika miaka ya karibuni kwa sababu makanisa hayatimizi wajibu wake ipasavyo.

Aliyasema hayo juzi, wakati wa Ibada ya Mkesha wa Mwaka Mpya 2020 iliyoambatana na maombi ya kuwaombea viongozi wa nchi na taifa na kuutangaza mwaka huu kuwa wa kanisa.

Alisema jukumu la kanisa ni kusimamia maadili na kutoa mafundisho kwa watu kuishi kwa kuwa na hofu ya Mungu, lakini inapojitokeza watu wanafarakana katika jamii tafsiri yake ni kwamba kanisa halijawajibika ipasavyo.

"Ukienda mahakamani utashuhudia kesi nyingi za migogoro ya wanandoa na hata watumishi wa Mungu unaweza kuwakuta huko, wakati mwingine watu wanauana kwa sababu ya usaliti kwa hayo kanisa ndio linapaswa kulaumiwa kwa kushindwa kusimamia maadili," alisema Tambikeni.

Alisema mwaka 2020 ni mwaka wa kanisa na kusisitiza kuwa kila mtu anapaswa kujitathmini ni wapi alianguka 2019 ili ajiimarishe kiroho na kimwili katika mwaka huu.

Akinukuu kitabu cha Yeremia 6:16, Tambikeni alisema mwaka 2020 waumini hawapaswi kurudia makosa waliyofanya kipindi cha nyuma, hivyo ni lazima wajifunze ni wapi walikosea na wanatakiwa wafanye nini ili kufanya mambo ya kumpendeza Mungu.

"Injili ya kweli lazima tuitangaze, 2020 msivuke kwa umalaya, kwa uzinzi, sote turudi kwenye toba ya kweli hajalishi ni mtu wa aina gani toba ni ya lazima na inarudisha heshima ya kanisa na taifa wawe mstari wa mbele katika maombi," alisema Tambikeni.

Alimwombea Rais John Magufuli azidi kuongozwa na Mungu katika uongozi wake kama ambavyo huwa anasema kwamba tumuombee ili aendelee kuliongoza taifa kwa haki na kwa maslahi ya wanyonge.

Aliwasihi waumini na wananchi kwa ujumla kumuomba Mungu asimamie uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika mwishoni mwa mwaka huu uwe wa amani ili nchi ipate viongozi bora watakaosimamia rasilimali kwa manufaa ya wananchi.





# Tume kutatua vikwazo vya asasi za kiraia

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKISHO la asasi za kiraia nchini (TANGO) linatarajia kuunda tume ya pamoja itakayosaidia kutatua vikwazo vinavyopatikana katika utendaji kazi wake kuanzia ngazi ya chini hadi taifa.

Akizungumza na Nipashe jana Mkurugenzi wa Tango, NgungeeTepani, alisema lengo la kufanya hivyo ni kutaka kufanya kazi kwa karibu na wabunge katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema wao kama asasi za kiraia wazo la kuanzisha tume ya pamoja lilitokana na mkutano uliofanyika Novemba mwaka jana, jijini Dodoma, uliokuwa na lengo la kuzungumzia changamoto za utendaji kazi wa asasi za kiraia wanazokutana nazo. "Timu hiyo ya pamoja itafanya kazi bila kujali ni maeneo gani inatakiwa kwenda kufanya kazi," alisema Tepani.

Alisema wamepanga kuanzisha tovuti mama ambayo itawawezesha wabunge kupata taarifa ambazo zitawasaidia katika utendaji kazi wao wanapokuwa bungeni kuchangia mijadala inayowasilishwa ikiwemo kuwasilisha hoja za msingi.

Alisema taarifa zitakuwa kila baada ya miezi mitatu, ambapo alisema anaamini tovuti hiyo itakuwa msaada mkubwa kwa wabunge pamoja na wao kama asasi za kiraia.

Alisema lengo lao ni kuona ushirikiano unaimarika kati yao na wabunge kwa kuwa wote wanafanya kazi za kijamii kuhakikisha wananchi wananufaika na utendaji kazi wao wa kila siku katika majimbo yao.

Akizungumzia kuhusiana na mpango mkakati wa mwaka huu, alisema wamejipanga kuhakikisha wanakuwa na mikutano ya mara kwa mara ili kufanikisha malengo waliojiwekea kwa mwaka 2020.

Alisema wamejipanga kutekeleza yale yote waliopanga katika mkutano wa mwaka jana ambao wanaamini mafanikio yataonekana.

Hata hivyo, aliwaomba wabunge kuendelea kushirikiana kwa pamoja ili kufanya kazi kwa lengo la kuisaidia Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema wana kila sababu ya kujivunia yale waliyofanya mwaka jana, lakini mikakati ya mwaka huu nayo wamepanga kuifanikisha kama walivyojiwekea.



Baadhi ya waumini wa Kanisa la Tanzania Fellowship of Churches mkoani Dodoma, wakisherehekea kwa kusifu nyimbo za dini katika mkesha wa kuukaribisha mwaka mpya wa 2020 uliofanyika juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mchungaji avipa somo vyama vya siasa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MCHUNGAJI Kiongozi wa Kanisa la Tanzania Fellowship Of Churches (TFC) Central Dodoma Christian, Rose Amani, amevitaka vyama vya siasa nchini kukaa meza moja na kuondoa tofauti zao ili kuepukana na machafuko ambayo yanaweza kutokea.

Mchungaji Rose alisema kuwa mwaka 2020, ni wa kuwa tofauti na kujitakasa na kuondokana na tabia ya kujengena chuki au kuchukiana, jambo ambalo halijengi jamii na taifa kwa ujumla.

Alitoa rai hiyo juzi wakati wa mkesha wa kuukaribisha mwaka mpya 2020, kitaifa ulioambatana na dua maalum,uliofanyika katika kanisa la Tanzania Fellowship Of Churches jijini Dodoma.

Mchungaji huyo alisema mwaka 2020 ni wa uchaguzi, hivyo hakuna sababu ya wanasiasa kusigana au kutofautiana kati ya chama na chama bali wanatakiwa kukaa meza moja ili kufikia mwafaka.

Alisema wanasiasa wanatakiwa kuwa na roho ya kusameheana kupatana kati ya vyama vya siasa pamoja na kuvunja roho za visasi.

Aidha, Mchungaji Rose alisema kuna haja ya kufanya maombi ili roho za Watanzania kuwa na tabia ya kupendana pamoja na kumwomba Mungu ili kuepusha matengano na chuki zinazotokana na mitazamo ya kiimani. Naye Mchungaji Frank Kunoga kutoka Kanisa la Calval Assembles of God (CAG) kutoka Kondoa akiombea kuimarika kwa uchumi wa nchi, alisema kuwa bila kuwa na uchumi imara ni ndoto kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025.

Alisema ili kuwa na uchumi mzuri, ni lazima Mungu asaidie uchumi usiyumbe na wala usiteteleke vinginevyo nchi itaendelea kukaa katika hali ya madeni.

Akiombea uchaguzi mkuu, Irine Bwire, muumini wa kanisa hilo alisema kuwa kama Watanzania hawataomba kwa bidii ili wapatikane viongozi wenye hofu ya Mungu hali itakuwa mbaya.

Mbali na kutaka Watanzania wamwombe Mungu ili wakati wa uchaguzi apatikane kiongozi bora. Pia alisema Wakristo na madhehebu mengine waombe kwa bidii ili matokeo ya uchaguzi yawe ya haki.

## Takukuru yabana makandarasi maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Dodoma imewaagiza makandarasi ambao miradi yao haikutoa maji warudi 'site' kutekeleza upya miradi hiyo kwa sababu uchambuzi bado unaendelea.

Makandarasi wanaotakiwa kufanya hivyo ni wale waliopewa zabuni kutekeleza miradi hiyo toka mwaka 2012 hadi 2015.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, wakati akizungumzia mradi wa maji wa kijiji cha Kelema ulioanza kutoa maji hivi karibuni baada ya Takukuru kuingilia kati na kubaini udanganyifu uliofanyika wakati wa utekelezaji.

Alisema moja ya kazi ambayo Takukuru imejipanga kuhakikisha miradi mbalimbali ya maendeleo inatekelezwa ni pamoja na kuendelea na uchambuzi wa miradi ya maji, ambayo ilitekelezwa chini ya kiwango kuhakikisha makandarasi wanarejea site kutekeleza miradi hiyo ili wananchi wapate maji.

"Naomba makandarasi wote ambao walikutwa na dosari kuhakikisha wanarejea kwenda kurekebisha miradi hiyo, serikali inaendelea kufanya uchambuzi kujua nini cha kufanya," alisema Kibwengo.

Alisema suala la jinai halifi hata kama mtu alilipwa fedha na hukutekeleza ipasavyo ni vema urudi site kwa sababu mkono wa sheria utawafikia.

Alisema Takukuru baada ya kukabidhiwa kuchunguza miradi hiyo, wanaendelea kuifanyia kazi ili kuhakikisha thamani ya fedha ambazo zinatolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo zinafanyiwa kazi ipasavyo.

Alisema makandarasi ambao wanafahamu miradi yao haikutoa maji, ni vema warudi site kufanya kazi katika miradi waliokabidhiwa kuhakikisha inatoa maji.

Akizungumzia kuhusu mradi wa Kijiji cha Kelema, alisema baada ya kukabidhiwa kuuchunguza walibaini ubadhirifu na kuamuru mkandarasi kurejea upya na hatimaye mradi huo umeanza kutoa maji.

Alifafanua kuwa makandarasi wote wanapaswa kuwa makini na miradi wanayokabidhiwa na serikali kwa sababu inatumia fedha nyingi kuhakikisha wananchi wanapata maji mijini na vijijini.

Kutokana na hali hiyo, alisema wananchi wanapaswa kutoa ushirikiano pale wanapoona mradi umetekelezwa chini ya kiwango.

Alisema kila mmoja anapaswa kuwa askari wa mwenzake, hivyo ni vema kutoa taarifa pale unapoona mkandarasi anafanya kazi kinyume cha maelezo ili kuisaidia serikali ambayo imetoa kipaumbele katika sekta ya maji.



## Dk. Shein afurahishwa kasi ya wageni Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuwa wananchi wa Zanzibar wameonyesha mapenzi makubwa, umoja na mshikamano baina yao na miongoni mwa wageni wanaokuja kuitembelea nchi katika kipindi chote cha mwaka 2019.

Akizungumza na wananchi kupitia vyombo vya habari katika kuukaribisha Mwaka Mpya wa 2020, alisema amani, utulivu na umoja vilivyoendelezwa vimewezesha kuitekeleza mipango ya maendeleo kwa mafanikio makubwa ambapo umepelekea uchumi wa Zanzibar kuendelea kukua kwa asilimia 7.1 kwa mwaka 2018 ikilinganishwa ma asilimia 6.8 kwa mwaka 2016.

Rais Dk. Shein alisema kuwa hali ya amani na utulivu iliyopo nchini imeongeza mshikamano na mapenzi baina ya wananchi na kusema kuwa nchi iko salama na kila mwananchi anafanya shughuli zake bila ya bughudha.

Alisema hali hiyo imechangia kuimarika kwa sekta ya utalii na watalii na wageni mbali bali walitembelea Zanzibar katika mwaka 2019, jumla ya watalii 477,579 walitembelea Zanzibar katika kipindi cha Januari hadi Novemba 2019.

Alieleza kuwa kuimarika kwa amani na utulivu pia, kulipelekea taasisi na mashirika mbalimbali ya kikanda na kimataifa walivutiwa kufika Zanzibar na kufanya mikutano yao ukiwamo mkutano wa Jumuiya ya Majaji na Mahakimu wa Afrika Mashariki (EAMJA), Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Mkutano wa Wabunge wa Jumuiya ya Madola.

Alisema kuwa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020 ya Zanzibar ambayo sambamba na Ilani ya Uchguzi Mkuu ya CCM ya 2015/2020 umefanyika kwa ufanisi na kukaribia kukifikia kiwango cha chini cha nchi za kipato cha kati cha Dola za Kimarekani 1,040 kwa mujibu wa vigezo vya kimataifa.

"Tumemaliza mwaka bila ya shida yoyote ya upatikanaji wa bidhaa za chakula na bidhaa nyingine muhimu kwa maisha ya kila siku ya wananchi wa Zanzibar," alisema.

Alisema kuwa miongoni mwa mafanikio makubwa yaliopatikana katika mwaka uliopita ni kuimarika kwa sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji na jitihada za serikali na wakulima zimewezesha kupata mafanikio makubwa katika sekta ya kilimo kwa kuongeza mavuno ya mazao ya chakula hasa mpunga, mboga na matunda.

Alisema kuwa kwa mwaka 2018/2019 wakulima walivuna tani 47,507.1 za mpunga kutoka tani 39,682.7 mwaka 2017/2018 ambapo mafanikio hayo kwa jumla yamewezesha kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 60 kutoka asilimia 51 mwaka 2011.

Kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, Rais Dk. Shein alisema kuwa serikali imeanza hatua za awali za kuanzisha Kampuni ya Uvuvi ya Zanzibar (ZAFICO), kushika nafasi ya Shirika la Uvuvi lililokuwapo kabla.

Vile vile, mwaka 2019 boti ya kisasa ya uvuvi inayoitwa SEHEWA II ilinunuliwa kwa Sh. bilioni 1.33 na tayari Kampuni ya ZAFICO imepanga kununua boti nyingine moja ya uvuvi.

Rais Dk. Shein alisema kuwa mwaka 2019 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliendeleza juhudi za utafutaji wa mafuta na gesi asilia, juhudi ambazo zilijumuisha tafsiri za taarifa za mitetemo ambayo ndio itakayoonyesha miamba au maeneo yanayosadikiwa kuwa na mafuta na gesi asilia.

Alisema katika mwaka 2019 mafanikio makubwa yamepatikana katika sekta za jamii ikiwamo utekelezaji wa sera ya kutoa huduma za afya na elimu bure na bajeti ya Wizara ya Afya imeongezeka mara 9.6 kutoka Sh. bilioni 10.81 mwaka 2010/2011 hadi Sh. bilioni 104.24 mwaka 2019/2020.

# Kiswahili chapendekezwa kiwe ngazi shahada

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema ni muhimu kwa programu ya ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya pili (TEKSOL), ikaanzishwa katika ngazi ya stashahada na shahada, ili vijana wengi zaidi waweze kujifunza namna ya ufundishaji wa lugha hiyo.

Dk. Shein amesema hayo katika sherehe za mahafali ya 15 kwa wahitimu wa mwaka wa masomo 2018/2019 ya Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), zilizofanyika, Mkoa wa Kusini Unguja.

Dk. Shein ambaye ni mkuu wa chuo hicho, alisema uanzishaji wa programu hiyo utasaidia kuongeza fursa za ajira kwa vijana wa Zanzibar kwenda kufundisha Kiswahili ndani na nje ya nchi.

"Kwa hivyo, sisi ambao lugha ya Kiswahili ndio lugha yetu mama, lazima tuwe mbele na tuamini kuwa tuna uwezo mkubwa zaidi wa kufundisha Kiswahili fasaha, kwa kuwa ndicho kilichotulea na kutukuza na vile vile, tunaujua utamaduni wake," alisema.

Aliwataka wahitimu wa masomo hayo kufanya kila juhudi kutafuta fursa za kwenda kufundisha Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani, ikiwamo za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Pia wahitimu kuchukua hatua ya kuwasiliana na taasisi zinazohusika pamoja na kufuatilia katika mitandao, ili kuhakikisha wananufaika na fursa hizo. Alieleza kuwa katika hafla ya ufunguzi wa Kongamano la Kimataifa la Kiswahili lililofanyika hivi karibuni, alifurahia hatua ya kukabidhiwa idadi kubwa ya tasnifu za wataalamu waliohitimu katika fani za lugha ya Kiswahili katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu na Shahada ya Uzamili kutoka vyuo vikuu mbalimbali nchini, ikiwamo SUZA.

Alisema kuwapo kwa hazina kubwa ya wataalamu wenye shahada za juu katika Kiswahili, ikiwamo Tasnifu 17 za Uzamivu (PhD) na 95 za Uzamili (Masters), kunapaswa kwenda sambamba na maandalizi ya kuanzisha shule ya tafsiri na ukalimani.

Alitaka juhudi zifanyike kuimarisha shule za Kiswahili na lugha za kigeni ili ifikie kuwa kitivo kikuu na kuifanya Zanzibar kuwa kituo bora, "Center of Exellence".

"Ni muhimu tuongeze vifaa na vivutio vingine ili kuwafanya wageni wanaotaka kujifunza lugha ya Kiswahili washawishike kujiunga na taasisi hiyo, tuandae mipango imara, tuwe na mikakati madhubuti pamoja na kutafuta nyenzo, kwa kuwa wazee walisema mti hauendi ila kwa nyenzo," alisema.

Naye Makamu Mkuu wa chuo hicho cha SUZA, Zakia Abubakar, alisema kuendelea kufanya vizuri kwa wahitimu wa kike ni jambo la kupongezwa linaloonyesha matumizi mazuri ya uwezo wao katika masomo.

Alisema katika mahafali ya mwaka huu, wahitimu wa kike wameendelea kufanya vyema kwa kupata asilimia 54 dhidi ya 46 za wanaume, huku mwanafunzi bora wa jumla akiwa mwanamke.

Alisema chuo hicho kinakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwamo ya ukosefu wa bweni, hususan katika kampasi ya Tunguu inayohusisha ukosefu wa maeneo ya utoaji wa huduma kitaaluma kwa wanafunzi.

Jumla ya wahitimu 1,719 kutoka fani mbalimbali wamefaulu na kutunukiwa vyeti, stashahada pamoja shahada, hatua inayokifanya chuo hicho kufikisha jumla ya wahitimu 12,000 katika kipindi cha miaka 15 sasa.



Mkuu wa Wilaya ya Mjini Unguja, Marina Thomas aliyeshika tolori, akiwa katika harakati za kufanya usafi wilayani humo, mjini Unguja. **PICHA NA RAHMA SULEIMAN**

# Wapongezwa kuboresha miundombinu elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wa Shehia ya Bambi, Wilaya ya Kati Unguja wamepongezwa kwa jitihada zao za kuboresha miundombinu ya elimu. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alitoa pongezi hizo baada ya matembezi mafupi ya kuangalia ujenzi wa madarasa nane ya Shule ya Bambi.

Alisema wananchi watakapokuwa mstari wa mbele katika suala la kutatua changamoto za maeneo yao inairahisishia serikali kukamilisha kwa kiasi kikubwa changamoto hizo.

Alieleza kila mmoja kwa nafasi yake anatakiwa kuwa mzalendo katika kazi za kujenga taifa ili kuhakikisha maendeleo ya sehemu husika yanafikiwa. Alimshukuru mbunge wa kuchaguliwa wa Jimbo la Uzini na wa Viti Maalumu mkoani humo, Mwatumu Dau Haji, kusaidia vifaa mbalimbali katika mwendelezo wa ujenzi huo.

Alisema ofisi yake itaangalia hatua ya ujenzi huo itakapofikia baada ya utekelezwaji wa ahadi za wabunge hao na kuangalia namna ya msaada atakaoutoa katika kufanikisha ujenzi wa madarasa hayo pamoja na ujenzi wa barabara za ndani za shehia hiyo.

Aliitaka kamati hiyo ya maendeleo endapo wabunge hao watachelewa kutekeleza ahadi walizoziweka wawasiliane kwa lengo la kutatua tatizo hilo na fedha watakazozileta wabunge hao zitatumika kwa mahitaji mengine.

Naye Salim Mwinyi Rehani, Mbunge wa Jimbo la Uzini na Mwatumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalumu, Mkoa wa Kusini waliahidi kutoa msaada wa vifaa vya ujenzi lengo ni kuhakikisha ujenzi huo unakamilika kwa wakati uliokusudiwa.

Kwa upande wake Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo wa Shehia ya Bambi, Hamad Ali Haji, alisema wanaendelea na ujenzi wa madarasa hayo kwa nguvu za wananchi na wabunge na wanategemea kukamilisha ujenzi huo kabla ya uchaguzi mkuu.



Waumini wa Kanisa la Romani Katoliki Parokia ya Ngokolo Shinyanga Mjini wakisali kwenye mkesha wa kuukaribisha Mwaka Mpya 2020. Kulia mwenye kilemba chekundu ni Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Operesheni ilivyopunguza ajali barabarani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MAKOSA ya usalama barabarani yaliyosababisha ajali kwa mwaka 2019 yanaelezwa kupungua, kutokana na operesheni nyakuanyakua iliyokuwa ikifanyika mara kwa mara katika mkoa huo.

Operesheni hiyo ambayo iliongozwa na Mkuu wa Usalama Barabarani mkoani Pwani, Mosi Ndozero, madereva wakorofi, wasiofuata sheria za barabarani, wamekuwa wakitozwa faini, kufikishwa mahakamani na wengine kupewa mtihani wa sheria za usalama barabarani.

Akizungumza Mjini Kibaha kuhusiana na taarifa ya makosa ya usalama barabarani, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Nyigesa Wankyo, alisema, mwaka 2018 ajali 41 ziliripotiwa wakati mwaka 2019 zimeripotiwa ajali 32.

Wankyo alisema ajali zilizosababisha majeruhi kwa mwaka 2018 zilikuwa 100 wakati mwaka 2019 ni 64 zilizoripotiwa.

Kutokana na hali hiyo Kamanda Wankyo aliwataka watumiaji barabara wote kuzingatia sheria za usalama barabarani kupunguza matukio ya ajali katika mkoa huo.

Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Pwani, Mosi Ndozero, alisema, wamefanikiwa kupunguza ajali kwa asilimia 7.5 kutokana na elimu ya sheria za usalama barabarani inayotolewa mara kwa mara kwa watumiaji.

"Tumeazimia Mkoa wa Pwani bila ajali inawezekana, madereva wameona moto ni mkali sasa wanatii sheria wameanza kujirekebisha na wale wasiobadilika tunawapeleka mahakamani," alisema.

Aidha, alisisitiza kuwa madereva wanatakiwa kutii vivuko vya watembea kwa miguu kuepuka ajali, ambapo pia alisema wanaendelea na operesheni nyakuanyakua hadi watakapohakikisha kila mmoja anafuata sheria za barabarani na hakuna ajali.

# Tuico yafunguka wafanyakazi kuheshimu ajira

**Na Sabato Kasika**

WAFANYAKAZI wametakiwa kuepuka vitendo vinavyoweza kuwaharibia ajira zao, badala yake waziheshimu wakitambua ndizo zinazowasaidia kuendesha maisha yao ya kila siku na familia zao.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) Kanda ya Dar es Salaam, Hassan Athuman ndiye aliyesema hayo juzi.

Athuman alikuwa akizungumza na wafanyakazi wa kiwanda cha kutengeneza mabomba cha Tanzania Steel Pipes Ltd (TSP), kwenye hafla ya kutoa zawadi kwa wafanyakazi bora wa kiwanda hicho.

"Kila mfanyakazi anatakiwa kutimiza wajibu sehemu yake ya kazi kwa kutambua kuwa ajira aliyonayo ndiyo inayomfanya aendeshe maisha yake ya kila siku pamoja na familia yake," alisema Athuman.

Alisema, wapo baadhi ya wafanyakazi katika maeneo mbalimbali ambao huwahi kazini, lakini hawawajibiki ipasavyo na kusababisha na ni wepesi kudai haki bila kutimiza wajibu. Aliwataka wafanyakazi wa TSP wasiwe miongoni mwa hao wasiozingatia wajibu wao, bali waonyeshe mfano bora kwa kufanya kazi kwa bidii, ili kuongeza tija na kujiletea maendeleo.

Aidha, Athuman alitaja wajibu na haki za viongozi wa Tuico kwa mwajiri katika uboreshaji wa utendaji kazi ni pamoja na kuboresha na kuendeleza hali nzuri ya wafanyakazi kazini. "Wajibu mwingine ni kushirikiana na kujadiliana na waajiri kuunda mabaraza ya wafanyakazi, kudumisha amani mahali pa kazi na kujadili, kufunga na kusimamia utekelezaji wa mikataba ya hali bora za kazi," alisema.

Naye Mwenyekiti wa TUICO tawi la kiwanda hicho, Ernest Mwenura, alisema chama hicho kina ushirikiano mzuri na mwajiri na kwamba hata maslahi ya wafanyakazi yanazingatiwa. "Pamoja na hayo, bado kuna haja ya kuboresha zaidi mkataba wa hali bora kwa manufaa ya wafanyakazi wa kiwanda hiki, hivyo nimuombe mwajiri wetu alione hilo," alisema Mwenura.

Kwa upande wake Meneja Msaidizi Rasilimali Watu, Peter Mlowe, alitaja tatizo lililopo kiwandani hapo kuwa ni baadhi ya wafanyakazi kutozingatia sheria ya afya na usalama mahali pa kazi.

"Sisi tunafahamu kuwa mahali pa kazi na mazingira ya kazi yanatakiwa kuwa salama bila hatari ya afya na vifaa vinatakiwa kuwapo, hapa kiwandani vipo, lakini baadhi ya wafanyakazi kwa makusudi hawavitumii," alisema Mlowe.

Alisema, wafanyakazi wa aina hiyo wanaweza kuumia na kwenda kulalamika kwenye vyama vya wafanyakazi wakidai kwamba wamepata madhara kwa sababu hawana vifaa na kumbe vipo lakini hawavitumii.

TSP tunatambua na kuzingatia usalama wa wafanyakazi wetu na niwaombe wale ambao huwa hawataki kutumia vifaa kwa ajili ya usalama wao, waache mtindo huo, wasihatarishe maisha yao," alisema.

# Wakulima korosho waahidiwa malipo

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

SERIKALI imeahidi kufuatili kwa karibu kuhakikisha kila mkulima aliyeuza korosho katika msimu wa mwaka 2019/2020 analipwa fedha zake.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro, wakati akijibu malalamiko ya wakulima wa Kijiji cha Marumba.

Mtatiro alisema kuwa miongoni mwa vikwazo vilivyosababisha kuchelewa kwa mauzo ya korosho za wakulima ni kuwapo kwa tatizo la kuchelewa kwa magunia ya kuwekea korosho za wakulima, jambo ambalo limeshashughulikiwa.

Alisema mahitaji ya maguni ya kuhifadhia korosho gafi wilaya ilikuwa na uhitaji wa magunia 395,000, na kwamba zaidi ya asilimia 90 zimeshapokelewa na kiasi kidogo kilichobakia kinatarajiwa kuwasili kabla ya Jaruari 5, mwaka huu.

Awali wakulima wa korosho katika kijiji chicho ambao walikuwa wakiongelea kero mbalimbali kwa wataalamu wa Asasi ya Tupace, walibainisha kuwa hadi Desemba 30, mwaka jana viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika wa wakulima (AMCOS) walikuwa wamelipa minada miwili kati ya minne waliyouza korosho zao.

Walisema ingawa hadi sasa jumla ya minada saba ya mauzo ya korosho imekwishafanyika wilayani humo, wakulima wengi katika maeneo yaliyopo pembezoni korosho zao zilikwama kuuzwa kutokana na ukosefu wa magunia, hivyo wakaiomba serikali kuandaa utaratibu wa kupeleka magunia mapema katika misimu ijayo ili kuwaondolea kero hiyo.

Mwajuma Selemani na Mohamed Yasin, ni miongoni mwa wakulima walionyesha katika mkutano huo na kueleza kuwa kitendo cha kucheleweshwa kwa malipo yao kinawafanya washindwe kumudu kuhudumia familia zao ikiwamo kupeleka watoto wao shule mwezi huu.

Mkurugenzi wa Asasi ya Tupace, John Nginga, alisema asasi yake ilibuni mradi huo baada ya kubaini kuwapo kwa malalamiko mengi kutoka kwa wakulima hasa kipindi cha mauzo ya korosho zao.

Alisema kupitia asasi hiyo wamekuwa wakifanya kazi kwa kushirikiana na viongozi wa serikali kwa lengo la kutatua kero za wakulima kwa haraka.

HABARI KIMATAIFA

# Mali za binti wa Dos Santos zakamatwa

**LUANDA,** Angola

MAHAKAMA ya Angola imeagiza kukamatwa kwa mali na akaunti za benki za mtoto wa Rais wa zamani wa Angola, Jose Eduardo dos Santos.

Kukamatwa kwa mali hizo, kunatokana na mipango ya serikali iliopo kukabiliana na ufisadi katika taifa hilo lenye utajiri mkubwa wa mafuta.

Utawala wa Rais Joao Lourenco, unataka kuchukua takriban dola bilioni moja ambazo umekuwa ukimdai Isabel Dos Santos, ambaye anaaminika kuwa mwanamke tajiri Afrika na washirika wake.

Isabela amepinga madai hayo na kusema kwamba hajafanya makosa yoyote wakati baba yake alipokuwa madarakani.

**Nimegundua kwamba kesi ilifanyika kwa siri nchini Angola na uamuzi wa kukamatwa, kutangazwa hakukufanyika mbele ya mawakili kutoka upande wangu, mbali na wakurugenzi wa kampuni zangu.**

Akidaiwa kuwa mwanamke tajiri zaidi barani Afrika, Isabela anakadiriwa kuwa na mali yenye thamani ya dola bilioni 2.2 kwa mujibu wa jarida la Forbes.

Mwanamke huyo mwenye umri wa miaka 46 anaishi ughaibuni baada ya kuondoka Angola kwa hofia maisha yake.

Mwanamke huyo anaendesha biashara kubwa akiwa na kampuni nchini Angola na Ureno, anamiliki hisa katika kampuni ya Nos SGPS.

Mahakama iliagiza mali ya Isabela kuzuiwa ikiwamo akaunti zake za benki mbalimbali na hisa zake katika kampuni nchini humo, ikiwamo ile ya Unitel na Benki ya Fomento de Angola BFA.

Katika taarifa alisema kwamba anashutumu kile alichokitaja kuwa shambulio linaloshinikizwa kisiasa.

"Nimegundua kwamba kesi ilifanyika kwa siri nchini Angola na uamuzi wa kukamatwa, kutangazwa hakukufanyika mbele ya mawakili kutoka upande wangu, mbali na wakurugenzi wa kampuni zangu," alisema Isabela kwenye taarifa hiyo.

Aliongeza " Tuliambiwa kuhusu uamuzi huo baada ya kuamuliwa nyuma yetu. Nimetumia muda wa saa 24 nikijaribu kuwahakikishia wafanyakazi wangu na familia zote zilizoathiriwa na agizo hilo kwamba hatutakubali. Nitatumia kila njia Angola na sheria za kimataifa kupigana dhidi ya agizo hili na kuhakikisha kwamba ukweli unajulikana".

Isabela Dos Santos alijipatia umaarufu mkubwa 2016 wakati baba yake akimteua kwa njia ya utata kuwa mkuu wa kampuni ya mafuta inayomilikiwa na serikali Sonangol.

Alifutwa kazi katika wadhifa huo na Lourenco, mrithi aliyeteuliwa na babake.

Nduguye Jose Filomeno Dos Santos anakabiliwa na kesi ya ufisadi nchini humo, huku upande wa mashtaka unasema kwamba yeye na wenzake walisaidia kutoa nje ya taifa hilo fedha kiasi cha dola milioni 500. **BBC**



Maelfu ya watu wakiwa eneo la bandarini Kaskazini mwa mji wa Sydney, Australia wakifurahia mwaka mpya 2020. Mbele yao kuna ukungu wa moshi unaotokana na moto unaoteketeza misitu na nyumba za wakazi wa eneo hilo. **PICHA: AP**

## Rais Trump amsihi Kim aheshimu makubaliano

**NEW YORK,** Marekani

BAADA ya kiongozi wa Korea Kaskazini kutishia nchi yake kujiondoa kwenye marufuku ya majaribio ya silaha kali, Rais Donald Trump wa Marekani amesema bado anaamini kuwa Kim Jong Un ni mtu anayeheshimu ahadi zake.

Rais Trump, ametumia salamu zake za Mwaka Mpya akiwa kwenye klabu yake ya Mar-a-Lago mjini Florida, kuzungumzia imani na wasiwasi wake kwa kiongozi wa Korea Kaskazini, saa kadhaa baada ya Kim kutangaza rasmi kuwa nchi yake haitajifunga tena na marufuku iliyojiwekea yenyewe ya kutofanya majaribio ya silaha za masafa marefu za nyuklia.

"Kiongozi wa Korea Kaskazini alisaini makubaliano kuhusu kuindoa nchi yake kwenye mpango wa nyuklia na naamini ni mtu mwenye kuheshimu kauli yake," alisema Trump mbele ya waandishi wa habari.

Aliongeza kwamba "Kim alisaini makubaliano hayo nchini Singapore."

Katika hotuba yake mbele ya mkutano mkuu wa chama tawala cha wafanyakazi, Kim alisema kwamba nchi yake inapanga kuendeleza mpango wake wa nyuklia, kuanzisha kile alichokiita. **DW**

## Vumbi Vita ya Pili ya Dunia kuzivuruga Marekani, Urusi

**MOSCOW,** Urusi

MGOGORO kati ya Urusi na mataifa ya Ulaya kuhusu kilichosababisha kutokea kwa vita ya pili ya dunia, umeendelea, huku ofisa mmoja mwandamizi wa Urusi akimshutumu Balozi wa Marekani nchini Poland.

Spika wa Bunge la Urusi, Vyacheslav Volodin, alikaripia ujumbe wa twitter uliochapishwa na Balozi Georgette Mosbacher, akisema ulikuwa ukiwatusi Warusi na Wamarekani.

Siku ya Jumatatu balozi huyo alituma ujumbe wa twitter uliosema "Kwa mpendwa Putin, Hitler na Stalin walishirikiana kuanzisha Vita vya Pili vya Dunia. Lakini Rais Putin anasema kwamba Poland na washirika wake wanapotosha historia."

Desemba 19 mwaka jana, Rais wa Urusi alisema ni makosa na haitokubalika kumlaumu kiongozi wa Nazi Adolf Hitler, na kiongozi wa Usovieti Joseph Stalin, kwa kuzuka kwa vita hivyo.

Putin alisema kwamba alikuwa ameomba stakhabadhi za Sovieti ili kuweza kuandika kitabu kuhusu suala hilo la uvamizi wa Nazi nchini Poland tarehe mosi Septemba na katika maoni yake ili kuweka kila kitu wazi.

Aidha, alihoji kwamba mataifa ya magharibi na Poland yaliunga mkono uchokozi wa Hitler, kwa kumruhusu kunyakua Czechoslavakia mwaka 1938.

Uvamizi wa Nazi nchini Poland ulijiri wiki moja baada ya Waziri wa Masuala ya Kigeni wa Hitler, Jachim von Ribbennstrop, na Waziri wa Masuala ya Kigeni wa Sovieti, Vyacheslav Molotov, kutia saini azimio la kusitisha uchokozi Agosti 23, mwaka 1939 ambalo liliishangaza dunia.

Kifungu cha siri katika makubaliano hayo, kilinyakua mashariki mwa Ulaya ndani ya Nazi na ushawishi wa Usovieti na hivyo kuwaruhusu madikteta hao wawili kunyakua na kuiharibu Poland.

Poland ilikuwa mwathiriwa wa madikteta hao wawili.

Lakini Volodin, ambaye ni mwandani wa karibu alisema kwamba idara ya masuala ya kigeni nchini Marekani inafaa kuhakikisha kuwa balozi kama Mosbacher alikuwa na habari za kutosha kuhusu historia ya taifa kabla ya yeye kutumwa kazi katika taifa hilo.

Bwana Putin amefufua ishara za kivita za Sovieti pamoja na picha za Stalin ambazo zinatumika sana Urusi kwa sasa. Mwaka 2020, maadhimisho ya 75 ya washirika wake kuhusu ushindi dhidi ya Nazi ya Ujerumani yataadhimishwa.

Zaidi ya raia milioni 20 wa Usovieti walifariki katika kile Urusi inasema ni vita vya kizalendo baada ya Nazi kuvamia USSR 1941.

Babake Putin alihudumu katika kikosi cha ujasusi cha Stalin na alijeruhiwa vibaya katika vita hivyo 1942. **BBC**

# Mbaroni na shehena ya samaki wachanga

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Iringa mkoani imekamata wafanyabiashara wanne wakubwa kwa tuhuma za kushirikiana na wavuvi haramu wakiwa na mzigo wa samaki wachanga wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 50.

Halmashauri hiyo kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo iliwakamata watu hao wakiwa na marobota 19 ya samaki wachanga ambao walikatazwa kisheria.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Richard Kasesela, alisema samaki wachanga wamekuwa wakivuliwa kwenye Bwawa la Mtera, hali ambayo amesema inahatarisha vizazi vya samaki kwa siku za usoni.

Alisema watu hao walikamatwa eneo la Igingilanyi katika Tarafa ya Isimani wakiwa na marobota ya samaki kwenye lori aina ya Fuso wakielekea Newala mkoani Mtwara kutoka Bwawa la Mtera.

Kasesela alisema walifanya doria katika Bwawa la Mtera na kufanikiwa kuwakamata kinamama wanne wakiwa na samaki hao wachanga marobota 19.

Alisema watuhumiwa hao baada ya uchunguzi kukamilika watafikisha mahakamani na kwamba samaki hao wametaifishwa na kugawia katika taasisi mbalimbali zikiwamo magereza, hospitali na shule.

"Watu wote waliokamatwa na samaki wachanga watapigwa faini na hatimaye kufikishwa mahakamani ili kutokomeza uvuvi harama katika Bwawa la Mtera," alisisitiza.

Kadhalika, Kasesela alisema kuwa lori lililobeba samaki hao nalo litataifishwa.

Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri hiyo, Mathew Sanga, alisema ofisi yake kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kupambana na uvuvi haramu kwenye bwawa hilo.

Alisema wilaya hiyo imejipanga kupambana na tatizo la uvuvi haramu mahali popte ndani na nje ya maji ili kutokomeza uvuvi haramu katika Bwana la Mtera lenye ukubwa wa kilomita za mraba 660.

Sanga pia aliwataka wavuvi wote katika bwawa hilo kuhakikisha wanatumia nyavu zinazokubalika kisheria, na kuwaasa wafanyabiashara wa samaki kutouuza samaki wachanga chini ya ukubwa wa nchi tatu, na kuongeza kwa kufanya hivyo wanaharibu vizazi vya samaki.



Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Mtwara, Locadius Kambale, aliyenyoosha mikono akitoa maelekezo mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, kufuatia kubomoka kwa daraja la Mto Mkoo lililopo katika kijiji cha Mkumbululu wilayani Masasi, ambako alifika kuangalia athari hizo jana. **PICHA HAMISI NASIRI**

# Askari ang'atwa na nyoka, afariki dunia kwa kuchelewa hospitali

**Na Stevie Chindiye,** NAMTUMBO

ASKARI msaidizi wa Idara ya Wanyamapori (VGS) katika kijiji cha Kitanda wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma, Halfani Mwale, ameng'atwa na nyoka na kufariki dunia muda mfupi baada ya tukio hilo.

Taarifa zinaeleza kuwa tukio hilo lilitokea Jumapili ambapo marehemu na askari wenzake walikuwa doria katika Pori la Wanyamapori la Jumuiya ya Mbarang'andu linalomilikiwa na vijiji kumi vya Wilaya ya Namtumbo.

Mtendaji wa Kijiji cha Kitanda, Ayubu Muhuwa, alisema askari huyo alikutwa na mauti baada ya kukimbizwa Kituo cha Afya Namtumbo na alipofikishwa kituoni hali haikuwa nzuri na kutakiwa kumpeleka Hospitali ya Rufani ya Mkoa Ruvuma, lakini kabla ya kufika hospitali alifariki dunia.

Askari mwenzake, Rashidi Maramae, alidai amefariki dunia kutokana na kuchelewa kupata huduma ya matibabu kwani eneo alilong'atwa na nyoka haifiki pikipiki wala gari, hali iliyowapelekea kumpatia huduma ya kwanza kwa kumfunga kamba na kumbeba kwenye machela mwendo wa saa nne kwa haraka na kufika eneo linalowezekana kupata usafiri.

Maramae alisema baada ya kufika eneo linalopitika kwa gari walipiga simu kwenye uongozi wa Jumuiya na kutumwa gari ya kumbeba marehemu, lakini muda uliotumika toka marehemu alipong'atwa na nyoka saa nane mchana, gari lilichelewa hadi saa 1 jioni, hivyo kuchelewa kumfikisha hospitali.

## Magufuli: Nitaendelea kutumbua

INATOKA UK. 2

Victoria.

Rais alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Chato, kufuatilia ukusanyaji wa mapato katika soko hilo na kuchukua hatua za kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato itakayobainika ili Halmashauri ya Wilaya ya Chato ipate fedha zitakazosaidia kutatua kero za wananchi ikiwamo kuboresha mazingira ya soko hilo na ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Nyabugera ambayo alichangia Sh. milioni 5.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Rais amemwagiza Mkurugenzi wa Chato Mwaiteleke kutangaza zabuni ya ujenzi wa barabara ya Kasenda hadi Muganza yenye urefu wa kilometa 2.2, ili ijengwe kwa kiwango cha lami kama alivyoahidi, na kwamba serikali itatoa fedha za ujenzi wa barabara hiyo.

Wakati huo huo, Rais Magufuli alipokea salamu za heri ya Mwaka Mpya wa 2020 kutoka kwa wananchi, viongozi mbalimbali wakiwamo marais wastaafu, maaskofu na masheikh ambao wamempongeza kwa kazi nzuri ya kuongoza nchi kwa mafanikio makubwa na wamemwelezea matarajio yao ya kufanikiwa zaidi katika mwaka ujao.

"Rais wangu, Dk. Magufuli, Bwana Yesu Asifiwe. Ninakupa hongera sana kwa wajibu mzito ulionao. Kwa neema ya Mungu tumejaaliwa kufikia siku ya mwisho kwa mwaka huu wa 2019. Mimi nakupongeza kwa jitihada zako nyingi za kuleta maendeleo kwa nchi yetu. Ninakuombea na kukutakia Mwaka Mpya 2020 wa heri na mafanikio makubwa. Uso wa Bwana uende nawe popote utakapokuwa," alisema Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Frederick Shoo.

Kabla ya kuondoka katika Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo, Rais Magufuli alimshukuru Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Dk. Allan Kijazi, maofisa na askari wote wa hifadhi hiyo kwa mapokezi mazuri na juhudi kubwa zilizowezesha hifadhi hiyo kuvutia.

Aidha, aliwahakikishia kuwa pamoja na kutoa Sh. bilioni 2 za ujenzi wa kivuko cha kwenda hifadhi ya Kisiwa cha Rubondo, serikali itatoa Sh. milioni 200 za kuboresha barabara za hifadhi hiyo.

**DK. SHEIN ATUMA SALAMU**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, jana, aliwapongeza wananchi wa Zanzibar kwa kushirikiana na serikali zao zote mbili katika kuidumisha amani na utulivu kwa kipindi chote cha mwaka 2019.

Katika hotuba yake kwa taifa, alisema wananchi wameonyesha mapenzi makubwa, umoja na mshikamano baina yao na miongoni mwa wageni wanaokuja kutembea nchini.

Alisema amani, utulivu na umoja vimewezesha kuitekeleza mipango ya maendeleo kwa mafanikio makubwa ambapo umepelekea uchumi wa Zanzibar kuendelea kukua kwa asilimia 7.1 kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 6.8 kwa mwaka 2016.

## HABARI KITAIFA

# Wanavijiji Katavi wapata fursa mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, amezindua huduma ya mawasiliano vijijini kwenye Wilaya ya Mlele mkoani Katavi.

Mhandisi Kamwelwe alifanya uzinduzi huo jana kwenye kijiji cha Kanoge kilichopo Kata ya Utende wilayani Mlele mkoani Katavi, kwa kuzindua mnara wa mawasiliano uliojengwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa kushirikiana na Kampuni ya Simu ya Vodacom Tanzania ambapo ujenzi wake umegharimu Sh. milioni 300.

Alisema zimekuwapo kampuni za simu ila hazikutaka kwenda vijijini bali kwenye maeneo yenye fedha, lakini serikali imeanzisha Mfuko wa UCSAF na inatoa ruzuku kwa kampuni za simu ambazo nazo zinachangia kujenga minara vijijini ili kupeleka mawasiliano maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara

"Na kwa vile leseni natoa mimi, sasa nazielekeza kampuni za simu nenda kijijini au mahali fulani ambapo hamna mawasiliano na hakuna mvuto wa kibiashara na wanakwenda ili kufikisha mawasiliano kwa wananchi," alieleza Mhandisi Kamwelwe.

Aliiagiza UCSAF kupeleka mawasiliano ya data badala ya sauti tu kwa kuwa bila data wanafunzi hawataweza kusoma shuleni, na kwamba wananchi pia wanataka data.

"Ndio maana awali nilileta kompyuta 50 kwa shule za msingi na sekondari, sasa naleta umeme ili watoto waanze kucheza na kompyuta kwa kuwa sasa hivi Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni uchumi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya UCSAF, Dk. Joseph kilongola, alisema kwa kutumia Mfuko wa UCSAF wanahakikisha mawasiliano yanawafikia wananchi kwa kuwa kampuni za simu pekee haziko tayari kupeleka mawasiliano maeneo ya vijijini.

Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Justina Mashiba, amesema kuwa hadi sasa usikivu wa mawasiliano umefikia kiwango cha asilimia 94 ukilinganisha na asilimia 45 mwaka 2009 wakati UCSAF inaanzishwa.

Mashiba ameongeza kuwa UCSAF imetangaza zabuni ya kujenga minara ya mawasiliano kwenye kata 252 nchini ambapo utekelezaji wa zabuni utakapokamilika usikivu wa mawasiliano utaongezeka na kufikia kiwango cha asilimia 96.

Alisema kuwa UCSAF itaendelea kuhakikisha kuwa shule za umma zinapata kompyuta kwa kuwa wanafahamu kuwa shule zetu zina ukosefu wa vifaa vya Tehama ili tuwe na Watanzania ambao wanaweza kutumia vifaa vya Tehama.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Rachel Kasanda, aliwaambia wananchi kuwa hakuna mtoto atakayebaki bila kwenda sekondari baada ya wiki mbili kupita baada ya shule kufunguliwa tarehe 6 Januari mwaka 2020.

# Walia kutolipwa fidia mashamba kuchukuliwa

**Na Hamisi Nasiri,** LINDI

WAKAZI wa Kijiji cha Mningulo, Kata ya Mnolela mkoani Lindi ambao sehemu kubwa katika kuendesha maisha yao wanaotegemea shughuli za kilimo, wamelalamikia kukosa kazi za kufanya kwa madai kuwa wameporwa mashamba yao yenye mazao na kupewa mwekezaji bila ya kulipwa fidia.

Juma Bakari, alisema baadhi ya wakulima wa kijiji hicho kwa sasa hawafanyi kazi zozote za kilimo kwa sababu ya mashamba yao kunyang'anywa na mwekezaji bila kulipwa chochote kama taratibu zinavyotaka.

Alisema hali hiyo imezua mgogoro kati ya Manispaa ya Lindi na wakazi wa kijiji hicho na mwekezaji aliyepewa ardhi yao.

Bakari alisema mgogoro umetokana na mpango wa Manispaa ya Lindi kuwa na mradi wa mashamba kwenye maeneo yao, lakini baada ya kuishiwa maeneo wakaingia eneo la Lindi Vijijini na kumpa mwekezaji huyo bila ya kuwashirikisha wananchi ambao ni ndio wamiliki wa mashamba hayo.

"Tatizo hapa ni kitendo cha manispaa kugawa eneo la ardhi bila kushirikisha wananchi wenye mashamba tena kwenye eneo la wilaya nyingine," alisema Bakari.

Naye Rukia Athumani, alisema mgogoro huyo umewaathiri kwani miongoni mwa maeneo yaliyochukuliwa ni pamoja na mashamba hekari 40 ya kikundi cha wanawake cha Upendo ambacho kimepewa mkopo wa shilingi milioni tano dhamana yake shamba lao ambalo limechukuliwa na mwekezaji huyo.

"Tunaiomba serikali kuchukua hatua kutatua mgogoro huu unatufanya tushindwe kufanya shughuli zetu za maendeleo kwani tumechukua mikopo kwa dhamana ya mashamba yetu," alisema Rukia.

Marry Clopaus, mkazi wa kijiji hicho alisema tunasikitishwa na kitendo cha uongozi wa Manispaa ya Lindi kuchukua uamuzi wa kugawa mashamba ya wananchi bila kuwashirikisha tena wakulima wadogo wanaotaabika kulima kwa ajili ya chakula cha kujikimu.

Rashidi Athumani alisema wananchi wana imani na serikali ya wanyonge ya Rais John Magufuli ambayo inasisitiza kutenga maeneo kwa ajili ya wakulima wadogo na inasisitiza watu kufanya kazi za uzalishaji mali kwa amani na utulivu.

Atha Swai, ni mwekezaji aliyepewa eneo hilo na serikali, alisema Manispaa ya Lindi ilitangaza kugawa mashamba kwa wakulima wadogo wakati na wakubwa baada ya tangazo hilo aliomba hekari 350 na alipewaa baada ya kufuata taratibu zote za kisheria zilizokawa zimewekwa.

Swai alisema baada ya kupewa maeneo hayo alianza kuyafanyia kazi ikiwamo kupanda mikorosho na mimea mingine ndipo wananchi walipokuja na kuvamia na kufanya uharibifu kwa madai ya kuwa shamba hayo ni mali yao.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, amekiri kuwapo kwa mgogoro, na kueleza kuwa ofisi yake imepokea migogoro zaidi ya 300 na mingi imeisha bado michache ukiwemo wa wanakijiji cha Mningula na mwekezaji huyo.

Alisema wameunda kamati ya pande mbili za mgogoro tayari wamefanya kikao kimoja, lakini kilishindwa kufikia muafaka.



Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo (katikati), akizungumza baada ya kumkabidhi mbegu za michikichi aina ya tenela Mkuu wa Gereza la Kwitanga lililopo Kigoma Vijijini, kwa ajili ya kupanda kwenye shamba lao la ekari 6,000. Kushoto ni Mkuu wa gereza hilo, Dominic Kazimili. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Muhongo ajitosa sakata madarasa

**Na Sabato Kasika**

MBUNGE wa Musoma Vijijini (CCM), Prof. Sospeter Muhongo, amejitosa kwenye sakata la upungufu wa madarasa katika shule za sekondari jimboni mwake, kwa kuanzisha harambee ya kuchangia ujenzi vyumba vipya.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kutoka jimboni, alisema, lengo la kuchukua hatua hiyo ni kutaka kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa kidato cha kwanza mwaka huu, wanapata nafasi.

Prof. Muhongo alisema, katika kufanikisha mkakati huo, kuanzia leo Januari 2, saa nne asubuhi, atatembelea sekondari mpya ya Busambara, ambayo itaanza kuchukua wanafunzi mwaka huu.

"Baadaye saa nane mchana nitakuwa Shule ya Sekondari Bugwema, ambayo ina upungufu wa vyumba vitatu, kisha Ijumaa saa nne asubuhi atakuwa katika sekondari mpya Dan Mapigano Memorial," Prof. Muhongo alisema.

Alisema, Januari 6 saa nne asubuhi nitakuwa Sekondari ya Nyakatende, ambayo ina upungufu wa vyumba viwili na kisha saa nane mchana atakuwa Sekondari ya Rusoli yenye upungufu wa chumba kimoja.

"Sekondari nyingine zenye upungufu wa vyumba vya madarasa ni Kasoma vinahitajika vyumba vitatu na Nyanja chumba kimoja, huko kote tutafanya harambee ya kuchangia ujenzi," alisema.

Alisema, hiyo ni njia mojawapo ya kusaidiana na serikali kwa ajili ya kumaliza tatizo hilo kwa kushirikiana na wananchi ili wanafunzi wote waanze masomo mapema iwezekanavyo Januari hii.

## HABARI MICHEZO




# CHELSEA YAFIKIRIA KUMSAJILI DEMBELE

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Lyon, Moussa Dembele ni mmoja wa washambuliaji wanaofikiriwa kusajiliwa na Chelsea wakati wa dirisha hili la Januari.

Dembele amefunga mabao 25 tangu alipohamia kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, akitokea Celtic kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 20 miezi 18 iliyopita.

Olivier Giroud na Michy Batshuayi wanaonekana wazi wanaondoka Chelsea wakati wa dirisha dogo la usajili na Frank Lampard amekuwa akimuwania Dembele kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa Sky Sports News, Lampard anaona mfanano kati ya Dembele na mshambuliaji wa zamani wa Chelsea, Didier Drogba.

Dembele alifurahia mafanikio akiwa na Celtic baada ya kujiunga akitokea Fulham mwaka 2016 chini ya kocha wa zamani Brendan Rodgers.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, alishinda mara mbili taji la Ligi Kuu ya Scotland, mataji mawili ya Ligi pale kwenye Uwanja wa Parkhead kabla ya kuhamia Lyon Agosti mwaka 2018.

Amefunga mabao 10 katika mechi 25 alizoichezea Lyon hadi sasa msimu huu.

# Solskjaer: 2020 mwaka wa Utd

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer anaamini 2020 unaweza kuwa mwaka wenyewe mafanikio binafsi wakati akijaribu kutwaa taji lake la kwanza kama kocha wa Manchester United.

United ilimaliza mwaka 2019 ikiwa nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu, na ushindi wao wa 2-0 dhidi ya Burnley ukiwaacha wakipitwa pointi nne kwenye nne bora.

Ushindi wa pale kwenye Uwanja wa Turf Moor ulimaliza nyakati mbaya kwa 'Mashetani Wekundu' hao, ambapo waliteua makocha wanne wa kudumu, lakini walishindwa kutwaa taji la nyumbani tangu kuondoka kwa Alex Ferguson aliyestaafu mwaka 2013.

Kikosi hicho cha Solskjaer hakijawa kwenye kiwango bora mfululizo msimu huu, lakini wameshinda mechi zake sita zilizopita kati ya nane kwenye mashindano yote kabla ya mwaka mpya, huku wakiwa na nafasi ya kushinda Kombe la EFL, FA na lile la Europa.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa United anafikiri timu yake yenye vijana wengi inakaribia kuwa ile anayoitaka kwa siku chache zijazo.

"Mwaka 2020 utanifanya kuwa bora zaidi kwangu binafsi," alisema kuelekea kwenye mchezo wake wa jana dhidi ya Arsenal.

"Nafikiri tupo kwenye njia sahihi. Tupo kwenye wakati wa mpito, tumeona klabu nyingine zikifanya hivyo na kuwa imara baada ya miaka kadhaa. Tutakuwa imara kwenye muongo huu kwa uhakika kabisa. Hiyo ndio asili ya klabu hii.

"Tunaimarika, na nafikiri tunaweza kuona mambo mengi zaidi yakija na tunataka kuonyesha utambulisho wetu, tuko timu imara."







# *Rooney kuanza kazi Derby County leo*

**LONDON,** England

WAYNE Rooney leo, Alhamisi anatarajiwa kuanza kuichezea timu yake mpya ya Derby County watakapokutana na Barnsley kwenye mchezi wa Ligi Daraja la Kwanza.

Mfungaji huyo wa wakati wote wa England, alisaini mkataba wa miezi 18 kama kocha mchezaji na timu hiyo Agosti mwaka jana, lakini hakuruhusiwa kuichezea hadi Januari Mosi.

Kutokana na kiwango duni cha Derby pengine kilimfanya kocha, Phillip Cocu kutarajiwa kumuanzisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34.

"Yupo fiti, anaweza kuisaidia timu hii kwa kipindi chote atakachokuwapo hapa," alisema Cocu akiwaambia waandishi wa habari.

"Anaweza asiwe fiti sana, lakini jambo la muhimu ni kwamba anaweza kuwa kwenye ubora wake na kuisaidia timu.

"Kama mchezaji ana ubora wake na ana uwezo na uzoefu kama Rooney unakuwa naye kwenye timu, basi ni wazi kwamba anaweza kuisaidia kwa namna nyingi."

## HABARI MICHEZO

# Guardiola: Tukijituma na kusali tutaifikia Liver

**LIVERPOOL,** England

PEP Guardiola amesema Manchester City lazima “ijitume kwa nguvu, kucheza vizuri na kusali” kumaliza pengo na Liverpool, lakini anajiamini kikosi chake kipo fiti na kinaweza kushindana kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu.

City imeshinda taji la Ligi Kuu miaka miwili iliyopita, bado imepitwa pointi 14 na vinara Liverpool, ambao wana mchezo mmoja mkononi wakati huu ikiingia mwaka 2020.

Wakati City ikionekana kuwa haikuwa sawa kwenye mechi zilizopita, Guardiola anaona kwamba kuumia kwa Aymeric Laporte na Leroy Sane kumechangia.

Alipoulizwa kama timu yake lazima ijiimarishe kuikamata Liverpool, kocha huyo wa City aliwaambia waandishi wa habari: “Wajitume, wacheze vizuri na kusali.

“Kwa kikosi chetu, ndio, (City inaweza kushindana). Kuna vitu ambavyo havipo kwenye uwezo wetu. Tunaweza kufanya tunachoweza.

“Lakini kuna vitu hatuwezi kwa uwezo wetu, kama timu ya kuvutia kama Liverpool ilivyofanya hadi sasa. Kama kila mmoja akiwa fiti, tunaweza.”

Guardiola alikataa kukubali kwamba kushindwa kusajili katika dirisha la usajili lililopita kumechangia matatizo.

“Hapana, nafikiri timu inavutia. Naipenda,” alisema. “Tulikuwa na matatizo kwa majeruhi, vitu vitatu vilitokea na Liverpool wako vizuri.”





# HODGSON ASEMA ZAHA HAUZWI NG’O

**LONDON,** England

ROY Hodgson anajiaminia hakuna mtu pale Crystal Palace anayefikiria kumuuza winga Wilfried Zaha wakati huu wa dirisha la Januari, lakini anatambua ofa “nono” inaweza kukubaliwa.

Zaha alikuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na Everton na Arsenal kwenye madirisha ya usajili yaliyopita, huku Hodgson akijua kwamba mchezaji huyo hakuwa na furaha kwa usajili wake kutokamilika.

Palace imeripotiwa kwamba imepanga kiasi cha pauni milioni 100 kwa ajili ya kumuuza mchezaji huyo.

Hata hivyo, baada ya Chelsea kufutiwa adhabu yake ya kutosajili inamaanisha kwamba wanaweza kufanya usajili Januari hii na Zaha anaonekana kuwa kwenye chaguo lao.

Mapema Desemba mwaka jana, wakala Federico Pastorello aliiambia Sky Sports News kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast “anastahili changamoto mpya na klabu kubwa”.

Hata hivyo, Hodgson amesema: “Wilfried hauzwi. Sihitaji uhakika.

“Hatutajaribu kumuuza Wilfried Zaha, tunajaribu kumbakisha Wilfried Zaha.

“Nina uhakika hakuna mtu klabuni kwetu ambaye atajaribu kumuuza Wilfried Zaha.

“Lakini bila shaka, huwezi kujua ofa gani tutapata kama klabu, na kama tutakuwa na ofa iliyonona bodi ya wakurugenzi wanaweza kuifikiria.”

# *Arteta hashangazwi uwezo wa Ozil*

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesisitiza hakushangazwa na uwezo wa Mesut Ozil aliouonyesha dhidi ya Chelsea, akiwa amevutiwa na kiungo huyo mchezeshaji wa Arsenal “kwa kiwango chake kwenye mazoezi”.

Ozil amekuwa akishutumiwa kwa kutokuwa kwenye kiwango chake pale Arsenal na mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa ameshindwa kuwa kwenye nafasi yake katika kikosi cha kwanza.


Lakini licha ya ‘Washikabunduki’ hao kufungwa 2-1 na Chelsea pale kwenye Uwanja wa Emirates Jumapili, Ozil alikuwa kwenye kiwango bora katika mchezo wa kwanza wa kocha Arteta kucheza nyumbani.

Malengo ya Arteta sasa ni kujenga timu bora kwani kiwango cha Ozil peke yake hakiwezi kuifanya timu kushinda.

“Ndio maana natumaini, anaweza kuendelea kuwa kwenye kiwango bora kwa siku tatu au nne,” alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari kabla ya jana kucheza na Manchester United.

“Ana imarika zaidi, na yupo tayari. Ndio maana naweza kuwaambia kwa kile ninachokiona kwenye mazoezi.

“Sikushangazwa. Najua uwezo wake, najua ni aina gani ya mchezaji niliyenae hapa. Muundo unasaidia kumfanya kuwa na timu bora kabisa.”



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SUAREZ SASA AISIKILIZIA BARCA AKISAKA REKODI

## Nafasi ya pili ni changamoto ngumu zaidi, lakini kumfikia Kubala, hilo...

**BARCELONA,** Hispania

LUIS Suarez anaamini yeye na Barcelona watafikia makubaliano kuhusu mkataba mpya wakati huu akitolea macho kuweka rekodi ya kuwa mchezaji wa pili katika orodha ya wachezaji wa wakati wote wanaoongoza kwa mabao klabuni hapo.

**Suarez alijiunga na Barca akitokea Liverpool mwaka 2014 na ameendelea kufurahia wakati wake mzuri hapo Camp Nou, kwa misimu yote kwa suala la mafanikio binafsi na ya klabu.**

Katika kipindi hicho, amefunga mabao 190 na kushinda kila taji lililowezekana, ikiwamo La Liga, Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'] na la Ligi ya Mabingwa Ulaya walipotwaa mataji matatu msimu wa 2014-15.

Suarez, 32, sasa ameonyesha dalili za kuporomoka ukilinganisha na mwaka jana ama zaidi, na taarifa za vyombo vya habari hivi karibuni zilidai kuwa Barca inataka kuzipa pengo lake kwa kumsajili straika wa Inter, Lautaro Martinez, licha ya nyota huyo wa zamani wa Ajax kujivunia kufikisha mabao 10 katokana na mechi 16 za LaLiga alizocheza msimu huu.

Lakini nyota huyo wa kimataifa wa Uruguay anaonekana kujiandaa kwa miaka michache zaidi katika klabu hiyo, kutokana na kuonekana kutarajia kukubali kuongeza mkataba wake wa sasa, ambao unamalizika mwaka ujao, 2021.

"Ni mwenye furaha sana katika klabu hii," aliliambia Sport. "Mara zote nimekuwa nikijioa kwa kila kitu. Takwimu na namba zinathibitisha hilo.

"Nadhani niko kwenye kazi hiyo na itakapofikia mazungumzo [ya mkataba], tutafika hitimisho nzuri. "

Suarez kwa mabao yake 190, inamaana amebakisha manne tu kumfikia mkongwe wa Barca, Laszlo Kubala - lakini malengo makubwa aliyonayo, macho yake yapo kwa Cesar Rodriguez.

Cesar alitupia mabao 232 wakati akiichezea Barca kuanzia mwaka 1942 hadi 1955 na ndiye pekee anayeshika nafasi ya pili nyuma ya kinara Lionel Messi kwenye orodha ya wafungaji wa wakati wote hapo Barca, ingawa Suarez amekiri kumkamata mchezaji mwenza huyo ambaye ana mabao 618 - haitawezekana.

"Mara zote nimekuwa nikisema kuwa changamoto binafsi zinapaswa kuwekwa kando, lakini kwa suala hili, wakati kuna idadi ndogo ya kumfikia ama kumpita mchezaji wa kihistoria kama Kubala na kufika pale [tatu bora], unajisikia fahari sana," aliendelea.

"Nafasi ya pili ni wazi ni changamoto ngumu zaidi, lakini hilo halitutoe nje ya mwelekeo.

"Mara zote unajaribu, lakini litafanywa kwa wakati. Nafasi ya kwanza haiwezekani, lakini inafurahisha sana kufikia idadi ya Cesar. "

## ZISIKUPITE

### INTER KWA AUBAMEYANG

INTER Milan imejiunga katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, 30. ***(Mirror)***

### RONALDO AINOGEA JUVE

JUVENTUS inapanga kuongeza mkataba na mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo, ambao utamfanya kukipiga hapo Turin hadi 2023, wakati atakapofikisha miaka 38. ***(Corriere dello Sport, via Mail)***

### DEMBELE AWINDWA CHELSEA

CHELSEA inajipanga kuifuata saini ya mshambuliaji wa Lyon, Mfaransa Moussa Dembele, 23. ***(Sky Sports)***

### XHAKA ANUKIA BERLIN

HERTHA Berlin imekubali kumsajili kwa mkopo kiungo wa Arsenal na Uswisi, Granit Xhaka, 27, na ikitazama uwezekano wa kumsajili jumla majira ya joto. ***(Independent)***

### MATIC NJIAPANDA UNITED

KIUNGO wa Manchester United na Serbia, Nemanja Matic, 31, amesema "ukweli hajui" kama ataongeza mkataba wake hapo Old Trafford. ***(Telegraf - in Serbian)***

### HODGSON AMBANIA ZAHA

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson amesisitiza mshambuliaji Muivory Coast Wilfried Zaha, hauzwi lakini akakiri klabu hiyo itapaswa kuzingatia "ofa nono" kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Guardian)***

### INTER KUJITOSA KWA EMERSON

INTER Milan inataka kutoa ofa ya pauni milioni 25 kwa beki wa kushoto wa Chelsea, Mtaliano Emerson Palmieri, 25. ***(Independent)***

### CHELSEA, CITY KWA CHILWELL

CHELSEA na Manchester City zitaenda uso kwa uso kuisaka saini ya beki wa Leicester na England, Ben Chilwell, 23. ***(The i)***

### CALVERT-LEWIN KUITOSA UTD

MSHAMBULIAJI wa England U-21, Dominic Calvert-Lewin, 22, atatia saini mkataba wa miaka mitano kuichezea Everton licha ya Manchester United kuvutiwa naye. ***(Telegraph)***

### BRUCE ATAKA WA3 NEWCASTLE

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce anataka kusajili wachezaji watatu katika dirisha hili la usajili la Januari. ***(Telegraph)***

### NORWICH YATIBUA MAN CITY

MANCHESTER City imevunja mkataba wa mkopo wa winga wake, Patrick Roberts, 22, katika klabu ya Norwich na badala yake ikampeleka Middlesbrough kutokana na kukosa nafasi ya kucheza katika timu hiyo ya awali. ***(Mail)***

### SHEFFIELD KUMFUATA BENITO

SHEFFIELD United inafikiria kumfuata beki wa Bordeaux na Uswisi, Loris Benito, 27. ***(Football Insider)***

## HABARI MICHEZO

# YANGA YAWAIBUA WADAU IKILAMBA KICHWA JEZI FEKI

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya sakata la wachezaji wa Yanga kuvishwa jezi feki katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Biashara United Jumatatu wiki hii, 'kula kichwa' cha Kaimu Meneja wa timu hiyo, Dismas Ten baada ya uongozi kuamua kumsimamisha kazi, wadau wa soka wamedai suala hilo linawahusisha viongozi wengi ndani ya klabu hiyo.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Taifa, ambayo Yanga iliibuka na ushinda wa bao 1-0, wachezaji wa Yanga walivaa jezi feki ambazo si zile zinazotengenezwa na mdhamini wao, GSM kwa mujibu wa mkataba, jambo ambalo uongozi wa klabu hiyo umeeleza kumsimamisha kazi Dismas ili kupisha uchunguzi wa kina wa suala hilo, huku ukiahidi kuchukua hatua zaidi kwa kila atakayebainika.

**Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Klabu ya Yanga jana, mbali na kumsimamisha Dismas, ilieleza kuwa uongozi utamtangaza meneja mpya atakayechukua nafasi iliyoachwa wazi.**

"Tunaomba radhi kwa mdhamini wetu kwa kitendo kilichofanywa na Meneja wetu na kuhakikisha hakitajirudia tena," ilieleza taarifa hiyo.

Hivi karibuni uongozi wa Yanga kwa kushirikiana na mdhamini wao wa jezi pamoja na Jeshi la Polisi uliendesha kampeni kabambe ya kusaka jezi feki kwa wafanyabiashara wa Kariakoo na kufanikiwa kuwatia wachache nguvuni, lakini kitendo cha wachezaji wao kuzivaa katika mechi hiyo kiliacha maswali magumu kwa wadau wa soka.

Karimal Hamdan, aliyejitambulisha kama shabiki wa Yanga, alisema: "Kumsimamisha Dismas Ten pekee, haiingii akilini, wapo wengi wanaohusika na suala hili ndani ya uongozi na wanaopaswa kuadhibiwa, hivyo isimfanye yeye kama mbuzi wa kafara tu."

George Michael, mdau mwingine wa soka kwa upande wake alisema: "Viongozi ndani ya klabu nyingi hapa nchini wao ndio chanzo cha jezi feki, na kuthibiti mtandao huo ni vigumu kwa kuwa wahusika wakuu wapo ndani ya uongozi, hivyo Yanga wajitazame wenyewe kwanza badala ya kumshughulikia mtu mmoja pekee."




Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Sharaf Shiboub, akimiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Ndanda FC ya Mtwara, Geofrey Joackim, wakati wa mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi na wenyeji hao kushinda 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba yafunguka kuuzwa straika

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kuhusishwa na kuwa mbioni kujiunga na timu moja ya Daraja la Kwanza katika usajili huu wa dirisha dogo unaotarajiwa kufungwa Januari 15, mwaka huu, hatimaye uongozi wa klabu ya Simba umefunguka kuhusu suala zima la mshambuliaji wao kinda, Rashid Juma, ambaye anagombewa na timu za Ligi Kuu.

Tangu kufunguliwa kwa usajili wa dirisha dogo Desemba 16, mwaka jana, Rashid amekuwa akihusishwa na kutolewa kwa mkopo katika klabu ya Majimaji, huku pia KMC, JKT Tanzania na Tanzania Prisons zikielezwa kuingia vitani kuisaka saini ya dogo huyo.

Na habari zimekuwa zikizagaa kuwa klabu ya Simba ipo katika mpango wa kumtoa Rashid kwa mkopo ili kwenda kupata nafasi ya kucheza zaidi kutokana na ufinyu wa namba katika kikosi chake na KMC ikitajwa kuwa katika nafasi nzuri ya kumnasa.

Hata hivyo, akizungumza na waandishi wa habari jana katika Hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam, Mtendaji Mkuu wa klabu ya Simba, Senzo Mbatha Mazingisa, alisema taarifa hizo si kweli na kwamba Rashid ni majeruhi na anaendelea na matibabu.

"Kuna tetesi kwamba Rashid Juma amesajiliwa na timu ya Daraja la Kwanza, si kweli. Rashid ni majeruhi na madaktari wa timu wanaendelea kumpatia matibabu," alisema.

Taarifa za Rashid kujiunga Majimaji ya Songea, kwa sasa zimefunika na kasi ya KMC kuwa katika hatua nzuri ya kuinasa saini ya kinda huyo ambaye kila akipata nafasi Simba, husaidia kuongeza kasi ya kushambulia.

Akizungumza na mwandishi wetu hivi karibuni, Rashid alisema bado hajapata timu ila wakati ukifika anaamini kila kitu kitakuwa sawa na klabu yake itamruhusu.

"Mimi bado ni mchezaji wa Simba kwa sasa na ninaendelea vizuri, kuhusu suala la kuondoka na kujiunga na klabu nyingine hilo ni jukumu la viongozi wangu, tusubiri tuone," alisema.

# *Kocha Ndanda: Simba hii ukifunguka unakula wiki*

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, Kocha Mkuu wa Ndanda FC, Meja mstaafu Abdul Mingange, ameshukuru timu yake kuepuka kipigo cha mbwa mwizi katika mchezo huo.

Katika mechi hiyo ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Taifa juzi, baada ya kuruhusu bao la mpira wa faulo lililozamishwa kimyani na Francis Kahata dakika ya 13, Ndanda ilicheza kwa kujilinda zaidi takriban dakika zote 77 zilizosalia, hivyo kuruhusu kushambuliwa zaidi na Simba ambayo ilimiliki mchezo huo kwa asilimia kubwa.

Mpango huo ulionekana kufaulu kwa Ndanda, kwani Simba ililazimika kusubiri hadi dakika tano kabla ya mchezo kumalizika kuweza kupata bao la pili lililozamishwa kimyani na mtokea benchi, Mkongomani Deo Kanda, hivyo kuzidi kujichimbia kileleni mwa ligi hiyo ikiwa na alama 34 baada ya kushuka dimbani mara 13 msimu huu.

Hata hivyo, akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo, Mingange alisema timu yake ililazimika kucheza kwa kujilinda zaidi ili kukwepa kupigwa mabao mengi kwa kuwa walifahamu ubora wa Simba hususan kwa timu inapocheza dhidi yao na kufunguka.

"Ukicheza na Simba halafu ukafunguka, unaweza kupigwa hata bao saba ['wiki'], hatukutaka ushindi bali lengo letu lilikuwa ni kupunguza kupigwa idadi kubwa ya mabao," alisema Mingange ambaye kabla ya mchezo huo alijigamba kuwa amefuata pointi tatu.

Mingange aliendelea kujitetea kuwa hiyo ilikuwa mechi yake ya pili kuiongoza Ndanda FC, tangu alipotwaa mikoba hiyo kutoka kwa Malale Hamsini iliyetimuliwa hivi karibuni kutokana na matokeo mabovu.

"Wewe ulitaka nifungwe mabao mengi? Ilikuwa lazima tucheze hivi kwa sababu kwanza ndiyo naijenga timu kwani hii ni mechi yangu ya pili baada ya mchezo wa kwanza kuiongoza kwenye Kombe la FA," alisema.

Matokeo hayo yanaifanya Ndanda kuendelea kubaki na alama zake nane baada ya kushuka dimbani mara 14 msimu huu, huku ikishika nafasi ya pili kutoka mkiani kwenye ligi hiyo inayojumuisha timu 20.

# Michezo

Alhamisi Januari 2, 2020

Nipashe





Suarez sasa aisikilizia Barca akisaka rekodi

HABARI UK.30

MTU KATI...



Beki wa Chelsea, Antonio Rudiger na kiungo mkabaji N'Golo Kante (kulia) wakimweka mtu kati straika wa Brighton, Neal Maupay wakati timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja AMEX jana. **PICHA: MTANDAO**

## Wasikie Tariq, Bocco J'mosi

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kucheza kwa dakika zote 90 kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu ya msimu huu kutokana kuwa nje akiuguza majeraha ya mguu, nahodha na mshambuliaji wa Simba, John Bocco, ameahidi timu yao kuendelea kupigania pointi tatu katika kila mchezo ukiwamo wa Jumamosi dhidi ya Yanga.

Kurejea kwa Bocco pia kulimfurahisha Kocha wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck baada ya kumshuhudia akionyesha jitihada kubwa wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ndanda FC kwenye Uwanja wa Taifa juzi.

Bocco, alisema: "Natambua itakuwa mechi ngumu dhidi ya Yanga, lakini tumejipanga kuendelea kuvuna pointi na naamini kwa maandalizi tunayoendelea kuyafanya tutafanikiwa kubeba pointi tatu."

Na kwa upande wake mshambuliaji mpya aliyetua Yanga katika dirisha dogo na kuanza kwa kuipa timu hiyo ushindi dhidi ya Biashara United Jumatatu wiki hii, Tariq Seif, alisema Simba ni timu kubwa na anaiheshimu, ila kama atapangwa atapambana ili kuendelea kuibeba timu yake.

"Naiheshimu Simba ni timu kubwa, ila kama nikipata nafasi ya kucheza, nitapambana kama (dhidi ya Biashara United) na ikiwezekana hata zaidi ili kuipa timu yangu ushindi, nashukuru mechi yangu ya kwanza nimepata nafasi na kuifungia bao muhimu," alisema Tariq aliyekuwa akicheza soka la kulipwa nchini Misri kabla ya kutua Yanga.

# Simba, Yanga waliamsha

**Na Mwandishi Wetu**

## Kuziona buku 7, Jonesia Rukyaa Pilato wa mechi, Jangwani wawekewa mil. 50/- mezani, Msimbazi ni moto...

WAKATI homa ya pambano la watani wa jadi ikizidi kupanda, Shirikisho la Soka nchini (TFF), limemtangaza Jonesia Rukyaa kutoka Kagera kuwa 'Pilato' [mwamuzi wa kati] wa mchezo huo, huku akisaidiwa na Sudi Lila pamoja na Hamisi Chang'walu wote kutoka Dar es Salaam.

**Katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Taifa Jumamosi majira ya saa 11:00 jioni, huku Simba ikiwa mwenyeji, TFF imetangaza Mwamuzi wa Akiba atakuwa Elly Sasii kutoka Dar es Salaam huku Kamishna wa Mchezo akiwa ni Khalid Bitebo (Mwanza) wakati Mtathimini Waamuzi akitangazwa atakuwa Sudi Abdi wa Arusha.**

Aidha, kwa mujibu wa taarifa hiyo ya TFF iliyotolewa jana, ilieleza kuwa viingilio vya mechi hiyo kwa mzunguko tiketi zitauzwa Sh. 7,000, huku VIP B na C zikiuzwa kwa Sh. 20,000 wakati zile za VIP A zikiuzwa kwa Sh. 30,000 tu.

Na kuelekea mchezo huo wa Jumamosi, licha ya juzi baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ndanda FC, Kocha wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck kugoma kuuzungumzia huku akidai ni mechi tofauti kabisa, uongozi wa Wekundu wa Msimbazi hao umejigamba kuibuka na ushindi.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, viongozi wa Simba kwanza uliwahamasisha mashabiki kujitokeza kwa wingi kununua tiketi za mchezo huo ambazo zilitarajiwa kuanza kuuzwa tangu jana.

"2020 tunaanza na Yanga. Kama klabu tupo tayari, tupo tayari kwa maandalizi, tupo tayari kwa mchezo," alisema Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mbatha.

Kwa upande wake Ofisa Habari wa klabu hiyo, Haji Manara, alisema: "Sisi tutakuwa wenyeji wa mchezo, nawaomba Wanasimba tununue tiketi mapema na tujitokeze kwa wingi. Lengo letu ni zaidi ya asilimia 70 ya uwanja tuwe sisi Wanasimba.

"Tumewafunga mara nyingi, lakini hatuwezi kuwadharau japo sisi tumewazidi. Tunakwenda kupambana kutafuta alama tatu kama ilivyokuwa mechi ya jana [juzi] dhidi ya Ndanda."

Kwa upande wa wapinzani wao, Yanga ambao wameongezewa wigo katika safu ya ushambuliaji baada ya TFF kumaliza sakata la mshambuliaji, Ditram Nchimbi kwa kuwapo mvutano kati ya Polisi Tanzania alipokuwa akicheza kwa mkopo na klabu yake mama ya Azam FC iliyomuuza Yanga, wamewaahidi wachezaji wake donge nono endapo watamuua 'Mnyama' hiyo Jumamosi.

"Shukrani sana kwa wadhamini wetu Brand Chapa Gsm @gsmtanzania kwa kumruhusu kuichezea timu hiyo baada ya motisha...GSM wameweka tena mezani ahadi ya shilingi milioni hamsini taslimu (50,000,000/=) kwa ajili ya motisha wa kupata pointi tatu dhidi ya Simba SC...Tukutane Jumamosi Uwanja wa Taifa," ilieleza taarifa ya klabu hiyo jana.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >